Nipashe
Jumanne Novemba 26, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0580085
www.ippmedia.com
nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710



## Magufuli awatangazia neema askari JWTZ, wakazi Dodoma

UKURASA 3




UKURASA 13

# Mhadhiri akiri kortini kuomba rushwa ngono

**AHUKUMIWA**, hakimu atoa onyo kukithiri kwa vitendo hivyo, ataka...

*Endelea ukurasa wa 2*

## YALIYOMO

**UKURASA WA 2**

**TRA YAKUSANYA TRI. 58.3/- MIAKA MINNE YA MAGUFULI**
MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA) katika kipindi cha miaka minne imeongeza mapato yake...

**UKURASA WA 4**

**ONGEZEKO WATU LAWEKA UHIFADHI NJIA PANDA-2**
KATIKA sehemu ya kwanza ya ripoti hii jana, ilielezwa hali halisi ya ongezeko la watu nchini...

## WATU 200 WAPATA VVU KILA SIKU NCHINI

UKURASA 3



Mkazi wa Kijiji cha Tandala, Wilaya ya Chemba, mkoani Dodoma, Aisha Khalifa akichota maji ya kisima kwa ajili ya matumizi ya nyumbani kijijini hapo, jana. PICHA NDOGO: Mwanafunzi Mzilifa Abuu wa darasa la pili katika Shule ya Msingi Tandala, akichota maji kisimani hapo, kitendo ambacho ni hatari kwa usalama wake. Kijiji hicho, kinakabiliwa na changamoto ya majisafi ya matumizi ya nyumbani. .**PICHA: IBRAHIM JOSEPH**


Scan Hapa
Fungua App ya QR code Reader kisha scan kupakua APP yetu
Google Play · App Store

## Wapinzani wacharuka nembo kutumika uchaguzi wa mitaa

UKURASA 2

**MICHEZO** KENYA YAWANYIMA KILI QUEENS REKODI UK. 32 · MAONI, KATUNI UK.6

HABARI KITAIFA

# Mhadhiri akiri kortini kuomba rushwa ngono

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam, imemhukumu mhadhiri wa Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT), Samson Mahimbo (69), kulipa faini ya Sh. milioni tano au kwenda jela miaka mitatu baada ya kukiri kuomba rushwa ya ngono.

Hata hivyo, Mahimbo ameshalipa faini ya Sh. milioni mbili kati ya tano baada ya kuingia makubaliano na Mkurugenzi wa Mashtaka Nchini (DPP).

Hukumu hiyo ilisomwa jana na Hakimu Mkazi Mkuu Huruma Shaidi, baada ya mshtakiwa kuandika barua ya kukiri kosa kwa DPP dhidi ya kesi ya uhujumu uchumi namba 80/2019.

Hakimu alisema tabia ya rushwa ya ngono imekithiri na ni gumzo katika vyuo nchini na kwamba inapaswa kukemewa.

"Kuonyesha majibu ya mtihani watoto tunapata wataalamu wasiokuwa na viwango vinavyostahili. Njia sahihi watu kama wewe mshtakiwa ni kukomesha vitendo kama hivyo kwa kuwafikisha mahakamani na kuwapatia adhabu chungu. Utalipa faini ya Sh.milioni tano au kwenda jela miaka mitatu," alisema Hakimu Shaidi wakati akisoma hukumu hiyo.

Hakimu alisema kitendo alichofanya ni cha

INAENDELEA UK 8



Naibu Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Msafiri Mbibo, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu mafanikio ya mamlaka hiyo, katika kipindi cha miaka minne ya uongozi wa serikali ya awamu ya tano. **PICHA: MIRAJI MSALA**

SSF
SUPER STAR FORWARDERS

KUPOTEA KWA KADI ZA MAGARI

**SUPER STAR FORWARDERS CO. LIMITED** inatangaza kupotelewa na kadi za magari zenye namba za usajili **T 534 BCP SCANIA TRUCK** yenye Chassis **No. 9BSP6X20003615601.** Engine namba 8096790 iliyoripotiwa kwa **RB No. DAR/BUG/RB/494221/2019. T 566 BCP SCANIA TRUCK** yenye **Chassis No. 3613621. Engine No. 8094761** iliyoripotiwa kwa **RB No. DAR/BUG/RB/494234/2019.** T 695 AGF DOLL TRAILER yenye Chassis No. 9996 iliyoripotiwa kwa **RB No. DAR/BUG/RB/494230/2019.**
T **937 AEC DOLL TRAILER** yenye **Chassis No. 1063** iliyoripotiwa kwa RB No. **DAR/BUG/RB/494227/2019.**

Yeyote atakayeziona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

## Wapinzani wacharuka nembo kutumika uchaguzi wa mitaa

**Na Waandishi Wetu**

VYAMA vitatu vya upinzani vilivyojitoa katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, vimeeleza kukerwa na kutumika kwa nembo zake kwenye karatasi za kupigia kura.

Vimedai hatua hiyo ni ukiukaji wa uamuzi wake wa kujitoa kushiriki katika uchaguzi huo na kulazimisha ushiriki wake.

Vyama hivyo ni Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Chama cha Wananchi (CUF) na ACT-Wazalendo.

Matokeo yaliyotangazwa jana kwenye maeneo mbalimbali, yalionyesha CUF kushinda kwenye kijiji kimoja na mtaa mmoja, huku kikipata viongozi katika vitongoji vitano.

Akizungumza na Nipashe jana, Mkurugenzi wa Habari na Mawasiliano wa CUF, Abdul Kambaya, alidai kuna ujanja mwingi uliofanywa na Chama Cha Mapinduzi (CCM) kuonyesha kuwa uchaguzi huo ulihusisha vyama vya upinzani.

Alidai baadhi ya mbinu hizo ni majina ya wagombea wa upinzani kubakishwa kwenye karatasi kwa nguvu baada ya ofisi za watendaji waliopaswa kupokea barua zao za kujitoa kufungwa.

Alidai eneo la Rubondo, chama chao hicho kimeshinda kwenye kijiji kimoja ambacho licha ya kujitoa, wananchi walimpigia kura mgombea wa chama hicho na kuibuka mshindi kwa kura 620 dhidi ya 400 za mgombea wa CCM.

"Msimamo wa CUF uko palepale, kuwa tulijiondoa kwenye uchaguzi huo, hatukuwa na wagombea, kwa aliyeshinda na uchaguzi wa wananchi ni matokeo ya wananchi na waliyemchagua, hatuwezi kumfukuza maana aliandika kujitoa na wananchi walimchagua," alisema.

Katibu Mwenezi wa ACT-Wazalendo, Ado Shahibu, alisema msimamo wa chama hicho

INAENDELEA UK 8

## TRA yakusanya tril. 58.3/- miaka minne ya Magufuli

**Na Romana Mallya**

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA) katika kipindi cha miaka minne imeongeza mapato yake na kufikia Sh. trilioni 58.3.

Naibu Kamishna Mkuu wa TRA, Msafiri Mbibo, aliyasema hayo jana wakati akizungumzia mafanikio ya miaka minne tangu Rais John Magufuli aingie madarakani, na kueleza kuwa katika kipindi cha miaka minne kabla ya hapo, TRA ilikusanya Sh. trilioni 34.97.

"Mwaka 2015/16 mapato yalikuwa Sh. trilioni 12.5, 2016/17 yaliongezeka na kufikia Sh. trilioni 14.4, mwaka 2017/18 yalikuwa Sh. trilioni 15.5 na mwaka 2018/19 yaliongezeka zaidi na kufikia Sh. trilioni 15.9 hivyo kufanya mapato kwa miaka minne kufikia Sh. trilioni 58.3," alisema.

Akilinganisha na miaka minne kabla ya utawala la Rais Magufuli, Mbibo alisema mwaka 2011/12 TRA ilikusanya Sh. trilioni 6.76, mwaka 2012/13 zilikusanywa Sh. trilioni 7.88, mwaka 2013/14 Sh. trilioni 9.52 na mwaka 2014/15 ilikusanywa Sh. trilioni 10.81.

"Kwa miaka minne, TRA imekusanya wastani wa Sh. trilioni 1.3 ikilinganishwa na wastani wa Sh. bilioni 850 kabla ya awamu ya tano. Kuanzia Julai hadi Oktoba 2019/20 wastani wa makusanyo umepanda hadi kufikia Sh. trilioni 1.45 kwa mwezi," alisema.

Alisema ongezeko hilo linatokana na sababu mbalimbali ikiwamo kuimarishwa matumizi ya mashine za kieletroniki za kutokea risiti (EFD), kuongezeka kwa mizigo kutoka nje ya nchi inayopitia bandari ya Dar es Salaam na udhibiti wa makusanyo ya bidhaa zinazopaswa kulipa kodi.

Mbibo alisema wamefanikiwa kuanzisha mfumo wa stempu za kodi za kielektroniki (ETS) ambazo ni mbadala wa za karatasi.

Alisema utekelezaji wa mfumo huo kwenye eneo la pombe kali na mvinyo katika kipindi cha mwezi Februari hadi Oktoba

INAENDELEA UK 8

## HABARI KITAIFA

# JPM atangazia neema askari JWTZ

**Na Elizabeth Zaya**

RAIS John Magufuli ameiagiza Wizara ya Fedha na Mipango, kufuta deni la zaidi ya Sh. trilioni moja za pango wanazodaiwa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) katika zaidi ya nyumba 6,000 wanazoishi wanajeshi nchi nzima.

Pia amemwagiza kuwalipa fidia wananchi wa kijiji cha Chololo kuanzia Desemba Mosi, mwaka huu.

Rais Magufuli alitoa agizo hilo jana jijini Dodoma wakati akiweka jiwe la msingi la ujenzi wa makao makuu ya Jeshi la Ulinzi la Wananchi Tanzania (JWTZ) katika eneo hilo lililoko kata ya Kikombo.

Alisema deni hilo litalipwa na serikali na si wanajeshi tena, huku akiagiza nyumba zote wanazoishi kutolipiwa kodi hiyo tena. Alisema serikali ilifanya makosa kutia saini mkataba wa kuwakata pesa wanajeshi katika nyumba za serikali na kusisitiza halitajirudia.

"Ni kweli kabisa serikali tulitia saini mkataba huo. Kwa wakati ule nafikiri ni mwaka 2012/13, ilikuwa kwamba nyumba zikijengwa, wanajeshi wanakatwa. Nimeshazungumza na Waziri na leo (jana) CDF (Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi) naye amezungumza hapa. Huwezi kumchukua askari ambaye anakaa kwenye maeneo ya kiaskari ambayo ni kama mahanga halafu uanze kumtoza pesa," alisema.

"Nafahamu deni hilo ni fedha nyingi sana lakini nataka kukuhakikishia CDF kwamba katika nyumba zote zilizojengwa nchi nzima ambazo mkataba wake ulisema wanajeshi wakatwe, hakuna kukatwa askari yeyote. Hilo deni litabebwa na serikali.

"Kabla sijaja hapa nimeshamwelekeza Waziri wa Fedha (na Mipango) na Katibu Mkuu, nafikiri kesho (leo) au keshokutwa (kesho) deni hilo litaanza kulipwa kwa kuanza kulipa Dola milioni 25. Siwezi nikawaweka askari wangu kwenye utumwa wa nyumba za kulala.

"Badala ya kulala anaota namna ya kupiga risasi, anaanza kuota namna ya kulipa deni la nyumba. Kwa wakati wangu hilo hapana, mkataba ni kweli ulikosewa lakini siwezi kukubali makosa ya namna hiyo yakaanza kufanyika katika kipindi changu," alisisitiza.

Akifafanua suala hilo, Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi, Jenerali Venance Mabeyo, alisema askari hao walikuwa wakikatwa kupitia mfumo wa 'Ngome Allowance' jambo ambalo hakubaliani nalo.

**KASI UJENZI**

Rais Magufuli aliahidi kutoa Sh. bilioni 10 kwa jeshi hilo kwa ajili ya kuanza mara moja ujenzi wa baadhi ya majengo yenye umuhimu katika mradi huo wa ujenzi wa jengo la makao makuu hayo ya ulinzi wakati wanasubiri pesa nyingine.

"Wakati tukijiandaa kujenga makao makuu, hatuwezi kusubiri watu kutujengea makao, mimi nitatoa Sh.bilioni 10 ili muanze kujenga na kushughulikia maeneo mengine mnayoona mtaanza nayo," alisema.

Rais aliagiza Wakala wa Barabara (Tanroads) kufikia wiki ijayo iwe imeanza ujenzi wa barabara ya kutoka njiapanda ya Chamwino hadi yanapojengwa makao makuu ya jeshi yenye kilomita 18 kwa kiwango cha lami.

"Hapa ni makao makuu, lazima pawe na sura ya makao makuu. Huwezi kuwa unakuja makao makuu halafu barabara ni ya changarawe tu, haiwezekani. Kama Amiri Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama, natoa amri kwa Meneja wa Tanroads na namna ukamweleze waziri, wiki kesho mtangaze rasmi tenda ya ujenzi wa kilomita zote 18 kwa kiwango cha lami, tena utangaze tenda wiki kesho," alisema.

Jenerali Mabeyo pia alisema serikali ya China imekubali kusaidia pia katika ujenzi wa makao makuu ya jeshi hilo na kwamba China ilituma timu ya wataalamu kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu na kwamba kwa sasa wanafanya usanifu.

Alisema kukamilika kwa ujenzi wa makao makuu hayo kutaweka mazingira bora ya kazi kwa jeshi hilo.

**NEEMA CHOLOLO**

Rais Magufuli pia alimwagiza Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma, kuanza kuwalipa fidia wananchi wa kijiji cha Chololo ambao wamepisha ujenzi wa makao hayo makuu ya jeshi.

Awali, Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Dk. Hussein Mwinyi, alisema Sh. bilioni 3.399 zinahitajika kwa ajili ya kulipa fidia hiyo kwa wananchi 1,509.

Pia alishauri kuangalia uwezekano wa kuwapimia wananchi hao walioondolewa viwanja vya bei nafuu kwa ajili ya kujenga nyumba pia kuangalia uwezekano wa kuwapimia maeneo mengine ikiwezekana kwa bei nafuu.

Dk. Mwinyi alisema tayari fedha hizo zilishatengwa na kusainiwa kwa ajili ya malipo ya fidia hiyo.

Pamoja na kuagiza walipwe fidia, Rais Magufuli aliwatahadharisha wananchi hao wenye sifa ya kulipwa fidia kuacha tabia ya kubadilisha fidia zao pamoja na kurubuniwa na wenyeviti na watu wanaojiita watetezi wao.

"Nataka nitoe wito kwa wananchi wanaostahili kulipwa fidia, wasianze kubadilisha fidia, kuna baadhi ya watu wanapita kwenye maeneo yenu na wengine wanajiita wenyeviti kwa ajili ya kuwatetea, ni matapeli achaneni nao. Mtetezi wenu ni Jamhuri tu, kila eneo la ardhi katika nchi hii lina thamani yake," alisema.

"Thamani ya ardhi ya hapa huwezi kuilinganisha na ya Osterbay au katikati ya mji wa Dodoma, Mzakwe au Milembe na sehemu nyinginezo, msidanganywe. Kila sehemu ina thamani yake, msidanganywe na matapeli."

Rais Magufuli aliwataka wananchi kuchangamkia fidia hizo pindi tu zitakapoanza kutolewa na kwamba yeyote atakayechelewa kuchukua katika kipindi hicho asilalamike.

**FURSA MAKANDARASI**

Akizindua jengo la makao makuu ya Bodi ya Usajili wa Makandarasi (CRB), Rais Magufuli aliwataka kuchangamkia fursa mbalimbali ambazo zinatangazwa na serikali.

"Ninawaomba mjitahidi kuchangamkia tenda, hiki ndiyo kipindi cha kufanya kazi kwa sAbabu ni nyingi. Mkishindwa katika kipindi hiki hamtazipata tena, hili nawahakikishia," alisema.



Rais John Magufuli akiwa na Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), Dk. Hussein Mwinyi (wa tatu kulia) na Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi, Jenerali Venance Mabeyo, wakipata maelezo kuhusu ujenzi wa Uwanja wa Maadhimisho ya Taifa, eneo la Chamwino jijini Dodoma jana. **PICHA: IKULU**

# 200 waambukizwa VVU kila siku

**Na Mwandishi Wetu, DODOMA**

ZAIDI ya Watanzania 200 wanaambukizwa Virusi vya Ukimwi (VVU) kila siku, hivyo kufanya idadi ya maambukizo kuwa watu 72,000 kwa mwaka.

Hayo yalielezwa juzi jijini Dodoma na Mkurugenzi Mtendaji wa Tume ya Kudhibiti Ukimwi (Tacaids), Leonard Makobo, alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu maadhimisho ya Siku ya Ukimwi Duniani.

Maadhimisho hayo mwaka huu yamepangwa kufanyika kitaifa jijini Mwanza.

Alibainisha kuwa takwimu zinaonyesha vijana wenye umri wa kati ya miaka 14 na 24 ndiyo wanaongoza kwa maambukizo, wakichukua asilimia 40 ya maambukizo mapya.

"Kwa kuzingatia kwamba takriban watu 200 wanaambukizwa VVU kila siku, 80 ni kutoka kundi hilo la vijana," alisema.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu(Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana, na Watu Wenye Ulemavu), Jenista Mhagama, alisisitiza kuguswa na suala hilo, akieleza kuwa ni lazima hatua zichukuliwe kukabiliana na kasi hiyo ya maambukizo kwa vijana.

Alisema Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, anatarajiwa kuwa mgeni rasmi katika maadhimisho ya Siku ya Ukimwi Desemba Mosi, mwaka huu kwenye Viwanja vya Furahisha jijini Mwanza.

Alisema kuwa katika kuadhimisha siku hiyo, jitihada zitawekwa katika kutoa elimu na kampeni ya kujitambua kwa vijana, ikiwa ni sehemu ya mikakati ya maambukizo mapya dhidi ya kundi hilo.

Alisema kuelekea siku hiyo, kutakuwa na shughuli mbalimbali, zikiwamo za upimaji wa hiari wa VVU na utoaji wa huduma za ushauri nasaha.

HALMASHAURI YA MJI WA BABATI

TANGAZO

MKURUGENZI WA MJI WA BABATI, ANAWATANGAZIA WANANCHI WOTE WALIOPEWA VIWANJA NA HALMASHAURI YA MJI WA BABATI, KUWA WANATAKIWA KUKAMILISHA MALIPO YA VIWANJA NDANI YA KIPINDI CHA MWEZI MMOJA (SIKU 30) KUANZIA SIKU YA TANGAZO HILI. VIWANJA HIVYO NI VILE AMBAVYO HAVIJAENDELEZWA NA PIA HAVIJALIPIWA KABISA, AU VIMELIPIWA NUSU KATIKA KIPINDI CHA MIAKA MITATU.

HALMASHAURI IMEDHAMIRIA KUWANYANG'ANYA VIWANJA WATU WOTE AMBAO HAWATATEKELEZA AGIZO HILI KATIKA KIPINDI KILICHOPANGWA. FEDHA KIDOGO AMBAZO ZILISHALIPWA HAZITAREJESHWA.

ORODHA YA MAJINA YA WATU WANAODAIWA IKO KWENYE TOVUTI YA HALMASHAURI YA MJI WA BABATI:
www.babatitc.go.tz


TANGAZO HILI LIMETOLEWA NA MKURUGENZI WA MJI WA BABATI.

215531592

RIPOTI MAALUM

# Ongezeko la watu linavyoiweka sekta uhifadhi, utalii njia panda

■ Makazi yawekwa shoroba kongwe




Mchoro unaoonesha ongezeko la watu nchini. **Chanzo: Takwimu za NBS**

**Na Sanula Athanas**

***KATIKA sehemu ya kwanza ya ripoti hii jana, ilielezwa hali halisi ya ongezeko la watu nchini, uamuzi wa serikali kuhalalisha rasmi vijiji vilivyomo ndani ya hifadhi na mtazamo wa Rais mstaafu Benjamin Mkapa kuhusu kasi ya ongezeko la watu nchini. Endelea kufuatilia sehemu ya pili ya ripoti hii:***

INGAWA wingi wa watu kwa upande mmoja ni mtaji wa nguvu kazi na wigo wa soko katika jamii, upande wa pili una mtazamo hasi kwamba una madhara kwa baadhi ya sekta, ikiwamo utalii na uhifadhi.

Wizara ya Maliasili na Utalii inabainisha kwamba sekta hiyo inachangia asilimia 17.5 ya Pato la Taifa, ikiipatia nchi asilimia 25 ya fedha zote za kigeni na kutoa ajira za moja kwa moja 600,000 na nyinginezo zaidi ya milioni mbili.

Sekta ya Utalii na Uhifadhi inajumuisha hifadhi za taifa 22 zilizo chini ya Shirika la Hifadhi za Taifa (Tanapa) liliolanzishwa kisheria mwaka 1959.

Maeneo yake mengine ni Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, yenye ukubwa wa kilomita za mraba 8,292, mapori ya akiba 28, yenye kilomita za mraba 114,782.47 na mapori tengefu 42, yenye ukubwa wa kilomita za mraba 58,565.02.

Tanzania pia ina hifadhi zenye hadhi ya kimataifa zilizowekwa kwenye orodha ya Urithi wa Dunia, ambazo ni: Pori la Akiba Selous; Hifadhi ya Taifa Serengeti; Hifadhi ya Taifa Kilimanjaro (Kinapa); Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro na Hifadhi ya Taifa ya Ziwa Manyara.

Licha ya umuhimu wake, ikiwamo kuliingiza taifa fedha nyingi za kigeni, maeneo mengi ya hifadhi kwa sasa yamevamiwa na watu wanaotafuta ardhi ya makazi na shughuli za uchumi, sambamba na uharibifu wa njia za wanyamapori, maarufu shoroba.

Miaka minane iliyopita, Michael Graham, mtaalamu wa sayansi, alieleza kuwa ongezeko la watu duniani ni tatizo kwa shoroba nyingi kwa sababu linaongeza shughuli za kibinadamu kwenye maeneo hayo muhimu kwa wanyamapori.

Alisema shoroba na maeneo ya mtawanyiko husaidia kupata kizazi imara cha wanyama. Maoni ya mtaalamu huyo ni kwamba, wanyama wanapofungiwa sehemu moja, huzaana ndugu, hali inayojenga urahisi wa kushambuliwa na magonjwa yanayowazunguka.

Graham alifafanua umuhimu wa wanyama kuhama kutoka hifadhi moja kwenda nyingine kuwa ni nyenzo ya kuhamisha vinasaba vinavyotengeneza makuzi bora na endelevu. Pia, kunaondoa uwezekano wa wanyama kuzaana ndugu.

Kwa mujibu wa mtaalamu huyo, duniani kuna shoroba za asili na za kutengenezwa, zikilenga kuruhusu wanyamapori waendelee kuwapo na kukamilisha ikolojia ya maeneo yaliyohifadhiwa.

Aliainisha kwamba viumbe hulazimika kutembea umbali mrefu kupata mahitaji lishe kama vile madini, jambo linaloendeleza utetezi wa kuwapo shoroba za viumbe hivyo.

Licha ya mtazamo huo wa kitaalamu, Nipashe imebaini kuwapo shughuli za maendeleo ya umma kwenye shoroba zinazokinzana na kanuni za maendeleo na usimamizi wa utalii na wanyamapori.

Imegundulika maeneo mengi ya shoroba yamejengwa makazi ya watu yakienda sambamba na shughuli za kilimo na ufugaji.

Vilevile, imebainika hata usajili wa baadhi ya vijiji unaofanywa na mamlaka za kiserikali katika baadhi ya maeneo, umekiuka taratibu na mwongozo unaolinda na kuhifadhi shoroba za wanyamapori na mengine muhimu yanayoathiri utalii na uhifadhi.

Mfano hai wa ushuhuda wa Nipashe, ni katika ushoroba wa Simanjiro mkoani Manyara ambako kuna vijiji vitano vilivyosajiliwa huku vikiingilia mpaka wa Hifadhi ya Taifa ya Tarangire.

**WANACHOKIONA WATAALAMU**

Mkurugenzi wa Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori (Tawa), Dk. James Wakibara, anakiri kuwapo uvamizi wa shoroba, ambao pia serikali ina mkono wake katika ujenzi wa miundombinu yake.

Dk. Wakibara anafafanua kwamba, kuna majengo makubwa katika baadhi ya maeneo ya shoroba, yanayohusu utoaji wa huduma za kijamii kama vile shule, vyuo, vituo vya afya, hospitali na miundombinu ya barabara, umeme na maji, mmiliki wake mkuu ni serikali.

Anatoa mifano ya Halmashauri za Mvomero na Rombo zilizojenga ofisi kwenye mapito ya wanyamapori. Anasema ni sababu ya wanyama kama tembo kuonekana kila mara kwenye maeneo hayo.

Pia, kwa kurejea mnamo Mei 2017, tembo wanne walionekana katika mandhari ya Chuo Kikuu cha Dodoma (Udom).

Wataalamu wa sekta hiyo walitolea ufafanuzi kwamba, walikuwa katika mapito yao kwa kuwa wanyama hao hukumbuka njia walizopita hata kwa miaka 100.

Mkurugenzi wa Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori (Tawiri), Dk. Emmanuel Lyimo, anaeleza kwamba, bila kuhifadhi na kutunza maeneo ya mtawanyiko wa wanyama, hatari iliyoko mbele ya safari ni taifa kubakiwa na hifadhi mbili tu kufikia mwaka 2050, anazozitaja kuwa ni Pori la Akiba Selous na Hifadhi ya Taifa Ruaha.

Anatoa ufafanuzi wa hoja yake kwamba, kinachoziponya ni kuzungukwa na maporomoko ya maji na Mamlaka ya Kihifadhi za Jamii (WMAs), ambazo shughuli za utunzaji wa maeneo husika hufanywa kisheria, hivyo kunusuru maeneo ya mtawanyiko wa wanyamapori.

Dk. Lyimo anatahadharisha kuendelea kuvamiwa na kuendelezwa kwa maeneo hayo ya mtawanyiko, kiuchumi mapato yatokanayo na utalii yatapungua maradufu kwa kuwa wageni watakosa wanyama wa kuangalia.

Asasi ya Kibunge Inayojihusisha na Idadi ya Watu na Maendeleo (TPAPD), ina maoni kwamba, bila hatua madhubuti kuchukuliwa kuikabili hali iliyopo, idadi ya watu nchini itafika milioni 130 mwaka 2050, ikiwa ni zaidi ya mara mbili ya idadi ya sasa.

Katika tamko lake la Machi 8, 2017 jijini Dar es Salaam kwenye maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Wanawake, kiongozi wake, Mary Mwanjelwa, alihimiza umuhimu wa kipaumbele katika uzazi wa mpango ili kukabiliana na ongezeko la watu, ambalo sasa ni asilimia 2.7 kwa mwaka.

"Uzazi wa mpango unahitajika katika kuiwezesha nchi kukabiliana na kasi ya ongezeko la idadi ya watu inayochangiwa na uzazi wa kiwango cha wastani wa watoto watano kwa kila mwanamke aliye katika umri wa uzazi.

"Hali hii huchangia utegemezi pamoja na umaskini na pia hudumaza juhudi za taifa za kufikia malengo ya maendeleo," kiongozi huyo alisema.

Mhadhiri Msaidizi katika Chuo cha Ustawi wa Jamii, Zainab Rashid, anataja madhara ya ongezeko la watu nchini yanajumuisha uharibifu wa mazingira na uvamizi wa maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya hifadhi za misitu na wanyamapori.

Zainab anataja madhara hayo, ni tofauti na yaliyozoeleka ya kutotosheleza kwa huduma muhimu za kijamii kama vile maji, elimu na afya.

"Kwa kadri idadi ya watu inavyoongezeka, ndivyo mahitaji ya ardhi yanavyoongezeka. Kwa hiyo, umaskini huja kwa kasi kwa sababu rasilimali zinakuwa hazitoshelezi kukidhi mahitaji hayo na mwisho wa siku, huishia katika uharibifu wa mazingira na kuvamia maeneo yaliyohifadhiwa.

"Elimu kuhusu uzazi wa mpango itolewe, ili jamii iachane na imani potofu. Mfano, mtu anataka apate watoto wa kiume tu! Watu waridhike na watoto walio nao, kwa sababu watoto wote ni sawa," anashauri.

Ni kauli inayoungwa mkono na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, inayoeleza haja ya serikali kuwekeza katika elimu ya uzazi wa mpango, kama njia ya kukabili kasi ya ongezeko la watu nchini.

Mwenyekiti wake, Peter Serukamba, anadokeza kamati yake imebaini kwamba, baada ya miaka 81 ijayo, Tanzania itakuwa nchi ya saba duniani na ya pili barani Afrika kwa idadi kubwa ya watu.

Serukamba anaeleza kuwapo ongezeko la takribani watu milioni moja kila mwaka nchini, akilitafsiri ni wastani wa watoto watano kwa kila mwanamke aliye katika umri wa uzazi.

"Kamati inatoa rai kwa viongozi wote wa nchi, wakiwamo wa kisiasa, kidini na hata kimila, kulizungumzia suala hili kwa nia njema kabisa ili kuwa na taifa imara na bora na lenye idadi ya watu inayoendana na rasilimali zilizopo," anashauri.

Mkurugenzi wa Sensa ya Watu na Takwimu za Jamii wa NBS, Ephraim Kwesigabo, anataja pande mbili za manufaa na hasara zinazotokana na ongezeko la watu nchini.

Angalizo lake ni nchini Tanzania, kwamba kasi ya ukuaji wa uchumi haiwiani na ongezeko kubwa la watu, hivyo upatikanaji wa huduma za kijamii unakuwa duni.

Mkurugenzi anatahadharisha: "La sivyo, huduma kama za afya, shule, ardhi na huduma nyingine haziwezi kutosheleza mahitaji. Watu lazima wanyang'anyane.

"Hili linawezekana zaidi katika nchi ambazo uchumi wake ni mara mbili au mara tatu ya Tanzania, lakini kwenye nchi kama hizi zetu, si rahisi kuendana na kasi hiyo.

"Watu wanaongezeka na matumizi yanaongezeka, lakini ardhi haiongezeki. Zipo athari nyingi sana za kijamii zinazosababishwa na ongezeko la watu; kukosekana kwa ajira, ongezeko kubwa la watu mijini na kuzalisha ombaomba."

* ITAENDELEA KESHO



Mafundi wakiendelea na ujenzi wa machinjio ya kisasa ya Vingunguti, jijini Dar es Salaam jana. Kwa mujibu wa mkandarasi anayesimamia ujenzi huo, Wakala wa Nyumba (TBA), hadi kufikia mwezi Desemba mwaka huu, watakuwa wameezeka paa la machinjio hayo. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# TFS yatoa gawio bil. 25 kwa serikali

**Na Mwandishi Wetu**

WAKALA wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) umetoa gawio la Sh. bilioni 24.891 kwa serikali kutokana na makusanyo yake kwa mwaka 2018/2019.

Akizungumza jijini Dodoma jana, baada ya makabidhiano ya hundi ya gawio hilo, Kamishna Mhifadhi wa Misitu, Prof. Dos Santos Silayo, alisema Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri TFS, Brigedia Jenerali Mkeremy, alikabidhi mfano wa hundi kwa Rais John Magufuli wakati wa hafla ya upokeaji gawio, michango na ziada kutoka mashirika na taasisi za umma iliyofanyika Ikulu, Chamwino.

Prof. Silayo alisema mchango huu unatokana na makusanyo ya TFS kwa mwaka 2018/19, akibainisha kuwa wakala ulipanga kuchangia Sh. bilioni 18.39 kwa mujibu wa Sheria ya Fedha za Umma Na. 6 ya Mwaka 2001, lakini umefanikiwa kuchangia Sh. bilioni 24.891, ikiwa ni ziada ya Sh. bilioni 6.5.

"Tumetoa gawio la Sh. bilioni 24.891 mwaka huu, gawio hili limeifanya TFS kuwa miongoni mwa taasisi sita bora kati ya 79 zilizochangia na kutunukiwa cheti cha uchangiaji bora kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali," Prof. Silayo alisema.

Aliwashukuru wafanyakazi wote wa TFS, uongozi wa Wizara ya Maliasili na Utalii chini ya Waziri Hamis Kigwangalla, Bodi ya Ushauri ya TFS na wajumbe wote kwa uchapakazi na uongozi thabiti uliowezesha TFS kukusanya na hatimaye kuwasilisha sehemu ya mapato yake kwa serikali.

"Niwatake wafanyakazi wote kuendelea kufanya kazi kwa bidii ili wakala uendelee kuwa kielelezo bora katika usimamizi endelevu wa rasilimali za kitaifa za misitu na nyuki ili kuchangia mahitaji ya kijamii, kiuchumi, kiikolojia na kiutamaduni kwa kizazi cha sasa na kijacho," alisema.

Hiyo ni mara ya pili kwa TFS kutoa gawio kwa serikali. Katika mwaka wa 2017/18, wakala huo ulichangia Sh. bilioni 22.41 kwa serikali kama gawio.

**"Niwatake wafanyakazi wote kuendelea kufanya kazi kwa bidii ili wakala uendelee kuwa kielelezo bora katika usimamizi endelevu wa rasilimali za kitaifa za misitu na nyuki ili kuchangia mahitaji ya kijamii, kiuchumi, kiikolojia na kiutamaduni kwa kizazi cha sasa na kijacho," alisema.**

# NMB yapewa mchongo wa biashara madini

**Na Mwandishi Wetu, DODOMA**

BENKI ya NMB imeshauriwa kutumia fursa za kibiashara zilizopo katika sekta ya madini zinazowalenga wachimbaji wadogo na wa kati ikiwamo kujifunza biashara ya madini inavyofanyika.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Madini, Prof. Simon Msanjila, alitoa rai hiyo wakati wa kikao baina yake na ujumbe wa wataalamu kutoka benki hiyo ulioongozwa na Mkuu wa Idara ya Uhusiano na Serikali ya Benki hiyo, Vicky Bishubo. Kikao hicho kimefanyika jana jijini hapa.

Prof. Msanjila alitoa ushauri huo kwa benki hiyo kutokana na juhudi za serikali kupitia Wizara ya Madini zinazolenga kuwapatia elimu wachimbaji ikiwamo kutunza kumbukumbu za uzalishaji, kufanya utafiti ili kujua kiasi cha mashapo kupitia Wakala wa Jiolojia Tanzania (GST) na Shirika la Madini la Taifa (Stamico) yanayolenga kuwawezesha wachimbaji kukopesheka na taasisi za fedha.

Pia Prof. Msanjila aliitaka benki hiyo kutumia fursa zilizopo katika masoko ya madini yaliyoanzishwa katika mikoa mbalimbali ili kurahisisha biashara ya madini na kutolea mfano wa soko la madini Arusha kwamba benki hiyo haina huduma katika soko hilo, huku biashara ya madini sokoni hapo ikifanyika kwa kiasi kikubwa.

Prof. Msanjila aliitoa wasiwasi benki hiyo kuwa hivi sasa biashara za madini zinafanyika katika mfumo wa wazi tofauti na ilivyokuwa awali na kuongeza kwamba: "Kuna biashara nyingi kwenye sekta ya madini. Niwaambie hivi karibuni serikali ya Qatar itaanza kununua dhahabu moja kwa moja kutoka Geita."

"Sekta ya madini haijatumiwa vizuri na benki, ninawakaribisha kwenye sekta hii. Pale Arusha ndipo mji pekee wa ukataji madini ya vito. Mwende mkaliangalie hili," alisisitiza.

Naye Bishubo alimshukuru Prof. Msanjila kwa kueleza fursa zilizoko katika sekta husika na kueleza kwamba benki hiyo imeyachukua kwa uzito mkubwa yote yaliyoelezwa na iko tayari kuyafanyia kazi.

"Tumejifunza sekta ya madini inavyofanya kazi. Kuna uwezekano wa sisi kuandaa mfumo wa kuwasaidia wachimbaji wadogo," alisema.

**"Sekta ya madini haijatumiwa vizuri na benki, ninawakaribisha kwenye sekta hii. Pale Arusha ndipo mji pekee wa ukataji madini ya vito. Mwende mkaliangalie hili," alisisitiza.**

KDF Kilimanjaro Development Forum
Today. Tomorrow. Together

P.O Box 32055,
Dar es Salaam, Tanzania
+255 688 591 182
john@stageneraltz.com
www.kilimanjarodevforum.co.tz

**MKUTANO MKUU WA MWAKA WA WANACHAMA**

Wanachama wa KDF wanatangaziwa kwamba kutakuwa na mkutano mkuu wa mwaka wa wanachama wote utakaofanyika tarehe 21, Desemba, 2019 katika ukumbi wa ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Manispaa ya Moshi.

**Agenda:**

1. Kupokea taarifa ya maendeleo ya KDF;
2. Kupokea na kupitia taarifa ya fedha ya KDF;
3. Kuchagua maafisa wa KDF na wajumbe wa bodi ya uongozi;
4. Kuteua wakaguzi na wadhamini au kuwathibitisha wanaoendelea;
5. Kupanga michango/ada za mwaka unaofuata, na
6. Kupitia na kupitisha marekebisho ya katiba.

**Uchaguzi wa viongozi katika nafasi zifuatazo;**

1. Mwenyekiti
2. Makamu Mwenyekiti
3. Katibu
4. Naibu Katibu
5. Mweka Hazina
6. Mweka Hazina Msaidizi

**Maombi ya kugombea nafasi hizi yatumwe kwa anwani zifuatazo:**

**Dr. Jonas Kipokola,**
**Katibu (KDF),**
**S.L.P 8448, Moshi au barua pepe**
**info@kilimanjarodevelopmentforum.org au piga simu 0754386003**
**Tarehe ya mwisho ya kupokea maombi ya kugombea ni tarehe 7 Desemba, 2019.**

Mkutano Mkuu utafuatiwa na sherehe ya Kilimanjaro Day itakayofanyika siku hiyo hiyo. Umoja wetu ndiyo nguvu ya mafanikio yetu, karibuni sana

**Imetolewa na:**
**Dr. Jonas Kipokola**
**Katibu, Kilimanjaro Development Forum**

615528802

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Gawio ni mapato muhimu serikalini

**RAIS** John Magufuli ametoa miezi miwili kwa viongozi wa mashirika, taasisi na kampuni za umma 187 kutoa gawio kwa serikali na endapo wakishindwa, waondoke wenyewe kwenye nafasi zao.

Kwa utendaji wa Rais Magufuli, ni wazi kwamba kauli yake haitarudi bure. Hapo ndiyo itakapodhihirika kuwa cheo ni dhamana, kwani ni shinikizo la kiutawala litakalowazindua kutoka usingizini, baadhi ya viongozi waliolala.

Tunatambua kuwa pia imewasababishia matumbo joto wale waliokuwa wamejisahau kuwajibika kuhakikisha wanaongoza vyema na kuwezesha taasisi au kampuni hizo zinajiendesha kwa tija na faida.

Rais Magufuli alitoa agizo hilo juzi Ikulu Chamwino jijini Dodoma, alipokea gawio, michango na ziada kwa mashirika, kampuni na taasisi mbalimbali ambazo serikali ina hisa au inazimiliki.

Hiyo si mara ya kwanza kwa Rais Magufuli kupokea gawio, kwani kampuni za simu za TTCL na Airtel. Kampuni zingine ni Puma Energy Tanzania na benki ya CRDB kwa nyakati tofauti zilikabidhi gawio kwa serikali.

Rais Magufuli alieleza kuwa serikali hadi sasa imeshawekeza mtaji wa Sh. trilioni 59.6 kwa mashirika na taasisi 266, ingawa anakiri kuna maeneo ya uwekezaji huo, unakabiliwa na changamoto ya usimamizi na utendaji duni. Alitoa mfano kuwa mwaka 2014/15, serikali ilikusanya Sh. bilioni 130 kutoka mashirika 24 na mwaka 2015/16 zilikusanywa Sh. bilioni 249.3 kutoka taasisi na mashirika 25.

Kutokana na kauli ya Rais Magufuli, tunaamini kuwa kuna ukimya kutoka kwa viongozi wa taasisi hizo, hali ambayo inajenga taswira ya kulegalega kwenda na kazi anayoitaka mkuu huyo wa nchi, ishara mojawapo inayojionyesha kupitia gawio.

Rais alisema tangu aingie madarakani serikali yake imechukua hatua kadhaa ili kuongeza ukusanyaji wa mapato, akitaja mifano: Mwaka 2016/17 zilikusanywa Sh. bilioni 677 kutoka taasisi 38; 2017/18 zilikusanywa Sh. bilioni 842.13 kutoka mashirika na taasisi 40; na mwaka 2018/19 Sh. trilioni 1.05 kutoka taasisi na mashirika 79.

Mapato ya gawio la taasisi, mashirika na kampuni yameongezeka na kufikia Sh. trilioni 1.05. Mashirika na kampuni 81 yaliyotajwa kuwa ni ya kibiashara, kati yao 40 yameshindwa kutoa gawio kutokana na madai ya kujiendesha kwa hasara.

Nasi tunajiuliza maswali kuwa wakati viongozi wa mashirika hayo 266 yaliyochangia ni 79 na serikali imeshawekeza mtaji wa Sh. trilioni 59.6 mengine yanafanya nini? Kwa haya mashirika 187 yaliyobaki, kuna nini wanapowaona wenzao wanawasilisha gawio lao wanawaza nini?

Kwa mujibu wa Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, asilimia 70 ya bajeti ya serikali inategemea makusanyo ya ndani, na nusu ya makusanyo yasiyo ya kodi yanatokana na gawio na michango kutoka kwa kampuni, taasisi, wakala na mashirika ya umma.

Kwa maelezo hayo, tunaweza kutambua jinsi gani gawio ni miongoni mwa vyanzo muhimu vya mapato kwa serikali, ambayo inawajibika kuhakikisha inaboresha upatikanaji wa huduma muhimu kwa wananchi kama maji, elimu, afya, barabara na zingine.

Tunapenda kuwakumbusha kuwa kila zama na nyakati zake, hivyo viongozi wenye dhamana waache kuishi kwa mazoea, badala yake wajitume kuhakikisha wanatumikia majukumu yao ipasavyo, ikiwamo taasisi wanazoziongoza zinatoa gawio kwa serikali kwa wakati mwafaka.

Michango na gawio kwa serikali kama vitatolewa wakati mwafaka, kuna uwezekano wa serikali kujiendesha na kutekeleza miradi mbalimbali badala ya kusubiri washirika wa maendeleo, ambao mara nyingi huchelewa kutekeleza ahadi za kusaidia na wakati mwingine kutotekeleza kabisa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com



## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Kambi za kitaaluma ni ufunguo kufaulu

**KAMBI** za kitaaluma zimekuwa na mchango mkubwa kwa wanafunzi katika kufikia maendeleo ya juu ya elimu kwa kuwawezesha kufanya vizuri kwenye mitihani yao na hivyo kuwa na uhakika wa kusonga mbele kitaaluma.

Wanafunzi ambao huwekwa katika kambi hizo maalum kwenye baadhi ya mikoa ni wale wa shule za msingi na sekondari, lengo likiwa ni kuwafundisha zaidi ili wafaulu.

Kwa kuzingatia hilo, kambi hizo za kitaaluma zinaandaliwa kwa ushirikiano kati ya shule na wadau mbalimbali wa elimu wakiwamo wazazi na walezi, ambao huchangia chakula na fedha.

Michango hiyo inawafanya wawe wadau muhimu kwenye maendeleo ya elimu kwa vile vyakula wanavyochangia na fedha vinatumiwa na watoto wao kambini wanapokuwa wanafundishwa.

Wanafunzi wanaowekwa kambini hupata muda mwingi wa kujifunza na kujisomea, kuchimba na kujiweka kwenye mazingira halisi ya kufanya mitihani.

Hali ambayo kwa namna moja au nyingine inasaidia kuongeza ari ya kupenda elimu na kufaulu.

Mkoa wa Simiyu ni moja ya mikoa iliyobuni kambi hizi kwa kushirikisha wadau mbalimbali na kufanikiwa kuongeza ufaulu kwa wanafunzi wa sekondari mkoani humo na kushika nafasi ya 10 kitaifa.

Nafasi hiyo ni katika matokeo ya mtihani wa taifa wa kidato cha sita mwaka 2018, kutoka nafasi ya 26 mwaka 2017 hadi kufikia ya 10 kwa mwaka jana.

Aidha, mkoa huo unaendelea kuziimarisha kambi hizo. Yapo maeneo mengine ambayo yameiga mfumo huo wa kambi za kitaaluma, lakini ninadhani ipo haja kwa nchi nzima kuutumia mpango huo ili kuwasaidia wanafunzi kupata muda wa kutosha kujiandaa kwa ajili ya mitihani.

Ikumbukwe kuwa katika mazingira ya Tanzania ni wanafunzi wachache ambao hupata nafasi ya kujisomea wanaporudi nyumbani au siku za mwisho wa wiki na wengi hawaipati.

Kutokana na hali hiyo, ipo haja kwa wanafunzi wengine wengi kuwawezesha kuwa na muda wa kutosha kujiandaa na mitihani badala ya kushughulika na majukumu mengine ya nyumbani na kukosa muda wa kujisomea.

Njia ambayo imeonyesha matokeo mazuri ni kuwa na kambi za kitaaluma kwani wanafunzi hukusanywa pamoja na kuwa huko kwa miezi kadhaa hadi siku za mitihani na wanatoka wakiwa wamenolewa kikamilifu.

Siyo vibaya mikoa mingine kuiga kile kinachofanywa na Simiyu chini ya Mkuu wa Mkoa, Anthony Mtaka, ambaye kwa kushirikiana na wadau wa elimu wa mkoa huo, walibuni kambi hizo za kitaaluma.

Najua kuna baadhi ya maeneo hapa nchini ambayo yameanza kuiga mfano huo, lakini ingependeza iwapo nchi nzima ingeiga mfano huo, kwani lengo ni kusaidia kuongeza uelewa na hata ufaulu kwa wanafunzi.

Kama nilivyosema, hali ya maisha inasababisha baadhi ya watoto wasipate nafasi ya kujisomea wawapo nyumbani, na inawezekana hiyo ndiyo ilikuwa sababu ya kuanzisha kwa kambi hizo mkoani Simiyu.

Inaweza kutokea siku za mwisho wa wiki, mwanafunzi anakwenda kuchunga ng'ombe, kulima na shughuli nyingine za nyumbani, hizo zote ni muhimu lakini pia anatakiwa awe na muda wa kujisomea.

Njia bora ambayo imebuniwa na Mkoa wa Simiyu ni hiyo ya kuweka kambi za kitaaluma, ambayo kimsingi ni nzuri, kutokana na ukweli kwamba imekuja na matokeo mazuri, ndiyo maana nikasema mfano huo uigwe.

Hivyo, itapendeza iwapo kambi za kitaaluma zitaenea nchi nzima, jambo la muhimu ni kuwashirikisha wadau hasa wazazi ili wawe tayari kuchanga chochote kwa ajili ya kufanikisha kambi hizo.

Ninaamini kwamba mzazi au mlezi anayejua umuhimu wa elimu atakuwa tayari kuchangia kwa ajili ya kusaidia kuinua kiwango cha elimu cha mtoto wake ili aweze kusonga mbele katika masomo ya juu.

Elimu ni ufunguo wa maisha, ni mali, akiba na ina haina mwisho, kwa kuona jinsi ilivyo ya muhimu kwa mwanadamu ndiyo maana wale wanaowakwamisha wanafunzi masomo huchulikuwa hatua za kisheria.

Hivyo, mikoa ambayo bado haijaamua kuandaa kambi za kitaaluma, itafakari na kuanza kuwawezesha wanafunzi kwa kuandaa kambi hizo, ili waweze kunolewa kakamilifu na hatimaye ufaulu wao uongezeke.

BARUA / MJADALA

# Tunahitaji maofisa ugani

***MHARIRI***

*HABARI za Dar es Salaam?*

*Nimehamia Dar es Salaam nikitokea Mvomero baada ya kufika mjini nimeamua kulima hapa nyumbani Kibaha Maili moja.*

*Hata hivyo, naomba niombe serikali itusaidie kumaliza suala la wadudu waharibifu wa mazao kwa kutupatia wataalamu.*

*Licha ya kupanda mahindi karibu heka 4.5 nimeanza kuteseka na tatizo la wadudu wanakula majani ya mahindi.*

*Sehemu kubwa ya majani yametobolewa na tatizo ni kubwa si kama nilivyokuwa nadhani.*

*Kwa bahati mbaya huku Dar es Salaam hakuna maofisa ugani wa kunishauri.*

*Ndiyo maana naomba serikali itukumbuke wakulima wa Dar es Salaam.*

*Itusaidie kwa kuwaajiri wakulima watakaotuhudumia maana tunachangamoto zinazohitaji maelezo yao.*

***Hamphrey Temu***
***Tanesco Kisarawe***
***Pwani***

# H/shauri mjikwamue kwa sheria

***Mhariri,***

*KUNA baadhi ya halmashauri nchini kutokana na matatizo mbalimbali walionayo, zimekuwa zikichukua hatua ya kutunga sheria ndogo kukabili baadhi ya matendo na mila zinazowakwamisha kitabia na kimaendeleo.*

*Nakumbuka mwaka 2006, Rais Jakaya Kikwete alizuru wilayani Tunduru, mkoani Ruvuma kukagua miradi ya maendeleo, zikiwamo barabara.*

*Huko alikutana na lililomkera hasa suala la mimba za shuleni zilizokithiri kupita kiasi. Aliuagiza uongozi wilaya kuchukua hatua na baada ya muda mfupi, zilichukuliwa hatua nyingi, ikiwamo kudhibiti sherehe za mila kwa kutunga sheria zake ndogo.*

*Baada ya miaka kadhaa mafanikio yalifikiwa, kasi ya mimba kupungua maradufu. Ushauri wangu ni kwamba, halmashauri zote zitumie sheria zake ndogo kukabili baadhi shida zao za kijamii.*

***Eshi Shaban,***
***Mbesa , Tunduru***

**WASILIANA NASI:**

**TUNAKARIBISHA BARUA NA MAONI YA MSOMAJI, UNAWEZA KUTUMA KUPITIA KWA MHARIRI S.L.P. 31042, DAR ES SALAAM AU mhariri@nipashe.co.tz**

# Bila kujali misitu taifa lisubiri kilio

**Na Christina Haule, MOROGORO**

MVUA zinazonyesha bila mpangilio, wakati mwingine kutokea ukame au jua kali na joto ni matokeo ya uharibifu wa mazingira unaotokana na shughuli mbalimbali zinazoharibu mazingira.

Shughuli hizo ni kama kukata miti, kuchoma mkaa na kulima bila kufuata utaratibu wa kisheria, miongozo na sera.

Juhudi mbalimbali za wadau wa misitu zinaendelea kufanywa ili kunusuru misitu na kuimarisha kwa lengo la kusaidia jamii katika kufanikisha mambo mengi ikiwamo kupatikana kwa ajira kwa vijana na kufikia lengo la serikali la kuwa na uchumi wa viwanda.

Ni wazi kuwa kwa kutumia mali asili misitu vijana wanaweza kuanzisha viwanda na kuajiri wenzao na hivyo kuleta manufaa kwao na taifa kwa ujumla.

Moja ya wadau wa misitu ni Shirika la Kuhifadhi Misitu Asili Tanzania (TFCG) ambalo linatekeleza mradi wa kuleta mageuzi katika sekta ya mkaa Tanzania (TTCS) katika wilaya za Morogoro, Kilosa na Mvomero.

Wahifadhi hawa wanahimiza uvunaji misitu unaofanywa kwa mujibu wa sheria na taratibu utumike ili kunusuru uharibifu wa misitu uliopo na unaosababisha upotevu wa hekta zaidi ya 469,000 kila mwaka kutokana na ufyekaji ovyo misitu unaotokana na mahitaji makubwa ya ardhi ya kilimo.

Mkurugenzi Msaidizi wa TFCG Emmanuel Lyimo, anasema, uandaaji mashamba kwa ajili ya shughuli za kilimo cha kuhamahama na uwepo wa mahitaji makubwa ya ardhi kutokana na matumizi ya teknolojia hafifu za kilimo unachangia kwa kiasi kikubwa upotevu wa misitu nchini.

Lyimo anasema, mara kadhaa serikali kupitia sera mbalimbali imekuwa ikikemea matumizi ya mkaa kama nishati nyumbani na kwamba ndiyo chanzo cha uharibifu na upotevu wa misitu.

Alisema jambo hilo si kweli kutokana na utafiti uliofanywa na TFCG mwaka 2010-2017 kupitia ufadhili wa mfuko wa Critical Ecosystem Partnership Fund.

Anasema, kuendelea kutoa elimu ya uvunaji mazao ya misitu kwa njia endelevu ambayo inapaswa kufuatwa ili kulinda misitu, ni jambo jema litakalosaidia kunusuru kupotea kwa misitu ambayo ndio njia sahihi ya kuhifadhi mvua na kuepukana na mabadiliko ya tabia nchi kama yanayotokea kwa kipindi hiki.

Lyimo anasema, ikiwa wakulima watalima kwa kutumia teknolojia sahihi wanaweza kutumia eneo dogo kuzalisha mazao mengi na kuachana na kuongeza maeneo kitendo ambacho huharibu na kupoteza misitu.

Hata hivyo, anasema serikali inapaswa kushirikiana na wadau kuendelea kutoa elimu ya mkaa endelevu na kusambazwa Tanzania nzima na kufanya kilimo hifadhi kuendelea kutumiwa na kupunguza au kuondoa uharibifu a mazingira na upotevu wa misitu.

Anasema, hatua zisipochukuliwa kwa uharibifu huo wa misitu na mazingira kwa ujumla unaofanywa mapema ni wazi kwamba vizazi vijavyo vitakosa maeneo kwa ajili ya shughuli mbalimbali.

Emmanuel Msofe ni Ofisa Misitu Mwandamizi kutoka Wizara ya Maliasili na Utalii, anauzungumzia msitu kama sehemu yenye thamani ikiwa watumiaji wake watatumia vyema elimu ya kuongeza mnyororo wa thamani katika mazao ya misitu nchini.

Msofe ambaye pia ni Mratibu wa Kitaifa Programu ya Kuendekeza Mnyororo wa Thamani kwenye Mazao ya Misitu (Forvac) anasema, matumizi ya elimu ya Forvac yanapaswa kuzingatiwa si tu kwa wakazi wa maeneo yenye programu bali kwa wakazi wote wa maeneo jirani na msitu ili kuleta manufaa kwao na taifa.



Moto kama huu ni kitisho cha misitu nchini na ndiyo mwanzo wa ardhi kuwa jangwa. **PICHA: MTANDAO**

Anasema lengo la Forvac ni kufanya jamii kuona faida ya mazao ya misitu badala ya kutumia misitu kujinufaisha ambapo wakitumia mazao ya misitu kwa kuzingatia mnyororo wa thamani wanaweza kunufaika na kuacha kuharibu mazingira kwa kuvuna msitu bila kufuata utaratibu.

Msofe anasema, upanuzi wa mashamba hasa kwenye maeneo yenye msitu wa mataji wazi (msitu wenye miti jamii ya miombo) umeendelea kuharibu misitu kufuatia wakulima kuchoma mkaa miti yote wanayovuna badala ya mingine kuikata mbao na kuandaa magome ambavyo vyote wataviuza na kuongeza kipato ambao ndiyo mnyororo wa thamani.

Anasema baadhi ya misitu ya hifadhi imeendeelea kuvamiwa na watu mbalimbali hasa wakulima na wafugaji na kwamba mmojawapo ni msitu wa Ukiredo ambao watu walikaa ndani yake kwa muda mrefu na kutaka eneo hilo kurasimishwa kuwa kijiji bila kujali madhara ya uharibifu wa mazingira yanayosababisha mabadiliko ya tabia nchi yanayoendelea kutokea.

Programu ya Forvac inatekelezwa katika halmashaui 10 nchini ambazo zimetengwa katika kongani (clusters) tatu zilizopo katika mikoa ya Tanga kwenye Halmashauri za Kilindi, Handeni na Mpwapwa ambayo imeongezewa ikitokea Mkoani Dodoma.

Kongano nyingine ni ya Lindi Halmashauri za Liwale, Nachingwea na Ruangwa na pia Ruvuma kuna Songea, Namtumbo, Mbinga na Nyasa Programu ambayo ilianza mwaka 2018 na inatarajiwa kuisha mwaka 2022.



# Mhadhiri akiri kortini kuomba rushwa ngono

INATOKA UK 2

aibu kwa umri wake na mtu wa taaluma ya mshtakiwa alipaswa kuwa mfano wa kuigwa lakini akaamua kujiingiza katika mapenzi na watoto wadogo ambao si hadhi yake.

Awali, Wakili wa Serikali Mkuu, Zakaria Ndasco, alidai kuwa Jamhuri haina kumbukumbu ya makosa ya zamani na tayari ameshalipa fidia ya Sh. milioni mbili.

Kabla ya hukumu hiyo, Wakili wa Utetezi, Claudia Msando, alidai kuwa mshtakiwa ana umri mkubwa na kwamba ameshaanza kupata maradhi ya uzee ikiwamo kutokusikia na kuona vizuri, ni mstaafu na ana familia inamtegemea.

Katika kesi ya msingi, mshtakiwa anadaiwa kuomba rushwa kwa mwanafunzi aliyekuwa anasoma katika chuo hicho.

Ilidaiwa kuwa mshtakiwa ambaye alikuwa akifundisha wanafunzi wa mwaka wa kwanza mwaka wa masomo 2015/16, aliomba rushwa hiyo kutoka kwa mwanafunzi Victoria Faustine.

Mwendesha Mashtaka wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukutu), Vera Ndeoya, alidai kuwa Januari 12, 2017 katika nyumba ya kulala wageni iitwayo Camp David iliyopo Mwenge jijini Dar es Salaam, mshtakiwa aliomba rushwa ya ngono.

Ilidaiwa kuwa mshtakiwa huyo akiwa mwajiriwa wa NIT katika kozi ya Usimamizi wa Barabara na Usafirishaji namba LTU 07101 kwa kutumia mamlaka yake alimlazimisha mwanafunzi huyo kutoa rushwa ya ngono.

Ilidaiwa kuwa aliomba rushwa hiyo ili kumfaulisha katika mtihani wake wa marudio katika kozi ya Usimamizi wa Barabara na Usafirishaji anayosomea ya Januari 5, 2017.



Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Rais mstaafu wa Awamu ya Nne, Dk. Jakaya Kikwete, akiwa na Mkuu wa Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa (MUCE), Prof. Esther Dungumaro (kushoto) na Mkuu wa Wilaya ya Kilolo, Asia Abdallah, wakati wa mahafali ya 11 ya MUCE mkoani Iringa wikiendi. **PICHA: FRIDAY SIMBAYA**

# Wapinzani wacharuka nembo kutumika uchaguzi wa mitaa

INATOKA UK 2

haujabadilika na wamesikitishwa na wasimamizi kuendelea kutumia nembo na majina ya wagombea wao waliojitoa.

"Hili halikutushangaza kwa sababu serikali ilishasema kuwa watatumia nembo ya chama na majina yatatokea kama walivyosema," alisema.

Alisema timu ya uchaguzi wa ACT- Wazalendo inafanya uchambuzi wa kina kwa maeneo yote ambayo nembo ilitumika isipokuwa mtaa mmoja wa Manispaa ya Moshi ambao mgombea aligoma kujitoa, akajitosa kwenye uchaguzi ikiwamo kufanya kampeni.

Alisema hadi sasa, hawajapokea taarifa yoyote ya ushindi kwa wote ambao majina yalijitokeza kwenye fomu hizo.

Mkurugenzi wa Itikadi, Uenezi na Mambo ya Nje wa Chadema, John Mrema, alisema: "Tunakusanya vielelezo na tutatoa ushahidi kwa halmashauri zilizokiuka agizo la chama."

**JAFO ATANGAZA MATOKEO**

Jafo atangaza ushindi wa CCM

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, jana alitangaza matokeo ya uchaguzi huo uliofanyika juzi, akieleza kuwa CCM imeshinda vijiji 12,260, sawa na asilimia 99.9.

Jafo pia alisema CCM imeshinda katika mitaa 4,263, sawa na asilimia 100 katika matokeo ya jumla, huku Chadema na CUF wakishinda katika kijiji kimoja kimoja.

Alisema katika nafasi ya mwenyeviti, CCM kimeshinda vitongoji 63,970, sawa na asilimia 99.4 na chama cha ACT - Wazalendo kikishinda kitongoji kimoja.

Akielezea mchakato wa uchaguzi huo, Jafo alisema jumla ya nafasi zilizogombaniwa ni 332,160, zote zilihusisha katika uchaguzi wa vijiji 12,262, mitaa 4,263, vitongoji 63,992, wajumbe kundi la wanawake 106,622 na wajumbe kundi la mchanganyiko 145,021.

Alisema Chadema katika nafasi ya wenyeviti wa vijiji imeshinda nafasi moja, wenyeviti wa vitongoji (19), kundi la wanawake (39), wajumbe kundi la mchanganyiko (71).

Alsiema CUF imepata nafasi moja ya kijiji, vitongoji viwili, wajumbe kundi la wanawake nafasi tatu na wajumbe kundi la mchanganyiko nafasi 14.

*Imeandikwa na Salome Kitomari (DAR), Marco Maduhu (SHINYANGA), Paul Mabeja (DODOMA) na Mary Mosha (MOSHI)

# TRA yakusanya tril. 58.3/- miaka minne ya Magufuli

INATOKA UK 2

mwaka huu, TRA imekusanya ushuru wa bidhaa Sh. bilioni 77.8 na kodi ya ongezeko la thamani (VAT) Sh. bilioni 23.5.

Alisema katika eneo la vinywaji laini matumizi ya ETS yalianza Agosti mwaka huu ambapo Septemba na Oktoba walikusanya Sh. bilioni 10 huku VAT ikiwa na Sh. bilioni 14.1.

Pia alisema serikali iliyafanyia kazi malalamiko ya wafanyabiashara ikiwamo makadirio makubwa ya viwango vya kodi ambapo yamefanyika mabadiliko ya sheria mbalimbali na kupunguza viwango vya kodi na kufuta tozo takriban 54.

"Tumepunguza viwango vya kodi vya wafanyabiashara wadogo kutoka Sh. 150,000 hadi kufikia Sh. 100,000 hawa ni kwa wale wenye mzunguko wa mauzo yanayozidi Sh. milioni nne," alisema.

Pia alisema wafanyabiashara wenye mauzo kati ya Sh. milioni 7 hadi Sh. milioni 11 viwango vya kodi vimepungua na kufikia Sh. 250,000 kutoka Sh. 318,000.

Mbibo alisema wenye mauzo kati ya Sh. milioni 11 hadi Sh. Milioni 14 viwango vimepungua hadi Sh. 450,000 kutoka Sh. 456,000.

Alisema wanaopaswa kutengeneza hesabu za mizania, viwango vimebadilika kutoka mauzo ghafi ya Sh. milioni 20 hadi kufikia Sh. milioni 100 kwa mwaka.

Alisema kutokana na mabadiliko hayo, wafanyabiashara wapya watakaosajiliwa TRA na kupewa Namba ya Utambukisho wa Mlipakodi (TIN) watapaswa kulipa kodi baada ya miezi sita.

"Tumeongeza idadi ya walipa kodi kutoka milioni 2.2 mwaka 2015/16 hadi milioni 3.0 hadi kufikia mwezi Oktoba, " alisema.

Mbibo alisema mamlaka ilitangaza msamaha maalum wa riba na adhabu kwenye malimbikizo ya madeni ya kodi kwa asilimia 100 tofauti na asilimia 50 iliyokuwapo awali.

Mbibo alisema serikali iliongeza muda hadi Desemba 31 na kuwataka wale wote walioomba msamaha na kukubaliwa walipe.

Kuhusu changamoto, alizitaja kuwa ni ukwepaji kodi wa makusudi, biashara za magendo kutokana na kuwapo kwa ukanda mrefu wa Pwani, mipaka mingi na rushwa.

Pia alisema changamoto nyingine ni utunzaji dhaifu wa kumbukumbu na baadhi ya wafanyabiashara wenye nia mbaya kutokutumia EFD.

# DUCE, shule Dar zapigwa jeki

**Na Mwandishi Wetu**

SHULE za msingi na sekondari za mazoezi (Chang'ombe, Temeke), zilizo chini ya Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu cha Dar es Salaam (DUCE), pamoja na Shule ya Sekondari Mbezi Inn wilayani Ubungo zimewezeshwa kwa kupatiwa vifaa mbalimbali.

Uwezeshaji huo umefanywa na Benki ya NMB, ambapo hafla za makabidhiano hayo zilifanyika kwa nyakati tofauti katika shule hizo, ambako Meneja wa NMB Kanda ya Dar es Salaam, Badru Idd, aliikabidhi na kupokelewa na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Ubundo, Beatrice Dominick na Mkuu wa Wilaya ya Temeke, Felix Lyaniva.

Akipokea msaada wa mbao 843 zenye thamani ya Sh. milioni 5 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa na ofisi moja ya Shule ya Sekondari Mbezi Inn – vilivyoteketea kwa moto Aprili 1, mwaka huu, Beatrice alisema msaada huo umekuja kwa wakati sahihi, kuelekea mwaka mpya wa masomo wa 2020.

Alisema, licha ya serikali kutenga kiasi cha Sh. milioni 50 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa na ofisi za Shule ya Sekondari Mbezi Inn, nguvu zaidi kutoka kwa wadau wa sekta ya elimu inahitajika, hivyo kutaka kilichofanywa na NMB kiwe mfano wa kuigwa.

"Wito wangu kwa wadau wengine kuiga utamaduni huu wa NMB, kwa sababu unakuwa ni sehemu ya kuunga mkono harakati za Serikali katika kutatua changamoto zinazokwaza ustawi wa elimu nchini. Sasa nina uhakika Januari shule zikifunguliwa, hapa patakuwa pamekamilika," alisema Beatrice.

Mkuu wa Shule hiyo, Noah Ballige, kwa niaba ya wazazi, walimu na wanafunzi wa Mezi Inn, aliishukuru benki hiyo kwa msaada huo, huku akiahidi sio tu kutunza miundombinu ya shule itakapokamilika, bali watahakikisha wanawawajibisha wanafunzi watakaohusika na uharibifu.

Katika hafla iliyofanyika DUCE, Badru alikabidhi msaada wa viti na meza 100 kwa ajili ya shule za misingi na sekondari zilizo chini ya chuo hicho, msaada ulipokelewa na DC, Lyaniva.

Lyaniva aliitaka benki hiyo kudumisha utaratibu huo, huku akiiomba kwenda mbali zaidi kwa kuchakata fursa ya kusaidia wanafunzi wa vyuo wasiojiweza kuwalipia ada za masomo yao.

Kwa upande wake, Badru alisema misaada hiyo ya juzi inaifanya NMB kufikisha zaidi ya Sh. milioni 850 za misaada mbalimbali kwa jamii kati ya Sh. bilioni 1 iliyotengwa na benki hiyo kupitia Programu ya Uwajibikaji wa Jamii (CSR) kwa mwaka 2019.

# 'Elimu magonjwa yasiyoambukiza itolewe kuanzia shule za msingi'

**Na Joseph Mwendapole**

SERIKALI imeshauriwa kutoa elimu kuhusu magonjwa yasiyoambukiza kama kisukari na shinikizo la damu kuanzia shule za msingi na sekondari kwa sababu ndiyo yanayoongoza kwa sasa kuwa na vifo vingi duniani.

Ushauri huo ulitolewa mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam na Mkuu wa Idara ya Magonjwa ya Sukari katika Hospitali ya Regency, Emmanuel Maganga, wakati wa kambi ya kupima sukari bure iliyoandaliwa na hospitali hiyo kwa kushirikiana na Jumuiya ya Baps Charities.

Alisema nguvu kazi kubwa ya taifa ambayo ni vijana kuanzia miaka 30 mpaka 45 ndiyo wanaosumbuliwa zaidi na ugonjwa huo hivyo kuna haja ya kutoa elimu kuanzia ngazi za chini kuhusu namna bora ya kuuepuka.

Alisema mtindo wa maisha hasa kwa vijana ambao wanapendelea zaidi kula vyakula vyenye mafuta mengi na kushindwa kufanya mazoezi kumesababisha rika hilo kuathirika zaidi na sukari.

"Ubaya wa sukari ni kwamba ukiipata tu ujue figo iko hatarini, shinikizo la damu nalo litakuandama na mwisho wa siku utapata pia matatizo ya macho kwa hiyo mimi nadhani tunapaswa kuwapa watu elimu ya kuepukana na maradhi haya," alisema Dk. Maganga.

"Watu waelimishwe namna ya kula vyakula vyenye msaada mwilini kama mboga, kwamba kula mboga siyo umaskini na wala kula chipsi na vyakula vyenye mafuta mengi si ufahari...Watu wa zamani hawakuwa wanakula vyakula vyenye mafuta na ndiyo sababu waliishi miaka mingi sana," alisema.

Dk. Maganga alisema vijana wengi wanashinda ofisini na wakitoka wanatumia magari hivyo kutotembea kwa muda mrefu hali ambayo imesababisha wengi kuugua ugonjwa huo.



Mafundi ujenzi wakitoa takataka zilizojaa kwenye Mto Ng'ombe, katika daraja la Tandale kwa Mtogole, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# TIC, Uholanzi wakubaliana

**Na Mwandishi Wetu**

KITUO cha Uwekezaji Tanzania (TIC), kimetiliana saini makubaliano ya ushirikiano wa kujenga mifumo ya biashara na Baraza la Biashara la Uholanzi-Afrika (NABC).

Makubaliano hayo yamesainiwa na Mkurugenzi Mtendaji wa TIC, Geoffrey Mwambe na Mkurugenzi Mkuu wa NABC, Peter Ruiter, yanayolenga kujenga mfumo wa pamoja wa kufanikisha biashara na uwekezaji zaidi baina ya Tanzania na Uholanzi.

Kwa mujibu wa taarifa kwa vyombo vya habari iliyotolewa na TIC, makubaliano hayo ni matokeo ya mkutano uliofanyika kati ya TIC na NABC nchini Uholanzi, Februari, mwaka huu.

"NABC ina kampuni wanachama zaidi ya 300 ambazo zimewekeza katika sekta mbalimbali nchini Uholanzi. Sekta hizo ni pamoja na kilimo na kuongeza thamani, viwanda (nguo, maziwa), afya nishati, bandari na ujenzi, mifugo," ilisema taarifa hiyo.

Akizungumza baada ya kutia saini Mwambe alisema makubaliano hayo yana tija kwa kuwa sasa Tanzania itatangazwa nje ya nchi kupitia mitandao ya NABC na mingine nchini Uholanzi.

Kwa mujibu wa Mwambe, itasaidia kuongeza imani kwa wafanyabiashara na wawekezaji wanachama wa NABC na Ulaya kuwa Tanzania ni nchi nzuri ya kuwekeza pamoja na kushawishika kuja kuwekeza kwenye sekta mbalimbali.

Alisema makubaliano hayo pia yatawezesha kufanyika makongamano ya biashara na uwekezaji kati ya Tanzania na Uholanzi kwa lengo la kufanikisha uwekezaji wa ubia, ajira, upatikanaji wa mitaji, teknolojia, utaalam na masoko.

Mkurugenzi huyo alisema Serikali inasimamia sera na Sheria za Uwekezaji ili kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji hatua ambayo inazidi kuimarisha na kuiweka nchini kuwa sehemu nzuri ya uwekezaji.

"Haya mnayoyaona yanatokana na usimamizi madhubuti wa Sera na Sheria za uwekezaji ambazo Tanzania imejiwekea, tunafanya hivi ili kuwa na uwekezaji wenye tija," alisema Mwambe.

Naye Ruiter alisema kupitia makubaliano waliyoingia na TIC, Tanzania itakuwa na nafasi nzuri ya kujitangaza Uholanzi na Ulaya kwa ujumla kwa sababu NABC itahamasisha na kushawishi wanachama wake kuchangamkia fursa zilizoko Tanzania kwa maendeleo ya nchi zote.

Alisema Uholanzi ni nchi ya kibiashara na uwekezaji hatua ambayo imewezesha kujenga uchumi wake.

"Huwezi kufanya uwekezaji kwenye nchi ambayo haijatulia, mazingira yake hayapo sawa na uchumi wake haulindwi, Tanzania ni nchi nzuri sana na tunaweza kuwekeza hapa," alisema Ruiter.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi Mkuu wa Baraza hilo, uwekezaji Tanzania una manufaa makubwa kutokana na kuwa na uchumi usioyumba, mapambano dhidi ya rushwa na usimamizi mzuri wa rasilimali za nchi.

# Watumishi wa serikali wanusurika kifo

**Na Mwandishi Wetu, PEMBA**

WAFANYAKAZI 11 wa wizara mbali mbali za serikali wamenusurika kufa, baada ya gari walilokuwa wakisafiria kupinduka wakati dereva alipokuwa akimkwepa mtu mmoja aliyekuwa akiendesha baiskeli.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kaskazini Pemba, Mohamed Shehan Mohamed, alieleza kuwa ajali hiyo ilitokea Penjewani Wilaya ya Wete majira ya jioni.

Kamanda Shehan alisema gari hilo aina ya Toyota Double Cabin lilikuwa likiendeshwa na Rashid Hassan Hamad ambalo likitokea Chakechake kwenda Wete.

"Gari hilo lilikuwa likitokea Chakechake na lilipofika maeneo ya Penjewani dereva alimkwepa mpanda baiskeli, ambae hakujuilikana na dereva kushindwa kurudi barabarani, hivyo gari hilo kupinduka," alisema.

Kamanda Sheikhan, aliwataka walionusurika kufa ni Omar Mjaka mkazi wa Mkwajuni Wete, Khamis Rashid Suleiman wa Bubujiko Wete, Omar Said Omar wa Bopwe Wete na Amour Juma Mohammed wa Limbani Wete.

Wamo pia Saleh Khamis Salum wa Kifumbikai, Farid Juma wa Bopwe na Faki Bakar Faki wa Kizimbani Wete ambao walifikishwa katika Hospitali ya Wete kwa matibabu.

Kadhalika, Omar Khamis Kaimu wa Gando ambaye ni askari wa JKU Wawi na Mohammed Massoud Abdalla wa Kizimbani wao walifikishwa Hospitali ya Vitongoji, huku Ali Omar Ali akifikishwa Hospitali ya Abdalla Mzee.

Hata hivyo, Kamanda Sheikhan alieleza hali za majeruhi hao zinaendelea vizuri wengine wakiruhusiwa kurudi nyumbani.

Kuanzia Januari hadi Oktoba mwaka huu, jumla ta ajali 19 zimetokea katika Mkoa wa Kaskazini Pemba, ambapo watu saba wamefariki na wengine 44 kujeruhiwa.




Mkuu wa Bidhaa wa Tigopesa, James Sumari, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, katika uzinduzi wa kampeni mpya ya 'Kishindo cha Funga Mwaka', ambapo wateja wa Tigopesa watajishindia zawadi za thamani ya zaidi ya Sh. milioni 500 katika kipindi cha kuelekea sikukuu za mwisho wa mwaka. Kushoto ni Meneja Wateja Maalum wa Tigopesa, Mary Rutta.
**PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Udumavu wa watoto wapungua kijijini

**Na Elizabeth Zaya, aliyekuwa MAKETE**

MPANGO wa kunusuru kaya maskini unaosimamiwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (Tasaf), umesaidia kupunguza udumavu kwa watoto wa kijiji cha Lupila kilichopo katika Kata ya Ukange wilayani Makete.

Akizungumza mbele ya maofisa wa Tasaf waliotembelea mradi wa kilimo cha viazi wa walengwa wa mfuko huo, Ofisa Maendeleo ya Jamii wa kijiji hicho, Veronica Kalimba, alisema kabla ya kupelekwa mpango huo kijijini hapo hali ya afya kwa watoto wa walengwa haikuwa ya kuridhisha.

Alisema tatizo la udumavu kwa watoto kijijini hapo lilikuwa linasababishwa na ukosefu wa chakula cha uhakika na bora.

"Mimi ninafanya kazi kwa karibu na wananchi hapa kijijini, na kwa maana hiyo nimekuwa nikizungumza na kutembelea familia mara kwa mara... tatizo la udumavu kwa watoto lilikuwa kubwa miaka zaidi ya sita iliyopita, lakini kwa sasa halipo kabisa," alisema Kalimba.

Aliongeza: "Kabla ya kuingizwa kwenye mpango wa Tasaf, chakula pekee ambacho angalau walikuwa wanakipata ni makande ambayo nayo ilikuwa ni kwa shida sana, lakini sasa hakuna changamoto kama hiyo. Wanalima viazi, mboga za majani za aina tofauti na wanafuga, kwa hiyo wanakula chakula wanachokitaka na siyo cha aina moja, tunaishukuru serikali kwa mpango wake huo."

Mlengwa wa Tasaf katika kijiji hicho, Evaristo Ndelwa, alisema baada ya kuingizwa katika mpango huo wa kunusuru kaya maskini, walipewa elimu ya namna ya kutumia pesa wanayopewa ikiwamo kuhakikisha familia inapata chakula bora.

Alisema jambo jingine ambalo wamenufaika kutoka Tasaf ni kupewa elimu ya namna ya kujiwekea akiba na kuazisha miradi mbalimbali ya kujiongezea kipato.

## Wadau kujadili kilimohai

**Na Faustine Feliciane**

WADAU wa kilimo nchini kutoka sekta binafsi na serikalini watakutana kwa siku mbili jijini Dodoma kujadiliana maendeleo ya kilimohai nchini.

Mkutano huo ulioandaliwa kwa pamoja kati ya Taasisi ya Kuendeleza Kilimohai nchini (TOAM), Wizara ya Kilimo na mashirika ya kimataifa utafunguliwa na Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga.

Mkutano huo utakaoanza leo utawakutanisha wadau wote wa kilimo wakiwamo pia watunga sera taasisi za serikali na zisizo za serikali na utajadili kwa kina ulinzi na usalama wa chakula pamoja na mabadiliko ya tabianchi.

Mshauri wa mawasiliano wa TOAM wanaoratibu mkutano huo, Costantine Akitanda, alisema ni muhimu kwa maendeleo ya kilimohai Tanzania.

Alisema kwa ushirikiano wa Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO) na Ubalozi wa Ufaransa nchini, wamechukua jukumu la kuhakikisha kilimohai kinaendelezwa kwa mustakabali wa baadaye.

## Umuhimu wa sheria, sera misitu watajwa

**Na Christina Haule, aliyekuwa TANGA**

SHERIA na sera za misitu zikiwekwa vizuri, zitasaidia kuondoa uharibifu wa misitu ulipo sasa nchini.

Kauli hiyo ilisemwa na Mratibu wa Programu ya Kuendeleza Mnyororo wa Thamani wa Mazao ya Misitu (FORVAC) Kitaifa, Emmanuel Msofe, wakati akizungumza kwenye mafunzo ya waandishi wa habari kutoka mikoa mbalimbali ya Tanzania yaliyofanyika jijini Tanga.

Msofe ambaye ni Ofisa Misitu Mwandamizi kutoka Wizara ya Maliasili na Utalii, alisema kwa sasa sheria na sera za misitu zilizopo ni za muda mrefu, na kwamba zinaendelea kufanyiwa marekebisho ili ziendane na hali halisi iliyopo.

Alitolea mfano sera ya misitu ya mwaka 1953 ambayo ni ya kwanza na ilifanyiwa marekebisho mwaka 1998, lakini haijakidhi mahitaji ya misitu kwa jamii, hivyo inaendelea kurekebishwa na kuletwa tena kwa ajili ya maendeleo kwa wananchi.

Naye Mratibu wa FORVAC Kongani ya jijini ya Tanga, Petro Masorwa, alisema lengo kuu la FORVAC ni kuongeza faida

## JPM apongezwa kwa elimu bure

**Na Cynthia Mwilolezi, MANYARA**

TAASISI ya Agape Mission Tanzania, imemshukuru Rais John Magufuli, kwa kutoa elimu bure kidato cha kwanza hadi cha nne, kwani wanafunzi wengi na wazazi wenye kipato duni wametumia fursa hiyo kupiga hatua kielimu.

Mkurugenzi wa Agape Mission Tanzania, Mchungaji Canon Kedmon Mlemeta, aliyasema hayo kwenye mahafali ya tano ya Shule ya Sekondari Mgutwa wilayani Simanjiro, mkoani Manyara.

Mchungaji Canon Mlemeta alisema dhana ya elimu bure ya Rais Magufuli ina manufaa makubwa kwa jamii kwani Taifa litakuwa na wasomi wazuri na nchi itainuka kupitia taaluma mbalimbali.

"Wengine watakuwa maprofesa, madaktari, walimu, wahandisi, wataalamu wa mifugo, kilimo, ujenzi, uashi na taaluma mbalimbali, hiyo yote ni kupitia dhana ya elimu bure ya Rais Magufuli," alisema.

Mgeni rasmi wa mahafali hayo, Ofisa Tarafa ya Moipo, Joseph Mtataiko aliipongeza Shule ya Mgutwa kwa kutunza mazingira kutokana na kugawa miche kwenye taasisi mbalimbali.

"Mmegawa miche kwenye shule na pia kule kwenye uwanja wa wazi wa soko na mnada wa Songambele Kata ya Mirerani miti mingi mliipanda na sasa imekuwa mikubwa," alisema Mtataiko.

Mkurugenzi wa Shule ya Sekondari Mgutwa, Shadrack Mlemeta, alisema shule hiyo iliyonzishwa mwaka 2012, imepiga hatua kwani imeanzisha kidato cha tano ambao wataanza masomo mwakani.

Alisema wametoa upendeleo kwa wanafunzi 23 waliohitimu kidato cha nne kusoma kozi ya kompyuta itakayoanza Januari mwakani.

Mmoja kati ya wahitimu, Mary Mndolwa, akisoma risala alisema walianza kidato cha kwanza mwaka 2016 wakiwa wanafunzi 48 ila wamehitimu wanafunzi 23 pekee.

Alisema wanafunzi wote wanawashukuru walimu na uongozi wa shule hiyo kwa kuwasimamia kitaaluma na nidhamu, kwa kuwalea kimwili na kiroho.

Katika mahafali hayo iliendeshwa harambee ya ghafla ya umaliziaji wa jengo la maabara ya wanafunzi wa shule hiyo na kupatikana Sh. 600,000.

**"Wengine watakuwa maprofesa, madaktari, walimu, wahandisi, wataalamu wa mifugo, kilimo, ujenzi, uashi na taaluma mbalimbali, hiyo yote ni kupitia dhana ya elimu bure ya Rais Magufuli," alisema.**

# Wafanyabiashara madini watii agizo la serikali

**Na Allan Isack, ARUSHA**

WAFANYABIASHA wa madini zaidi ya 1,000, wakiwamo wakubwa, wakati na wadogo katika soko la madini jijini Arusha, wameitikia wito wa serikali wa kuhamia katika soko hilo.

Licha ya kuitikia wito huo, wameiomba serikali kuboresha miundombinu, ikiwamo huduma ya vyoo ambayo hairidhishi na inaweza kusababisha magonjwa ya mlipuko.

Mwenyekiti Taifa wa Chama cha Wafanyabiashara wa Madini (Tamida), Sammy Mollel, alisema mwitikio wa wafanyabiashara hao umesababisha eneo la madini kufurika na kusababisha foleni ya magari.

Alisema hatua hiyo, imetokana na ufinyu wa eneo na kuwapo kwa tatizo la huduma ya vyoo, kitendo ambacho wanahofu kinaweza kusababisha maambukizi ya magonjwa.

Mollel alisema tangu kuzinduliwa kwa soko hilo Juni 15 mwaka huu, wafanyabiashara wapatao 40 wamepata ofisi za kudumu na wengine 57 hawajapata.

Alisema baada ya kuanzishwa kwa soko hilo, limewawezesha kupata faida kubwa na kodi ya ongezeko la thamani (VAT) kwa biashara ya madini kwenye masoko yote yaliyoanzishwa na serikali nchini.

"Mwitikio kwa wafanyabiashara wa madini katika soko la madini ni kubwa na kunafaida nyingi sana kwa wafanyabiashara wa madini katika soko la pamoja ikiwamo huduma ya kibenki ambayo itakuwapo, ulinzi wa polisi na kukutana na wafanyabiashara wa kimataifa watakaofika kununua madini hapa," alisema Mollel.

Katika hatua nyingine, mwenyekiti huyo ameiomba serikali kuwaondolea tozo ya asilimia moja inayotozwa na serikali kama tozo za ukaguzi wa mizigo ya madini yanayosafirishwa kwenda nje.

Hata hivyo, alisema tozo hizo zinawaumiza wafanyabiashara hao, kwani zimekuwa zikiwapatia usumbufu na kuchelewesha kupata kibali cha kusafirisha madini.

Alisema hadi kupata kibali cha kusafirisha madini inayochukua zaidi ya siku mbili hadi tatu.

"Tuna tatizo la ushuru unaoitwa Tasac, hii ni kodi mpya iliyokuja kivingine na kodi hii inaleta urasimu katika biashara ya madini kwa lengo la kuwaumiza wafanyabiashara hao," alisema.

Ameiomba serikali kuondoa urasimu huo, wenye lengo la kuwabughudhi wafanyabiashara hao.



Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Arusha, Dk. Maulid Madeni (kulia), akiongozana na aliyekuwa Mstahiki Meya wa jiji hilo, Calist Lazaro, baada ya kuwasili viwanja vya halmashauri hiyo jana, kwa ajili ya kuaga watumishi na kukabidhi ofisi. **PICHA: CYNTHIA MWILOLEZI**

# 'Utandawazi dawa ya umaskini Afrika'

**Na Daniel Sabuni, ARUSHA**

WASOMI wa Afrika wenye ujuzi wa kufanya biashara katika dunia ya utandawazi wametakiwa kutumia teknolojia hiyo, kupunguza umaskini kwa wananchi wa Afrika.

Akizungumza katika mahafali ya 18 ya Chuo Kikuu cha Uongozi, Utawala na Biashara cha Kusini Mashariki mwa Afrika (ESAMI), Mkurugenzi wa Kitengo cha Chuo hicho, Peter Kiuluku, dunia inapoelekea Waafrika wataweza kufanya biashara kisasa na kwa viwango vya kimataifa.

Alisema chuo hicho kimeandaa mtaala ambao unatoa mafunzo halisi yatakayomkomboa Mwafrika kwa ajili ya kupunguza wimbi la umaskini.

"Tunahitaji wasomi waliobobea kwenye biashara na wenye mbinu zinazoendana na mwendo wa teknolojia mpya za kibiashara ili kumudu soko la ajira na mahitaji yanayotakiwa ili kupunguza matatizo yanayokabili wananchi wa bara letu," alisema Kiuluku.

Alisema chuo hicho mpango wake ni kuwajengea uwezo wasomi wa Afrika ili waweze kusaidia nchi zao kupata mafanikio kwa kutumia utandawazi.

Kiuluku alisema, katika mahafali ya chuo hicho, jumla ya wanafunzi 100, kutoka nchi 21 za Afrika walihitimu shahada ya uzamivu na uzamili katika fani za sera za biashara, sheria na biashara.

"Kila mtu anajua sasa chuo chetu sio tu cha Kusini Mashariki mwa Afrika, bali Afrika nzima tayari tumesaini mkataba mpya wa kuunganisha Afrika nzima kuwa kitu kimoja.


Alisema wahitimu hao watasaidia nchi zao kufanya makubaliano ya kibiashara kati ya nchi moja na nyingine kwa kubadilishana bidhaa.

Alisema endapo nchi hizo zitafanya biashara kwa pamoja, watakuza uchumi wa nchi zao na kwa mwananchi mmoja mmoja.

Alieleza kwamba nchi za Afrika zilizokua kiuchumi na ambazo hazijakua pia zitapata fursa ya kunufaika.

Alimpongeza Hayati Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, ambaye ndiye aliyebuni wazo la kuanzishwa kwa chuo hicho mwaka 1974.

"Chuo hiki kilianzishwa kwa malengo ya Afrika Mashariki, baadaye mwaka 1982, kilifika Kusini Mashariki na 1997 kilifika nchi zote za Afrika," alisema.





# CCM yashinda vijiji, mitaa Vunjo, Mwanga

**Na Mwandishi Wetu, MOSHI**

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) kimeibuka kidedea katika uchaguzi wa serikali za mitaa uliofanyika juzi katika vijiji vitano vilivyofanya uchaguzi katika mkoa wa Kilimanjaro pamoja na vitongoji 10 katika majimbo ya Mwanga na Vunjo.

Kwa mujibu wa Ofisa Usimamizi wa Uchaguzi katika Jimbo la Mwanga, Erick Kaaya.

Katika jimbo hilo lilikuwa linafanya uchaguzi katika vijiji vinne ambavyo Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), na Chama Cha Mapinduzi (CCM), vilisimamisha wagombea.

Vijiji hivyo ni Mbambua kilichoko kata ya Lembeni Gongoni Kata ya Toloha, Vuchama Mdambwe Kata ya Shighatini na Sofe Kata ya Kilomeni na Kilaracha Jimbo la Vunjo.

Kaaya alisema katika kijiji cha Mbambua, mgombea uenyekiti wa kijiji kupitia CCM, William Mvungi aliibuka kidedea kwa kupata kura 300, huku mgombea wa Chadema, Leon Mvungi akipata kura tisa.

Kwa upande wa kijiji cha Gongoni, alisema mgombea wa CCM, Yassin Msangi, alipata kura 95 huku akimbwaga mpinzani wake wa Chadema, Mshangama Juma aliyepata kura nne na kijiji cha Vuchama Ndambwe, Ismail Mmbughu wa CCM, alipata kura 308, huku mgombea wa Chadema, Akilimali Leghela, akipata kura 39.

Katika kijiji cha Sofe, mgombea wa CCM, Daudi Msofe, aliibuka kidedea kwa kupata kura 481 huku Mwaluma Joseph wa Chadema akipata kura 25.

Katika jimbo hilo pia kulifanyika uchaguzi wa wenyeviti wa vitongoji 10 na CCM ilibuka na ushindi kwa kunyakua viti vyote huku Chadema ikiambulia patupu.

Katika Jimbo la Vunjo, kulikuwa na uchaguzi katika kijiji cha Kilaracha ambako ni nyumbani kwa Mwenyekiti wa TLP Taifa, Agustino Liatonga Mrema.

Kwa mujibu wa msimamizi wa uchaguzi katika jimbo hilo, Juma Tukosa, waliojitokeza kujiandikisha katika daftari la wapigakura ni 912, huku waliojitokeza kupiga kura wakiwa 619.

Alisema uenyekiti wa kijiji kupitia CCM, Thomas Mrema aliibuka kidedea kwa kupata kura 518, huku mgombea wa TLP, Andrea Lekule, akipata kura 101.

**Kaaya alisema katika kijiji cha Mbambua, mgombea uenyekiti wa kijiji kupitia CCM, William Mvungi aliibuka kidedea kwa kupata kura 300, huku mgombea wa Chadema, Leon Mvungi akipata kura tisa.**

# Mapambano ujangili sasa kidijitali

**Na Mary Mosha, MOSHI**

TATIZO la ujangili katika hifadhi mbalimbali nchini limepata ufumbuzi baada ya Shirika la Misaada ya Maendeleo ya Kimataifa la Marekani (USAID) kutoa kompyuta 30 kwa Chuo cha Usimamazi wa Wanyamapori Mweka zenye programu maalumu kwa ajili ya kutazama maeneo walipo wanyama.

Kompyuta hizo mbali na kufungwa mtandao maalumu wa kijiografia utakaowasaidia wanafunzi kupata mafunzo ya kisasa, zitawasaidia katika kukabiliana na ujangili ndani na nje ya nchi.

Akipokea kompyuta hizo jana, Waziri wa Maliasili na Utali, Dk. Hamis Kigwangala, alisema ujio wa vifaa hivyo utasaidia kuleta mabadiliko ya kisayansi katika kukabiliana na ujangili.

"Wanafunzi watakaohitimu katika chuo hiki watakuwa tayari kukabiliana na changamoto za ujangili zilizokithiri nchini kutokana na masomo wanayopewa ni ya kisasa na yatakayoleta mabadiliko katika sekta ya maliasili na utalii.

"Tunatambua umuhimu wa serikali ya Marekani kwani wameanza kutusaidia kwanzia miaka 60 iliyopita katika chuo hiki kwa kujenga mabweni ambayo hadi leo yanatumika. Tunaomba muangalie sera yenu kama inaruhusu kutusaidia katika ujenzi wa miundombinu mbalimbali hapa chuoni ikiwamo ukumbi," alisema.

Mkuu wa Chuo hicho, Prof. Jafari Kidegesho, alisema kompyuta hizo zitasaidia kuleta mabadiliko katika sekta ya utalii ikiwa ni pamoja na kukidhi mahitaji ya ulimwengu wa sayansi na teknolojia katika kukabiliana na matukio ya kihalifu na kuwalinda wanyama.

"Mwanzoni tulikuwa tunakabiliwa na uhaba wa kompyuta na mtandao kutokana na jiografia ya hapa pia idadi ndogo ya kompyuta iliyowafanya wanafunzi washindwe kupata mawasiliano ya kisasa kulingana na vitu wanavyovisoma. Lakini kwa ujio wa kompyuta hizi kutawasaidia wanafunzi kujisomea kupitia mtandao na kujiongezea ujuzi," alisema Prof. Kidegesho.

Mkurugenzi wa Usaid, David Thomson, alisema wataendelea kushirikiana na serikali ya Tanzania katika kusaidia maendeleo na kuzalisha vijana bora zaidi watakaouzika katika soko la dunia.

Joseph Mramba, Mkuu wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (Tahama) Mweka, alisema kompyuta hizo zitasaidia wanafunzi kujisomea kwa urahisi kutokana na mifumo iliyowekwa ya kumkutanisha mwalimu na mwanafunzi (E- learning).

"Mfumo huu wa mawasiliano na kusoma kwa njia ya Tehama, utatusaidia kupata ujuzi zaidi na kufahamu wenzetu duniani wanafanya nini na pia kupunguza gharama za kutafuta vitabu kwa ajili ya kujisomea," alisema Jacqueline Julius, mwanafunzi wa chuo hicho.



Spika wa Bunge, Job Ndugai (kulia), akipata maelezo kutoka kwa mwanafunzi wa mwaka wa pili Shahada ya Utawala na Wanyamapori, Boaz Loya, kuhusu tabia za ndege mbalimbali alipokuwa akikagua maonyesho yaliyoandaliwa na chuo hicho, mkoani Kilimanjaro jana. Wa pili kulia ni Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Khamis Kigwangala. **PICHA: BUNGE**

# Waziri aagiza mashine zilizouzwa kurejeshwa

**Na Mary Mosha, SAME**

NAIBU Waziri wa Kilimo, Omari Mgumba, ameagiza kurejeshwa kwa vifaa vyote vya mradi wa umwagiliaji wa Ndungu wilayani Same ambavyo vilipigwa mnada Juni Mosi, mwaka huu.

Mgumba alitoa maagizo hayo jana alipotembelea wakulima hao na kukutana na changamoto ambayo imeibua mgogoro kwa wakazi wa eneo hilo kutokana na halmashauri kupiga mnada mashine za wakulima hao.

Alisema ni marufuku vifaa vilivyoko kwenye eneo hilo la umwagiliaji kuchukuliwa na vyote vilivyopigwa mnada virejeshwe hadi serikali itakapojiridhisha na mnada huo.

Awali, wakulima Yohana Karani na Cyphod Gomera, wakizungumza katika mkutano wa hadhara, waliomba serikali kupitia Wizara ya Kilimo kutatua changamoto zinazowakabili kwa kuwa zimedumaza uzalishaji katika eneo hilo.

Naye Mwenyekiti wa Mradi huo, Juma Kapongo alimwambia Naibu Waziri kuwa vifaa hivyo viliuzwa pasipo wakulima kushirikishwa na pia walizuiwa kununua kitu chochote katika mnada huo.

Kapongo alisema wamerudhika na uamuzi alioutoa Naibu Waziri kwa kuwa vifaa hivyo havikuwa chakavu kama ambavyo Wakala wa Ufundi na Umeme (Temesa) waliishauri Halmashauri ya Wilaya ya Same, hivyo kuamua kuviuza.

Mkuu wa Wilaya ya Same, Rosemary Senyamule, amekiri kupokea maelekezo ya Naibu Waziri na kuahidi kufanyia kazi na kutoa mrejesho kamili.

Nipashe
# TESA
Jumanne Novemba 26, 2019
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI



Ukurasa 18

## Ukarimu unasaidia kuishi muda mrefu

Ukurasa 15



## Kwa jitihada hizi wasichana mshindwe wenyewe kusoma



Ukurasa 19

HAKI, UWAJIBIKAJI & VITA YA RUSHWA

## Ubia wake na ushirikishaji



# Ofisa Elimu Ilala afunguka mzizi wao kunga'ra darasa saba kitaifa

Ukurasa 16

## ELIMU KUTOKA POLISI

# IFAHAMU AFRIPOL

AFRIPOL linaweza kuwa neno geni masikio mwa baadhi ya Watanzania, lakini naomba unitegee sikio ili nitumie fursa hii kukujuza AFRIPOL ni nini na umuhimu wake katika Jeshi la Polisi na Tanzania kwa ujumla.

Kimsingi, AFRIPOL ni Shirikisho la Majeshi ya Polisi ya Bara la Afrika na ni taasisi ya kitaalamu iliyoanzishwa na Umoja wa Afrika (AU) kwa ajili ya ushirikiano wa nchi wanachama wa Umoja wa Afrika chini ya Idara ya Ulinzi na Usalama kupitia itifaki ya Baraza la Amani na Usalama ya Umoja wa Afrika katika kupambana na wahalifu na uhalifu wa kupanga na kuvuka mipaka.

AFRIPOL ilianzishwa na Wakuu wa Nchi na Serikali kwenye Mkutano wa 28 wa Umoja wa Afrika uliofanyika huko Addis Ababa nchini Ethiopia mnamo mwaka 2017. Makao Makuu ya AFRIPOL kwa sasa yapo katika jiji la Algiers nchini Algeria likiwa na wanachama 54 ambazo ni nchi zote zinazounda AU.

Aidha, Tanzania ilijiunga na Shirikisho la Majeshi ya Polisi katika Bara la Afrika mwaka 2017 na ofisi yake ipo katika makao makuu ya upelelezi wa makosa ya jinai na kusimamiwa na Mratibu Mkuu wa shirikisho hilo Inspekta Damas Nyungula.

Akizungumza na Nipashe Nyungula alisema kuwa lengo kuu la AFRIPOL ni kuimarisha ushirikiano wa majeshi ya polisi ndani na nje ya Afrika katika kuzuia na kupambana na uhalifu wa kupanga na kuvuka mipaka ikiwamo ugaidi, uhalifu wa kimtandao na kushughulikia changamoto za kiusalama zinazokabili bara la Afrika.

"Sambamba na kupambana na uhalifu unaovuka mipaka, AFRIPOL pia inafanya kazi ya kuunganisha majeshi ya polisi Afrika kupitia mfumo maalum wa mawasiliano ujulikanao kama AFSECOM, jukumu jingine ni kuratibu mafunzo kwa wataalam wa Kiafrika katika vyuo vya nchi wanachama na kufanya upelelezi na operesheni za pamoja ikiwa ni pamoja kubadilishana na kupeana taarifa kiintelejensia za uhalifu na wahalifu." Alisema Mratibu Mkuu wa AFRIPOL.

Jeshi la polisi nchini na Tanzania inanufaika kuwa mwanachama wa AFRIPOL kwa kuunganisha nguvu za pamoja na nchi nyingine za Afrika katika kupambana na makosa ya kupanga na kuvuka mipaka ikiwamo ugaidi na uhalifu wa kimtandao hasa ukizingatia ukubwa na uwazi wa mipaka ya Tanzania na Afrika kwa ujumla.

Vilevile wananchi wananufaika na AFRIPOL kwa kupata huduma za kuchunguza magari yaliyoibwa kabla ya kununua au kuingiza nchini ikiwa ni pamoja na kupata usaidizi wa karibu na rahisi wanapotendewa uhalifu wa kimtandao ambao unashamiri kwa kasi Afrika.

Uongozi wa AFRIPOL unaundwa na kamati tendaji chini ya uenyekiti wa nchi ya Algeria ikisaidiwa na Makamu Wenyeviti ambapo Makamu wa Kwanza ni Uganda, wa Pili ni Nigeria, wa tatu ni Afrika ya Kati pamoja na Kamishna wa Amani na Usalama wa Umoja wa Afrika.

Pia Kamati tendaji inaundwa na mashirikisho mengine ya Majeshi ya Polisi Barani Afrika ambayo ni Shirikisho la Wakuu wa Polisi Afrika ya Kati(CAPCCO) ambalo mwenyekiti wake ni nchi ya Niger, Shirikisho la Wakuu wa Polisi Mashariki mwa Afrika(EAPCCO) ambayo Tanzania ni Mwenyekiti, Shirikisho la Wakuu wa Polisi Kusini mwa Afrika (SARPCCO) chini ya Zimbabwe ambaye ndiye mwenyekiti.

Shirikisho la Wakuu wa Polisi Magharibi mwa Afrika (WAPCCO) chini ya Nigeria pamoja na Ushirikiano wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama Kaskazini mwa Afrika(NARC) ambayo mwenyekiti wake ni Libya.

Aidha, Sekretarieti ya AFRIPOL inaongozwa na Mkurugenzi Mtendaji wa AFRIPOL ambapo inashirikiana na mashirikisho ya Polisi ya Kimataifa ya INTERPOL, EUROPOL, AMERIPOL, ASEANAPOL na FRONTEX katika kukabiliana na uhalifu wa kimataifa na kuifanya dunia kuwa mahali salama pa kuishi.

***IMETOLEWA NA***
***OFISI YA UHUSIANO***
***POLISI MAKAO MAKUU***
***DAR ES SALAAM***
***habari.phq@tpf.go.tz au tamimu.adam@tpf.go.tz***



Mkuu wa Jeshi la Polisi, IGP Simon Sirro. **PICHA: MTANDAO**



## TUJIFUNZE KISWAHILI

**BARNABAS MARO**
marobarnabas@yahoo.com

# Chombo hakiendi ikiwa...

WAHENGA wetu walituachia utajiri wa methali zenye maana na mafunzo. Kwa mfano, "Chombo hakiendi ikiwa kila mtu anajipigia kasia."

'Kasia' ni ubao wa kuendeshea chombo cha bahari kama vile mashua. Ni vigumu chombo cha majini kwenda, kama kila mtu anajipigia upondo (ujiti/mti mrefu au ufito) unaotumika kuendeshea na kuelekeza chombo majini kama vile mtumbwi.

Aidha ni ufito mrefu unaotumika katika shindano la kurukia juu; kuruka kwa upondo; wenzo.

"Bora kujenga madaraja kuliko kujenga kuta." Maana yake ni afadhali kujenga madaraja ya kuwaunganishia watu kuliko kuta za kuwatenga.

Methali hii hutumiwa kuwaonya watu wasiwe na tabia ya kusababisha utengano au kutoelewana baina ya wenzao. Ni heri kuwaunganisha watu kuliko kuwatenganisha.

Kwa mujibu wa Kamusi la Kiswahili Fasaha la Baraza la Kiswahili Zanzibar (BAKIZA), Ni kawaida Mswahili anapozungumza na wenzake kuipamba lugha yake kwa kutumia tamathali mbali mbali za usemi kama vile tashbihi, tashihisi, istiara, jazanda, methali, misemo au nahau ambazo humjengea uwezo wa kuwa fasaha wa matumizi ya lugha katika mawasiliano yake.

'Tashbihi' ni usemi unaofananisha kitu kimoja na kingine kwa kutumia maneno kama vile kama, mithili au sawa.

'Istiara' ni matumizi ya neno kwa maana ile isiyokuwa ya msingi; tamathali ya semi inayofananisha viumbe viwili kwa kutumia sifa wanayoweza kuwa nayo.

'Jazanda' ni taswira (picha ya jambo inayomjia mtu akilini mwake anaposoma au anaposikiliza maelezo; umbo linalofanana na kiumbe kingine kilichochongwa, lililochongwa au lililofinyangwa.)

'Methali' au 'mithali' ni maneno ya kiufundi yaliyorithiwa tangu zama za dahari zilizopita katika jamii, na yanasadikiwa kuwa na ukweli, na hutumika kutolea mfano au kufumbia.

Maneno haya yanabeba ujumbe mpana zaidi kimaana kuliko maneno yenyewe yalivyo. Usemi unaowasilisha dhana mbili wenye dhima ya kufunza maadili.

'Misemo' ni kundi la maneno ambalo watu katika jamii huyatumia kwa namna mahsusi ili kupata mafunzo mema. 'Nahau' ni maneno yanayotumiwa na jamii, ambayo maana zake hazitokani na maana ya msingi ya maneno hayo.

Sasa tuone maneno yatumiwayo na waandishi wa magazeti, na watangazaji wa redio na runinga: "Mwisho wa siku." Neno 'mwisho' ni hali ya kumalizika; ukomo wa jambo; kikomo, hitimisho.

'Siku' ni muda wa saa 24 kuanzia saa moja asubuhi mpaka saa sita usiku. Baada ya muda huo ni siku ingine. Kwa mfano kusema: "Mwaka jana nilijitahidi sana kulima lakini 'mwisho wa siku' sikufanikiwa," si sahihi.

Tatizo lingine ni matumizi sahihi ya neno 'kwa'. Magazeti na hata wazungumzaji hutumia neno hilo tofauti na maudhui* yake.

*Maudhui ni neno lenye maana mbili tofauti. Kwanza ni wazo kuu linaloelezwa katika kazi ya fasihi. Kwa muktadha huu, maana ya pili ni wazo linaloelezwa katika maandishi au katika kusema.

'Kwa' ni neno lenye maana nyingi, tofauti na jinsi litumiwavyo siku hizi. Gazeti liliandika hivi: "Hatua ya kuondoka kwa Aussems huku nyuma ndani ya Simba inataka kutumika kama kumpiga teke chura ..."

Inapoandikwa "... kuondoka kwa Aussems ..." maana yake ni mtu aliyeondoka nyumbani kwa Aussems. Hata hivyo sentensi haikuandikwa ipasavyo. Ingeandikwa:

"Kutokana na Aussems kuondoka, Simba itatumia mwanya huo kumpata m-badala wake na kufanya mabadiliko kwenye benchi la ufundi."

Sentensi ingine ikaandikwa pia kwa kutumia neno 'kwa' kimakosa: "Meneja wa Simba, Patrick Rweyemamu alipoulizwa juu ya kuondoka kwa Ausems alisema kikosi kitakuwa chini ya Kitambi na Abel Zrane ..."

Ingeandikwa: "Meneja wa Simba, Patrick Rweyemamu alipoulizwa kuhusu Aussems kuondoka, alisema timu itakuwa chini ya Kitambi na Abel Zrane ..."

'Kwa' ni neno linalounganisha sentensi mbili. Neno linalotumika kuhusisha tendo na kifaa kitakachotumika kutendea: "Amelima kwa jembe," "alikula kwa kijiko; alikula kwa mkono." Ni kosa kusema "alikula 'na' kijiko" au alikula 'na' mkono" kwani maana yake ni kwamba "alikula na kijiko pamoja" au "alikula pamoja na mkono wake!"

Vilevile 'kwa' ni neno linalotumika kuunganisha vitu viwili katika kulinganisha; neno linalounganisha kitu kimoja na kingine katika utendaji.

Waandishi hushindwa kuandika sentensi kwa mtiririko mzuri: "Bodi ya Simba na hata wanachama na mashabiki wao hawaridhiki na kiwango cha soka kinachopigwa sasa katika timu hiyo na tayari mpango kamili wa kubadilisha sehemu kubwa ya benchi la ufundi hilo inafanyika kwa siri katika kukamilisha kuborwesha timu hiyo." (Maneno 40 katika sentensi moja isiyoeleweka!)

**marobarnabas@yahoo.com**
**0784 334 096**

ELIMU
NA GAUDENSIA MNGUMI

# Kwa jitihada hizi wasichana mshindwe wenyewe kusoma




Wanafunzi wa Shule ya Msingi Kilindoni ya Mafia, wakiwa kwenye mabunge ya wanafunzi, moja ya mbinu inayotumiwa na SVAGs kulinda mabinti dhidi ya unyanyasaji. **PICHA: GAUDENSIA MNGUMI**

KWA mwaka 2015/2016 takribani asilimia 40 ya wanawake wenye miaka kati ya 15-49 walifanyiwa ukatili wa kingono na kwamba 5,902 walibakwa.

Taarifa hizo ni kwa mujibu wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu. Jeshi la Polisi nalo katika takwimu zake linadokeza kuwa mwaka 2016/2017 watoto 2,571 wa kike na kiume walibakwa na kulawitiwa.

Hizo si habari njema masikioni mwa wazazi, walezi na serikali ambayo inagharamia mabilioni ya Shilingi na Dola kuwekeza na kuwezesha miundombinu na wataalamu wa elimu kusomesha watoto.

Lakini, nini kinafanyika kuwasaidia watoto wasome na kuwaepusha na unyanyasaji unaokatisha masomo na kuwalazimisha kuwa wazazi na walezi wenye umri mdogo tena mafukara?

Katika kuzitambua jitihada zinazofanywa na serikali na wadau kumsaidia mtoto hasa binti, mapema mwezi Novemba, Nipashe ilitembelea Wilaya ya Mafia, ambacho ni kisiwa katika Mkoa wa Pwani wakati wa ziara ya wanahabari iliyoandaliwa na shirika la kimataifa la ActionAid Tanzania linalohamasisha maendeleo ya eneo hilo.

Mafia kwa mujibu wa Kaimu Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Wilayani, Yohana Lwende, mambo si shwari kwa mabinti, kwani kiwango cha watoto wanaobakwa, kulawitiwa na kupata mimba katika umri mdogo ni kikubwa.

Anasema wilayani Mafia kuanzia mwaka 2015 hadi 2019 kupitia taarifa za waratibu wa elimu wa kata nane za wilaya hiyo, wanafunzi 21 walipata mimba, watatu walilawitiwa, wane walibakwa wakati mabinti 19 wanatumikishwa kingono.

"Wanatumiwa na wanaume kingono licha ya kwenda shule na wengine walitoroshwa nje ya Mafia na wananyanyaswa kingono," anasema.

Si hivyo tu anaongeza kuwa kati ya mwaka 2018 na 2019 jumla ya makosa 22 ya ukatili wa kingono yaliripotiwa polisi na watuhumiwa 16 walikamatwa huku sita wakiingia mitini.

"Kati ya hayo 13 yalikuwa ubakaji, moja kujaribu kubaka, matano ulawiti na matatu ni kuwapa mimba wanafunzi," anaeleza Lwenda.

### MASANDUKU YA MAONI

Yohana anazitaja juhudi zinazofanyika ikiwamo shirika la Actionaid kushirikiana na Halmashauri ya Mafia kunusuru mabinti kwa kuanzisha mikakati ukiwamo masanduku ya maoni shuleni.

"Masanduka ya maoni yalianzishwa katika shule 40 za Wilaya ya Mafia kwa kushirikiana na asasi ya Sauti ya Wanawake Mafia (Sawama), tulitembelea shule hizo na kupata maoni kwa maandishi kuhusu unyanyasaji," anasema.

> Wanatumiwa na wanaume kingono licha ya kwenda shule na wengine walitoroshwa nje ya Mafia na wananyanyaswa kingono.

Anaeleza kuwa watoto walitaja kuwa wanafanyajiwa ukatili na baba walezi, wajomba, jamaa wa karibu wanaowatishia kuwa iwapo watawataja watawadhuru.

### MABINTI WANUSURIKA

Akizungumzia maelezo ya ulinzi wa mabinti, Mratibu wa ActionAid Mafia, Samwel Mesiaki, anasema shirika limewekeza katika kutetea wasichana kupitia mradi wa kuhamasisha usalama wa wasichana shuleni (Stop Violence Against Girls in Schools- SVAGs).

Aidha, Mafia ni miongoni mwa wilaya ambako wanafunzi wa kike wanakabiliwa na vikwazo vingi katika kufikia ndoto za elimu na kwa mujibu wa utafiti walioufanya kwa wastani wasichana 10 au asilimia (0.2) hukatisha masomo kila mwaka kutokana na mimba za utotoni na unyanyasaji na ukatili wanaokutana nao nyumbani.

"Mmoja kati ya kila wasichana wanne, hukutana na unyanyasaji wa kihisia kutoka kwa jamaa au ndugu wa karibu na kusababisha kupunguza kujithamini na kujiamini, hivyo kupunguza msukumo wa elimu na kusababisha elimu kwa watoto hawa kuonekana kama ni kupoteza rasilimali ,"anaeleza Mesiaki.

Changamoto ni nyingi anasema na mojawapo ni wasichana mmoja katika kila 10 kuripoti kunyanyaswa kingono, wakati zaidi ya nusu wanaripoti kunyanyaswa na walimu.

"Kwa kushirikiana na Sawama ActionAid inatekeleza mradi wa Kutokomeza Vitendo vya Unyanyansaji dhidi ya Wasichana Shuleni. Tumefikia wanafunzi 9, 552, katika vijiji 23, shule za msingi 34 na sita za sekondari. Kati ya wanafunzi 9,552, wasichana ni asilimia 52" anaeleza Mesiaki.

### NDOA ZAPUNGUZA

Jambo la kujivunia analotaja Mesiaki ni pamoja na kupunguza ndoa za utotoni kwa kiwango kikubwa. Ni kwasababu tumekubaliana na tunatekeleza hakuna ndoa inayofungwa bila sheikh wala mchunguji au padri kupata cheti cha ndoa na kuthibitisha umri.

"Kwa mwaka 2015 kesi tisa zinazohusiana na ndoa za utotoni ziliripotiwa. Mwaka 2016 zikawa saba, mwaka 2017 zilikuwa tatu wakati 2018 zilikuwa mbili. Tumezipunguza ni mafanikio," anasema Mesiaki.

### MAHUDHURIO JUU

Aidha, mauhudhurio ya wasichana shuleni yameongezeka na sasa yamefikia asilimia 99.8 jambo linaloashiria kuwa wazazi wana uelewa wa umuhimu wa kusomesha wasichana baada ya kupata elimu ya uhamasishaji.

"Kuongezeka kwa utoaji taarifa kutoka kesi tano mwaka 2016 hadi kufikia kesi 17 mwaka 2017 na kesi 19 mwaka 2018 ni uhalisia wa uelewa wa jamii kuhusu kuripoti taarifa za unyanyasaji ndani ya jamii."

Mratibu wa ActionAid Mafia, anasema hayo yamefanyika kupitia kuunda mifumo na mitandao ya kijamii ya ulinzi wa wasichana.

### MCHANGO WA KINAMAMA

Sauti ya Wanawake Mafia (Sawama) ambaye ni mdau wa kutetea haki za wasichana kupitia miduara ya kinamana imewaelimisha wanawake na mabinti katika maeneo yote wilayani humu kuhusu ulinzi wa watoto na kuripoti matukio ya unyanyasaji.

Mwezeshaji wa Sawama, Fatuma Mohamed, anasema wanawake, wanaishukuru ActionAid kwa kuwaanzishia miduara hiyo ambayo imewaamsha, kuibua, kujadiliana na kumaliza changamoto za matatizo yao kwa pamoja.

Kwa kutumia miduara wanafuatilia ulinzi wa mabinti, wanafikisha kesi mbele ya vyombo vya dola, na pia wanawaelimisha wenzao kuhusu athari za unyanyasaji watoto katika mikusanyiko ya kijamii kama kwenye harusi na mikutano ya kiserikali, anasema Mwanaimani Abdallah.

### UFUMBUZI

Pamoja na kuwapo sheria ya kifungo cha miaka 30 jela kinachotolewa na Kanuni ya Adhabu, wanawake hawa wanataka kuwe na sheria ndogo ndogo za vijiji na halmashauri kuogopesha watu wasiwanyanyase watoto.

Wanashauri kila anayebaka alipe Sh. 500,000 kwa serikali ya kijiji. Aidha, mali zake kama nyumba, pikipiki zitumiwe kugharamia watoto aliowaumiza. Sawama wanataka sheria ndogo zimbane anayetelekeza familia kulipa Sh 1,000,000 na mali zake kuwekwa mikononi mwa serikali ya kijiji ili zihudumie familia.

Kwa wazazi na walezi wanashauri sheria hizo ziwabane washitakiwe na kuadhibiwa iwapo watoto wao watabakwa, kupata ujauzito lakini wakawaficha na kuwalinda watuhumiwa.

ELIMU

**NA BEATRICE MOSES**

# Ofisa Elimu Ilala afunguka mzizi wao kunga'ra darasa saba kitaifa

## • Walishikamana kuunda kikosi ushindi • Mitihani majaribio ilikuwa kila kukicha • Pekee Kiingereza serikalini 'haijambo'

MKOA wa Dar es Salaam, ndiyo ulioibuka kinara kwa miaka mitatu mfululizo, aliyepata matokeo mazuri kwenye Mtihani wa Taifa wa Darasa la Saba, unaondaliwa na Baraza la Mitihani Tanzania (Necta). Hiyo ni tangu mwaka 2017.

Mafaniko hayo ya kimkoa, ni wazi yamechangiwa na bora wa viongozi wa sekta ya elimu katika ngazi mbalimbali, ikiwamo wilaya. Hapo ndipo inapoibuka Halmashauri ya Wilaya ya Ilala, iliyoshika nafasi ya tano kitaifa, katika orodha ya 10 bora.

Ofisa Elimu Taaluma wa Wilaya ya Ilala, Rehema Msologonhe, anaeleza mafanikio yanayotokana na kufanya kazi katika sura ya timu moja.

Ni mapambano yanayoongozwa na kikosi kazi kilichoongozwa chini ya Ofisa Elimu wa Wilaya Ilala, Elizabeth Thomas, akiunga mkono na maofisa wengine wa elimu ya msingi, walimu, wanafunzi, wazazi , walezi, kamati za shule na wadau kwa ujumla.

"Kila mmoja alishika nafasi yake kwa kadri alivyoweza au alivyoelekezwa. Jambo la kufurahisha, tumefanikiwa. Kipekee tunashukuru Mungu na ushirikiano mzuri wa walimu wetu," anasema.

Elizabeth anabainisha kuwa walikuwa na jumla ya watahiniwa 25628 waliosajiliwa kufanya mtihani kati yao 23956 walifaulu.

Alifafanua kuwa kati ya waliofaulu wasichana ni 12431 wavulana ni 11425, sasa wanasubiri kupangiwa shule za sekondari ili kuendelea na masomo.

Elizabeth anasema, katika orodha kuna wanafunzi 284 ambao hawakufanya mtihani, kati uwiano wavulana 180 na wasichana 104, katika jumla ya shule za msingi 212 wilayani.

Anasema katika orodha hiyo, kuna 96 ni zilizoko katika mfumo wa Kiingereza, mbili kati yake zunamilkiwa na serikali, ambazo ni: Diamond na Olympio na zilzobaki 14 ni za mfumo wa Kiswahili, zote zinamilikiwa na serikali.

### SIRI MAFANIKIO

Ofisa Elimu huyo anaeleza, wanafunzi walikuwa wakipewa mitihani ya majiribio kila mara na baadhi yake ni ya miaka iliyopita walioifanya kwa kushindanishwa kwa ngazi mbalimbali zilizowekwa.

Elizabeth anaeleza cha kuwafurahisha wanafunzi walikuwa na ari kubwa ya kushiriki kutokana na hamasa waliyopewa na walimu wao.



Aliyekuwa Waziri wa Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi, Mhandisi Stella Manyanya, alipowatembelea darasani wanafunzi wa Shule ya Msingi Olympio, Upanga, Dar es Salaam. **PICHA: TOVUTI YA WIZARA.**

> Kamati ya shule imejipanga kuibua vyanzo kadhaa vya fedha za mradi wa ujenzi huo, ambavyo aliahidi atavitaja baadaye.





Watahiniwa walipokuwa katika chumba cha mtihani wa darasa la saba. Ofisa Elimu wa Wilaya ya Ilala, Elizabeth Thomas. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

"Mashindano yao ya mitihani ya kujipima ilianzia katika ngazi ya kata, wilaya hadi mkoa, wanafunzi bora kutoka shule moja walishindanishwa na shule nyingine. Hii ilifanywa kwa shule za serikali na binafsi zilikuwa na mikakati yao," anasema.

Kwa kawaida, shule binafsi kupitia umoja wao uitwao Ngopso, hufanya mikakati yao ukiwamo mitihani ya kuwanoa, kuwapa umahiri wanafunzi wao.

Ofisa Elimu - Ilala, Elizabeth, anasema washindani waligawanywa katika maeneo manne, ambayo ni Gerezani, Chanika, Ukonga na Kimanga, na mwanafunzi akipita kwenye mtihani wa kata ndiyo anakwenda kufanya katika ngazi hiyo ya juu.

Anaeleza matokeo ya mitihani hiyo yalitoa mwelekeo mzuri, hata kwenye mtihani wa majaribuo ya mkoa (mock) ilionyesha dalili njema kwa wanafunzi waliopo .

"Japo hawakufikia lengo letu katika mtihani huu wa taifa, kwani tuliamini miongoni mwao kuingia kwenye 10 ya taifa, lakini tunafurahi wengi wamepata ufaulu mzuri, tunaendelea kujiandaa vizuri kwa mitihani mingine," anasema.

### KAMATI ZA SHULE

Ofisa Elimu huyo anasema, kuwa wazazi wengi walio makini wamekuwa wakifuatilia kwa karibu maendeleo ya watoto wao, hata kufika shuleni kuwasiliana na walimu wao.

"Ukweli ni kwamba, wazazi wengi wamekuwa wakifuatilia kwa karibu zaidi watoto wao kwenye madarasa ya mitihani. Wameonyesha ushirikiano mzuri ambao nao kwa namna moja umefanikisha ufaulu huu, " anasema.

Ofisa huyo anatoa ari wazazi na walezi kuendelea na umakini kwenye malezi ya watoto hao , ikiwamo kufuatilia nyendo zao, kuhakikisha wanakua katika maadili mazuri kwa maendeleo ya taifa.

"Kuna vitendo vya kikatili ambavyo baadhi ya watoto wamekumbana navyo vimewaathiri. Hata hivyo, inaonyesha kuna baadhi ya wazazi hawapo makini katika kufuatilia watoto wawapo nyumbani, badala yake walimu ndiyo wamekuwa wakigundua wanapoona mtoto hana furaha au utulivu kwenye masomo," anasema.

Anapongeza kamati za shule kwamba zimesaidia kuratibu, kusimamia na kudhibiti rasilimali zake, hivyo kuwezesha ufanisi katika utekelezaji mpango wa jumla wa maendeleo ya shule.

### SHULE OLYMPIO

Hiyo iliyoko Upanga jijini Dar es Salaam, ni ya mchepuo wa Kingereza na ndiyo iliyoongoza kuwa na idadi klubwa ya watahiniwa darasa la saba wilayani Ilala.

Kwa mujibu wa matokeo yaliyotangazwa na Baraza la Mtihani(Necta ), shule hiyo ilianzishwa mwaka 1956. Wanafunzi wake waliofanya mtihani mwaka huu, walikuwa 431; wasichana 220 na wavulana 211. Wote wamefaulu mtihani huo.

Ni matokeo yanayoonyesha wanafunzi 243 walipata alama 'A' kati yao wasichana 69 na wavulana 174 na waliopata alama 'B' walikuwa 179, kati yao wasichana 142 na wavulana 37. Wengine tisa ambao wote ni wasichana, walipata alama 'C'.

Mwenyekiti wa Kamati ya Shule, Amiry Rajab, anawapongeza walimu wa shule hiyo chini ya uongozi wa Mwalimu, Mkuu, Salim Mgamba, kwa kushika nafasi ya saba, kati ya shule 90 za wilaya hiyo.

Pia, kimkoa imeshika nafasi ya 34 kati ya 459 kimkoa. Rajaba anafafanua: "Wanajituma vyema katika kati yao, matokeo yanathibitisha hilo, kwani licha ya kukabiliwa na changamoto ya idadi kubwa ya wanafunzi wameweza kuwajengea uwezo wanafunzi wote kufanya vyema mtihani huo."

Anaeleza imani yake, matokeo yatawatia moyo wazazi kushiriki kuikwamua shule kwenye matatizo mbalimbali yanayoangukia katika wajibu wao wa msingi shuleni hapo.

"Kamati imeiona changamoto ya idadi kubwa ya wanafunzi, tuna mpango wa kujenga jengo jipya litakalokuwa na madarasa kadhaa, maktaba na shule ya awali," anasema.

Anasema, kamati ya shule imejipanga kuibua vyanzo kadhaa vya fedha za mradi wa ujenzi huo, ambavyo aliahidi atavitaja baadaye.

Rajab anasema, jengo jipya litakalokamilika litawapa nafasi walimu kufundisha kwa uhuru zaidi, wakiwa na imani kuwa chanzo cha hatua zaidi ya ufaulu kwa wanafunzi.

Olympio ina wasifu mwingine wa kuwahi kutunukiwa cheti cha pongezi kutoka Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), kwa kushika nafasi ya tatu kati ya shule 20 bora za serikali zilizofanya vizuri Mtihani wa Taifa Mwaka 2018.

Shule nyingine zilizokuwa na watahiniwa wengi ni pamoja na Kivule (417) iliyoko Kitunda, Minazi Mirefu (415) ya Ukonga.

### WANAFUNZI WACHACHE

Shule ya Msingi Amana iliyoko Ilala, ndio ilikuwa na wahitimu wachache zaidi, ikilinganishwa na nyingine za wilayani Ilala, ambao ni 24.

Katika shule hiyo, hapakuwapo mwanafunzi aliyepata alama 'A'; 18 walipata alama 'B' kati yao wasichana 10 na wavulana 8 na watahiniwa sita walipata alama 'C' inayojumuisha msichana mmoja wavulana watano.

HAKI, UWAJIBIKAJI & VITA YA RUSHWA

# Ubia wake na ushirikishaji



Wakazi wa kijiji cha Ngabolo, wakimuuliza maswali ya ushirikishwaji, mbunge wao Emannuel Papian (hayupo pichani), katika mkutano wa hadhara uliofanyika kijijini Ngabolo, wilayani Kiteto. **PICHA: TOVUTI WILAYA YA KITETO**

**Na Niko Kasera**

UHUSISHWAJI ni dhana muhimu katika tasnia ya Utawala Bora na imeendelea kushika kasi kwa namna mbalimbali.

Serikali imeshaweka wazi umuhimu wa kuwahusisha wananchi moja kwa moja kwenye miradi ya maendeleo.

Msingi wa uhusishwaji unaanza na ngazi ya utambuzi wa wadau wote kwenye utekelezaji miradi ya maendeleo. Pasipo utambuzi wa wadau hawa, ni bayana miradi itakosa nyenzo mojawapo muhimu ambayo ni umiliki wake

Nitoe mfano mmoja wa lililotokea hapa mkoani Morogoro, katika chuo kikuu kimojwapo katika miaka kadhaa iliyopita, kilibaini wanakijiji waliofuata huduma ya maji safi na salama chuoni hapo.

Ili kuwapunguzia adha ya kuhangaikia maji, uongozi wa chuo uliamua kuwasaidia wanakijiji wapate maji jirani na makazi yao.

Kwa maana hiyo, chuo kilitoa mabomba ambayo idadi yake ingetosha kusambaza maji kutoka chuoni hadi kijijini. Kama ilivyo ada, wanakijiji walihusishwa na hilo na wakaombwa wachangie nguvu kazi kwa kuchimba mitaro ili yatumike kulaza mabomba.

Ajabu ni kwamba, wanakijiji waligoma kutoa mchango wao, huku baadhi wakihoji kwa kauli:"Iweje mfadhili aanze kutuomba sisi tuchangie nguvu kazi bila malipo. Waombaji wananufaika na ardhi yetu, wafadhili aina gani hawa?"

Pamoja na nia njema hiyo na kuhusishwa kwenye mradi, matokeo yake haukufanikiwa wakati huo, hadi hivi karibuni serikali tena ilipojitolea kuwashirikisha 'mwanzo mwisho' wanakijiji wale.

Tunachojifunza na simulizi hiyo ni kwamba kazi bado tunayo. Katika jamii wapo wengi bado ni waumini wa dhana ya misaada na wafadhili na hawajapokea mageuzi ya kuwa washiriki. Hilo linaangukia kauli ya Rais Dk John Magufuli, ambaye kila kukicha anatoa rai kuhusu haja ya uwajibikaji kwa Watanzania.

Bila kupokea na kuzingatia uwajibikaji, itajenga vizingiti vya taifa kufikia dira na malengo yake, ikiwamo safari ya kuipata Tanzania ya Viwanda na Uchumi wa Kati, ifikapo mwaka 2025.

Dhana ya uwajibikaji ndio inabeba msingi wa kujituma, haki, weledi na utawala bora.

Asasi za Kiraia ambazo ni wabia wakubwa wa maendeleo zinaisaidia serikali kwenye dhana nzima ya maendeleo kwa namna ambazo zimeajiri na zinalipa kodi na tozo mbalimbali.

Ni dhahiri kwamba, zinatoa ushirikiano kwenye sekta zote nchini, iwe za umma au binafsi. Kuna ufanisi wa hali ya juu unaopigiwa debe, ubabaishaji unapigwa vita na kukemewa.

Taratibu, utamaduni wa kitaifa wa kuwekeza kwenye tunu za thamani kama vile uchapaji kazi, uadilifu, uwajibikaji kujitolea na kadhalika, hujengeka.

Daima nchi ya namna hiyo watu wake hutembea wakijiamini, kuelekea mustakabali wao huku wakiamini kuna siku njema mbele ya safari.

Viongozi wa nchi zilizoendelea au zilizo katika njia ya kuelekea kwenye maendeleo, hawategemewi kuwa na mengi mapya tofauti kila kukicha, maana dira na malengo inajulikana kwa kila mmoja wao.

**Mwandishi anapatikana kupitia barua pepe: samawatiarts@yahoo.com**

## JE, WAJUA?

## NA REUBENI LUMBAGALA

# Uking'ara kitaaluma ni lazima utaibuliwa



Katibu Mtendaji wa Necta, Dk Msonde akimpa zawadi mwanafunzi bora wa Sekondari ya Ihsan, Rahma Ngaja hivi karibuni. **PICHA: MIRAJI MSALA**

MOTISHA ni kichocheo katika kuchagiza ufanisi na utendaji kazi mahiri na wenye kutoa matokeo chanya. Ni hatua ya kuthamini kazi nzuri iliyofanywa na mtu mwingine katika kuleta mabadiliko ambayo ni chachu ya mwendelezo wa mambo bora zaidi ya sasa na baadaye.

Hivi karibuni, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Suleiman Jafo, amekuwa shuhuda wa utoaji Tuzo za Elimu kwa wanafunzi na walimu na shule zilizofanya vizuri kwenye matokeo ya mitihani ya kidato cha sita na darasa la saba kwa mwaka 2019, na kusema kuwa ni chachu ya kuendeleza kazi za kutukuka.

Katika hafla hiyo, Waziri Jafo anatoa fursa kwa wanafunzi waliofanya vyema katika mitihani ya darasa la saba kuchagua shule za sekondari wanazozipenda ili kuendelea na masomo yao.

Anasema kwa wa kidato cha sita Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, iliachiwa wanafunzi wa kidato cha sita ili iweze kuwasaidia kujiunga na vyuo vikuu wavipendavyo. Waziri anasema "Yule kijana Tanzania One nilimsikia anasema anatamani kwenda Shule ya Sekondari Ilboru nitashangaa sana kama hatakwenda huko, hawa ni vijana spesho waambieni wachague shule wanazotaka waende kusoma.

"Naomba niwahakikishie, Rais John Magufuli na serikali anawapenda sana, mtachagua shule zile mnazotaka ninyi kwenda kusoma, Katibu Mkuu shughulikia hilo".

Uhuru waliopewa wanafunzi kuchagua shule na vyuo wanavyovitaka ni motisha kubwa kwani wakati mwingine licha ya kufanya vizuri wanasoma katika shule ambazo hazikuwa matarajio yao na hilo huenda linawavunja moyo kwa sehemu.

Tuzo na zawadi hizo zilizotolewa kwa walimu na wanafunzi zitachechemua kwa kiasi kikubwa ukuaji wa taaluma mashuleni. Wanafunzi na walimu, kila mmoja ataongeza ari katika usomaji na ufundishaji ili kuendelea kupata tuzo na zawadi hizo mara nyingi zaidi.

Ni vyema tuzo hizi zikawa ni jambo endelevu ili kuendelea kujenga shauku kwa walimu na wanafunzi kujituma zaidi. Motisha ni eneo muhimu linalohitaji uwekezaji ili kuongeza tija ya kazi.

Katika sehemu mbalimbali kama maeneo ya kazi, taasisi za elimu, kampuni za umma na binafsi na katika familia utoaji wa motisha ni jambo jema ambalo linahamasisha matokeo chanya na utendaji kazi wenye kasi na viwango. Ndiyo maana katika katika kuziangazia nafasi za tuzo na zawadi katika kuchochea ukuaji wa taaluma kwa shule za msingi na sekondari nchini ni jambo muhimu.

Sekta ya elimu ni muhimu kwa maendeleo ya kila nyanja kama vile kijamii, kiuchumi na hata kisiasa. Kutokana na umuhimu wa elimu, kumekuwa na mikakati ya kuifanya itoe matokeo chanya hasa kwa wanafunzi ambao wapo shuleni kwa ajili ya kusaka maarifa, ujuzi na stadi mbalimbali. Mkakati mmojawapo wa kuchagiza ukuaji wa taaluma ni pamoja na utoaji wa tuzo kwa wanafunzi na walimu kama njia ya kuwahamasisha kujifunza na kufundisha kwa bidii, nidhamu na weledi ili matunda ya elimu hiyo yaweze kuonekana kwa wahusika.

Pamoja na kuwa mwanafunzi anao wajibu wa msingi wa kusoma kwa bidii, kujifunza bila kuchoka na kujituma katika masomo, lakini upo umuhimu wa kuthamini kazi nzuri iliyofanywa na wanafunzi hadi kufanya vizuri katika masomo yao kwa kutoa tuzo na zawadi kwa wahitimu wetu.

Halikadhalika, walimu nao wanao wajibu wa msingi wa kufundisha kwa bidii, kujituma katika majukumu yao, aidha, ipo haja ya kuthamini kazi za walimu kwa kutoa tuzo na zawadi kwa wale ambao masomo yao yamefanya vizuri katika mitihani ya taifa.

Katika hafla hiyo ya utoaji tuzo iliyoratibiwa na Taasisi ya Elimu ya Global Education Link kwa kushirikiana na Baraza Mitihani Tanzania (Necta) na kufanyika jijini Dar es Salaam, Jafo anasema tuzo hizi ni chachu ya ukuaji wa taaluma na kuongeza ufaulu kwa wanafunzi.

"Hizi ni tuzo za kwanza kutolewa na serikali kwani vijana na walimu waliofanya vizuri kwenye mtihani hiyo wanastahili pongezi ili waendelee kufanya vizuri. Tunaamini itaongeza ubora zaidi kwa shule zetu kuendelea kufanya vizuri" anasisitiza Jafo.

Jambo la kipekee katika tuzo hizi ni kwamba wanafunzi na walimu kwa pamoja wanathaminiwa kwani hawa wawili wanategemeana katika kufikia mafaniko ya kitaaluma. Kama walimu watajituma kufundisha kikamilifu na kwa mujibu wa mitaala, huku wanafunzi wakishindwa kujisomea kwa bidii, juhudi za walimu hazitazaa matunda yanayotarajiwa.

Vivyo hivyo kwa wanafunzi ambao wanapenda kusoma huku wakikosa walimu wa kuwafundisha watashindwa kufikia malengo yao ya kufaulu masomoni kwa viwango vya juu. Kwahiyo, ni vyema matokeo mazuri yanapotokea, kila mmoja yaani mwalimu na mwanafunzi kutambuliwa mchango wake katika mafanikio hayo kwani kwa pamoja watakuwa wameweze-sha kufikia mafanikio hayo.

***Tafakari.***

***Reubeni Lumbagala ni Mwalimu wa Shule ya Sekondari Mlali iliyoko wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma.***

***Maoni: (+255) 764 666349.***

## RIPOTI

# Ukarimu unasaidia kuishi muda mrefu

UKARIMU gani unaweza kuufanya? Ni sawa mtu kuonyesha hisia zake?

Inawezekana kuna ukweli, wanasayansi na wasomi katika kituo cha utafiti wanasema kuwa mtu anaweza kufanya mambo mengi zaidi ya ukarimu na kuongeza muda wa kuishi.

Wafanyakazi wa taasisi ya ukarimu ya Bedari ya Chuo Kikuu cha California, huko Los Angeles (UCLA) wako tayari kwa ajili ya utani.

"Tukiangalia upande wa kisayansi . Ni kama tuko kwenye mzunguko, hapa tunazungumzia upande wa kisaikolojia na kibaiolojia," Daniel Fessler, mkurugenzi wa taasisi anaeleza.

Anasema suala la mtu kuwa mkarimu limechukua vichwa vya habari hivi karibuni.

Rais wa zamani wa Marekani Barack Obama anasema kuwa:"Kuwa jasiri ni ukarimu. Hakuna ubaya kwa mtu kuwa dhaifu au kuwa na huruma."

"Mtu kuwajali watu wengine si udhaifu. Ni jambo jema, tunapaswa kujali wengine kwa kuwa na uadilifu na kuwajali wengine kwa heshima."

Ellen DeGeneres aliwahi kuzungumzia ukarimu wakati akizungumzia urafiki wake na George W Bush:

"Ninaposema kuwa mkarimu, 'Unapaswa kuwa mkarimu kwa wengine, simaanishi kama watu wanafikiria sawa na vile wanavyotenda. Ninachomaanisha ni kwamba uwe mkarimu kwa kila mtu bila kujali.'"

Leo ikiwa siku ya ukarimu duniani (Novemba 13) Tunaangazia ukarimu una maana gani na kujiuliza kwa nini ni muhimu?

Hilo ndilo jambo ambalo wataalamu wanataka kufanyia utafiti.

Je, wako makini , je ni suala ambalo linazingatia uhai na vifo vya watu. Kazi ya Fessler ilikuwa ni kuangalia namna ambavyo watu wanaweza kushawishika kufanya vitendo vya ukarimu, kwa kushuhudia fadhila na kueneza ukarimu.

"Nadhani ni sawa kusema kuwa tunaishi katika umri ambao sio rafiki," alisema.

"Duniani kote, kile tunachokiona ni ongezeko la migogoro baina ya watu ambao wana maoni tofauti katika masuala ya kisiasa au tofauti za kiimani."

Ukarimu, anasema kuwa ni "fikra, hisia na imani ambayo ina uhusiano na hatua ambazo zinaweza kuwanufaisha wengine, Kuwanufaisha wengine haimaanishi kuwa ndio mwisho."

Na kutokuwa mkarimu kwa upande mwingine ni jambo a lisilovumilika kutokana na watu kupunguza thamani kwa wengine. Fessler anasema kuwa msongo wa mawazo ni miongoni mwa changamoto.

Kuishi na watu wanaokutendea vizuri ni bora, kuliko kuishi kwa hofu na mbaya zaidi kunafupisha maisha yako. Kuishi na watu kwa ukarimu , na kuonyesha namna mtu anaweza kuwa mkarimu wa wengine kunasaidia mtu kutopata tatizo la shinikizo la damu.


Kuna faida za kukabiliana na msongo wa mawazo na wasiwasi. **BBC**



ELIMU

NA MICHAEL ENEZA

# Mnapotaka tusema 'kuonesha' na si 'kuonyesha' mnakanganya




BAADHI ya wataalamu wa Kiswahili, kutokana na mazoea, wameanza kusanifisha kutumika kama Kiswahili sahihi siyo 'sanifu' kwani kusanifu ni kutunga, kuremba na siyo usahihi wa kina neno 'kuonesha' wakisema linatokana na'kuona.'

Wanadai kuwa neno 'kuonyesha' linatokana na 'kuonya' jambo ambalo siyo sahihi kabisa na kwa maana hiyo neno halisi ni 'kuonesha' wakati neno hilo lilizuka miaka ya 1990 hadi 2000 kutokana na udhaifu tu wa matamshi na watu wengine wakaiga, wakazoea.

Siyo jambo la ajabu kwani yako maneno kadhaa yanayotokana na matamshi, ishindikane kurekebisha.

Neno lingine ambalo wataalamu hao wamekuwa wakilitangaza kuwa ni sahihi wakati kinyume chake hakina matatizo yoyote katika lugha ni dawa kutumika kila mahali, na 'madawa' siyo sahihi kokote pale, jambo ambalo linashangaza. Hapo pia walianza kutumia watu fulani dhana ya 'dawa za kulevya' katika vyombo vya habari zaidi ya miaka 10 iliyopita na hatua kwa hatua ikaanza kuonekana kuwa ni matumizi sahihi wakati ni kupendelea tu kusema hivyo, bila uhakika wa usahihi wake.

Kwani 'dawa' ni ishara ya kitu chema, wakati 'madawa' ni aina kadhaa za vitu vinavyodhuru vinavyofanana na 'dawa,' kwa umbile.

Dhana ya 'madawa ya kulevya' ina chembe ya kuchukia 'dawa' hizo zinazodhuru mwili, wakati dhana ya 'dawa za kulevya' inatoa ishara kuwa anayetumia anadhani anachukua dawa, kujisitiri au kupunguza makali ya ugonjwa fulani, iwe ni 'kulevya' kama ilivyo malaria, au mwingine. Huwezi kusema neno 'dawa za kulevya' ni sahihi au halipingiki bila kuonyesha dhamira ya 'dawa' katika usemi huo, kwa mfano mtu akisema 'dawa ya panya' ni sahihi kwa sababu ni dawa kwa binadamu ambaye anahangaika na baa la panya nyumbani kwake.

Ukweli halisi ni kuwa ni 'sumu ya panya' ila ni 'dawa' kwa hitaji la kuondoa tatizo hilo jambo ambalo halipo katika 'dawa za kulevya' kwani hazitibu chochote, ni haribifu.

Yako maneno kadhaa yanayotokana na matamshi, na mara nyingine kwa sababu ya mchanganyiko wa jamii zenye mikondo tofauti ya lugha, hivyo anaweza kutamka neno mhadhiri eneo fulani asiyeweza kusema 'kupapasa,' kwani lugha ya Kiarabu kwa mfano ina tatizo kubwa na herufi 'p' inapenda kubadili iwe 'b.' Hivyo aliyekuwa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa Boutros Boutros-Ghali angeandika jina lake kwa Kiyunani (Kigiriki) lingesomeka Petros Petros-Ghali lakini kwa Kiarabu linakuwa Boutros, kwani wana shida kubwa na herufi 'p.'

Sasa anatokea mhadhiri hawezi kusema 'imani ya kupapasa' anasema 'b' halafu wanaomsikiliza wanasanifu neno 'imani ya kibubusa,' na inatumika hivyo hadi sasa.

Kuna tofauti kiasi fulani kati ya 'kupapasa' na 'kibubusa' kwa mtu anayesikiliza, na la kushangaza ni kuwa hilo neno lililosanifiwa linatosheleza haja ya kihisia kama lile la kwanza, kwani 'kupapasa' ni kutojua usahihi wa kitu uko wapi. 'Kibubusa' kinaashiria u-bubu wa jambo fulani, kigugumizi, yaani mkwamo wa kihisia au kufafanua kiini cha jambo fulani, hali inayomaanisha au kuashiria hali kama ile ya 'kupapasa' ambako ishara inakuja kutokana na kushindwa kujieleza.

Ni kupapasa kwa mdomo au akili badala ya kupapasa kwa mkono, au 'kupapasa' kwa kutafuta nukuu mahali kuthibitisha usemi, uikose...

Cha kushangaza katika maelezo ya wataalamu wa Baraza la Kiswahili la Taifa (Bakita ) ni dai kuwa neno onyesha linatokana na 'kuonya' kwa hakika ni uwongo mtupu.

Ni hali ambayo mtaalamu anaona lugha hiyo ni mali ya Bakita , wanafanyia maamuzi wanayotaka, hata kutunga sababu isiyo sahihi ya neno 'kuonyesha.' Kuonyesha ni neno linalojitegemea, kusisitiza kuona na kuliwezesha hilo kwa mwingine.

Ukisikiliza kutamka 'kuonesha' bila kuwa na sababu ya usanifu wa neno hilo kutoka kwa mtaalamu wa Bakita au Taasisi ya Taaluma za Kiswahili (Tataki) wenzao wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, unapata picha ya ulegevu ule ule wa matamshi kama 'kibubusa.' Ni tatizo la kutamka maneno linalotokana na lugha ya asili ya mzungumzaji, kwa mfano yako maeneo nchini ambako kutamka kwa usahihi 'lira' na 'rila' itamchukua takriban mwezi ajifunze hilo, na kama wangekuwa ndiyo wako maeneo ya pwani wametawala lugha ya Kiswahili, si ajabu usanifu ungekubali mchanganyiko huo.

Ipo michanganyiko ya ki-pwani waliyoisanifu kitambo, mojawapo ya michanganyiko hiyo ya matamshi ambayo wataalamu wenye kuzingatia matamshi ya eneo la pwani au mikusanyiko ya aina hiyo ni kuharibu matumizi ya herufi 't' ambayo ni matamshi ya awali na kuingiza herufi 'd' .

Awali tulijifunza neno 'kutarizi,' lakini haikupita miaka mingi likaanza kupenyeza neno 'kudarizi,' na si ajabu ukiangalia huko katika kamusi za wana-pwani utakuta Kiswahili Sanifu ni 'kudarizi.'

> Ni hulka iliyotokana na miaka mingi ya kujenga uhusiano kwanza dhidi ya ukoloni na halafu 'mabaki ya ukoloni' baada ya Azimio la Arusha.

Ni mazingira ya 'kesi ya nguruwe unampelekea ngiri' pale Kiwahili kinapovurugwa na matamshi mazito ya pwani, halafu waseme '..naam!'

Hata ukiangalia tofauti ya neno 'kuonyesha' na 'kuonesha' unakuta ni uvivu tu wa matamshi na kutafuta njia rahisi ya kukubali neno hilo kutowaumbua wazee wa ki-pwani ambao kwa jadi ni 'wasafiri wenza' wa wataalamu wa Kiswahili.

Ni hulka iliyotokana na miaka mingi ya kujenga mahusiano kwanza dhidi ya ukoloni na halafu 'mabaki ya ukoloni' baada ya Azimio la Arusha.

Ingekuwa kweli wanatafuta vyanzo, neno 'kuonyesha' halikaribiani na 'kuonya' kwani ni vitu viwili tofauti, ila linaweza kukaribiana na 'kunyesha' kwani ina chimbuko linalofanana.

Aliyesema neno 'kuonyesha' msingi wake ni 'kuonya' anaashiria kuwa huwezi kuwa na neno kama hilo nje ya haja ya 'kuonya' ijengewe humo, kitu ambacho siyo sahihi. Maneno yenye 'ny..' na ziada ya a,e, i, o, u ni mengi tu, iwe ni 'nyama' au 'nyesha' hivyo 'kuonyesha' haihitaji 'kuonya,' kwani kuonya inaashiria hitaji la maadili, wakati kinachotakiwa hapa ni kuona tu, kwa mfano 'kuonyesha' mvua ilivyo-nyesha...



WADAU
**SABATO KASIKA**

# Sauti za wadau

Elimu ni moja ya haki za mtoto, lakini wapo baadhi ya wazazi, ambao kwa sababu wanazozijua wenyewe, hawawapeleki watoto shule, na kusababisha wakose haki hiyo. Wadau wanasemaje?



**JUMA HAMIS (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)**

KUMNYIMA mtoto elimu ni ukatili, na wanaofanya hivyo wajue kuwa huwawezi kuwanyima watoto haki ya kupata elimu wakabaki salama, waweza kujikuta katika maisha duni.

Serikali yetu imekuwa ikituhimiza kusomesha watoto na kuwaeleza umuhimu wa elimu, lakini inasikitisha kusikia bado wapo baadhi ya watu hawaelewi hilo.

Kwa sasa serikali inatoa elimu bure kuanzia shule ya msingi hadi kidato cha nne. Kwanini tusitumie fursa hii kusomesha watoto wetu kwa ajili ya maendeleo yao ya baadaye?

Kimsingi elimu ni moja ya haki muhimu za mtoto awe wa kiume au wa kike, ingawa kuna baadhi ya jamii zinamuona mtoto wa kike kama hafai kupata elimu na badala yake kuwa kitegauchumi cha familia.

Naomba nitoe wito kwa wazazi wenzangu kwamba vyema kutenda mema kwa watoto ikiwa ni pamoja na kuwapa elimu ambayo ndiyo urithi muhimu katika maisha yao.

Yaani wazazi tuwekeze elimu kwa watoto ili baadaye waavune walichopanda, lakini kama wataendelea kuwapo wale wasiowapeleka watoto wao shule, wajue kuwa mtindo huo ni sawa na kuendelea kumkumbatia adui ujinga ambaye alitangaziwa vita mara tu baada ya nchi hii kupata uhuru mwaka 1961.

Tuendelee kuunga mkono juhudi za serikali za kutoa elimu bure kwa kuwapeleka watoto wetu shule.

Nafasi hii ya kusoma bure kuanzia shule ya msingi hadi kidato cha nne siyo ya kupita tu bali ni ya kuchangamkiwa na kila mzazi, awe mwenye uwezo kifedha na hata asiyekuwa na uwezo huo.



**JOHN SAMBU (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)**

ELIMU ni kati ya haki msingi za kibinadamu. Ni kutokana na umuhimu wa elimu katika jamii, Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa, Desemba 2018 likaazimia kuanzishwa kwa Siku ya Elimu Duniani, itakayokuwa inasherehekewa Januari 24 ya kila mwaka.

Lengo ni kuwezesha kila mtu kusoma, kujifunza na kuhakikisha kwamba, binadamu wote wanafikia vipawa vyao kikamilifu. Nimejaribu kugusia hapo kidogo, lakini kwa ujumla ni kwamba ninajua wapo baadhi ya wazazi, ambao kwa kweli hawana nyuma ama mbele wanahitaji kusaidiwa kwa kila hali, ili watoto wao wasome, hawa siwezi kuwalaumu ila wale, ambao kwa makusudi hawataki kusomesha watoto wao huku wakiwa na uwezo wa kiuchumi, ni vizuri watakambua kuwa wanawanyima watoto haki ya msingi.

Ni wajibu wa mzazi au mlezi kumpa mtoto elimu. Mtindo huu wa kutopeleka watoto shule inaendekezwa na baadhi ya wazazi na walezi, ambao mimi ninawaona kama hawafai kuitwa wazazi kwa kushindwa kuwajibika ipasavyo kama wazazi.

Ni ajabu kuona au kusikia katika dunia ya leo kuna wazazi na walezi hawataki kuwasomesha watoto wao.

Ninadhani ipo haja ya kurudi kwenye mfumo wa zamani wa kuwa na wajumbe wa nyumba kumi ambao pamoja na mambo mengine watakuwa na kazi ya kufuatilia katika maeneo hayo ili kujua kama kuna watoto hawapelekwi shule na kwa sababu gani, ili iwe rahisi kubaini wazazi na walezi wasiopeleka watoto shule kwa makusudi na kuwachukulia hatua za kisheria.



**JONATHAN MANGA (MKAZI WA BUNDA, MARA)**


SUALA la mtoto kupata elimu halina mjadala, kwani hiyo ni haki yake ya msingi. Sasa wanapokuwapo wazazi na walezi wasiosomesha watoto wao, ni dalili kwamba bado tuko nyuma, hatujawa na mwamko wa kutosha katika elimu, ni bora tusaidiwe ilii tubadilike.

Inawezekana wazazi kama hao ndiyo wale ambao watoto wakisomeshwa na watu wengine kisha wakawa na maisha mazuri, wanajisogeza ili kusaidiwa, wanahasau kwamba elimu ambayo walikuwa wakikataa kuwapa ndiyo imewafikisha watoto hapo walipo.

Katika mfumo wa maisha yetu, kila mzazi anatakiwa kumpeleka mtoto wake shule ili naye baadaye ale matunda ya kusomesha ingawa siyo lazima. Iwapo wazazi wana maisha duni, ni vyema hali hiyo ijulikane kuliko kunyamaza tu wakati watoto wanakosa elimu.

Ninajua suala hili lina upana wake na unaweza kukuta wazazi wote wawili wana matatizo ikiwamo kuzaa watoto wengi na kushindwa kuwahudumia na kuwapa haki zao za msingi.

Katika hilo, kuna umuhimu wa kulingana na uwezo wa kumudu kuwahudumia ili wote wapate elimu bila kikwazo chochote, ambacho kinaweza kusababisha waishie madarasa ya chini au wasisome kabisa. Kwa sisi wakristo kuna maandiko katika Biblia yanayotuagiza kumshika sana elimu kwa kuwa ndiye uhai wetu. Hivyo kila mzazi kwa mzazi atambue kwamba elimu ni muhimu kwa mtoto wake.



**ZAINABU MSALAMA (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)**

MTU anapozaa ana haki ya kuitwa baba au mama, na pia anawajibika kuhakikisha watoto wake wanapata elimu.

Lakini inapotokea anashindwa kuwasomesha kwa makusudi, mzazi kama huyo achukuliwe hatua za kisheria kwasababu anachangia kukwamisha maendeleo ya baadaye ya mtoto wake.

Katika jamii yetu, wapo wazazi, ambao hawajui kabisa umuhimu wa elimu ingawa uwezo wa kiuchumi wanao, wapo wenye uwezo kiuchumi na wanajua umuhimu wa elimu, lakini pia hawataki tu kuwasomesha watoto wao.

Vilevile wapo wanaijua umuhimu wa elimu, lakini bahati mbaya hawakujaliwa kuwa na maisha bora, hivyo ni vyema kundi hili likasaidiwa.

Yaani wasio na uwezo kiuchumi wasaidiwe kusomeshewa watoto wao na hao wengine waelimishwe kutambua umuhimu wa elimu kwa watoto, kwa ajili ya maisha yao ya baadaye kwa elimu ni haki ya msingi ya kila mtoto.

Mzazi au wazazi wasiosomesha watoto wao wanaikwamisha serikali. watafakari na kisha wachukue hatua sahihi za kuhakikisha watoto wao wanapata elimu kadri inavyowezekana.

Wawajibike kuwapeleka watoto shule wapate elimu, ambayo itawawezesha kuendesha maisha yao vizuri na hata kuwasaidia wazazi wao waliochangia kuwafanya wawe na maisha bora.



**MAIKA MAPUNDA (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)**

SIDHANI kama bado kuna mzazi wa aina hiyo kipindi hiki ambacho elimu inatolewa bure. Huyo atakuwa miongoni mwa wale wasiojua maana ya elimu.

Mzazi wa aina hiyo anatakiwa kufuatiliwa na kujua kiundani matatizo yake ili ijulikane kwenye jamii inayomzunguka kama kweli alishindwa kumsomesha mtoto wake kwa kutokuwa na uwezo kifedha, lakini kama ni mzazi anayelewa na kusahau familia yake, basi ashurutishwe, na yule ambaye ni maskini, anasaidiwe kuhakikisha mtoto wake au watoto wanasoma, vinginevyo familia inaweza kuendelea kuwa maskini kwa kukosa elimu.

Ninajua kwamba nchi hii wapo watu ambao hawana uwezo kabisa, ndiyo maana serikali ikiweka elimu bure na inawezekana bado wapo ambao hawan uwezo hata wa kuwanunulia watoto wao vifaa vya shule, watu wa aina hiyo ni muhimu watambuliwe na kusaidia.

Lakini wale ambao kwa sababu wanazozijua wenyewe hawataki kusomesha watoto wao, hao siyo wa kuachwa, washughulikiwe ili washiriki kikamilifu katika vita ya kupambana na maadui watatu.

Watu wasiojua maana ya elimu, katika karne hii ya 21 wasaidiwe kutambua na kuithamini elimu, kwani ndio pekee inayoweza kumfanya mtu akawa na maendeleo.



HABARI MBEYA

# Waishukuru serikali ujenzi kituo cha afya

Na Nebart Msokwa, MBEYA

WANANCHI wa Kata ya Ikukwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, wameishukuru serikali kwa kuwajengea kituo cha afya, wakieleza kuwa kitawasaidia kuondokana na adha ya kutembea umbali mrefu kufuata huduma katika Mji wa Mbalizi.

Wananchi hao wamedai kuwa kabla ya kujengwa kwa kituo hicho, walikuwa wanalazimika kwenda katika Hospitali Teule ya wilaya hiyo iliyoko Ifisi, takriban kilomita 80 kutoka katika kata yao ama kwenda Hospitali ya Mwambani wilayani Songwe.

Mmoja wa wananchi hao, Jescar Shombe, alidai wanawake ndiyo waliokuwa wanapata shida zaidi kutokana na tatizo hilo, akieleza kuwa wajawazito walikuwa wanalazimika kusafiri kwa pikipiki, hivyo kuhatarisha maisha ya mama na mtoto.

Alisema baadhi yao walikuwa wanajifungulia njiani kutokana na miundombinu ya barabara kuwa mibovu, hasa kipindi cha mvua.

"Tunaishukuru serikali kwa kutusogezea hospitali hii, tulikuwa tunapata shida sana, hasa wanawake. Kwa sasa, tutakuwa tunajifungua hapahapa badala ya kusafiri kwenda Ifisi ambako gharama za usafiri ni kubwa," alisema.

Moses Kuyamba, mkazi wa kata hiyo, aliiomba serikali kuwasaidia kuboresha miundombinu ya barabara ili kuwarahisisha wananchi kukifikia kituo hicho na Hospitali ya Wilaya.

Alisema barabara nyingi za eneo hilo ni mbovu na baadhi hazipitiki kipindi cha mvua kutokana na madaraja yake kuwa mabovu.

Hivi karibuni, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, Mwalingo Kisemba, alisema kutokana na adha wanayopata wananchi hao, wameamua kujenga barabara ya kupitia Mlima Mbeya kwenda kutokea Mbeya mjini ambayo ni fupi kuliko waliyozoea.

Alisema barabara hiyo inajengwa na Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (Tarura) na kwamba ikikamilika, itasaidia kuwapunguzia gharama za usafiri.

# Jukwaa la alizeti laanzishwa

Na Nebart Msokwa, MBEYA

WADAU wa alizeti mkoani Mbeya wamezindua jukwaa maalum kwa lengo la kushughulikia matatizo yanayolikabili zao hilo.

Vilevile, katika kuunga mkono jitihada hizo, serikali imewaagiza wazalishaji wa mbegu, kuzalisha kwa wingi kuendana na mahitaji ya wakulima.

Jukwaa hilo liliundwa Julai mwaka huu chini ya ufadhili wa Shirika la Maendeleo la Uholanzi (SNV) kupitia mradi wake wa uboreshaji wa mifumo ya masoko katika maziwa na alizeti (Tam), likiwashirikisha wadau mbalimbali, wakiwamo wakulima. Akizungumza wakati wa uzinduzi wa jukwaa hilo mwishoni mwa wiki, Mshauri wa Masuala ya Sera wa Tam, Renatus Mbamilo, alisema waliamua kushirikiana na wadau wa zao hilo kuunda jukwaa baada ya kubaini matatizo yanayolikabili.

Alisema wanalenga kulifanya zao hilo kuwa la biashara badala ya watu kuendelea kulima kwa mazoea na kwamba wanatekeleza mradi huo chini ya ufadhili wa Shirika la Maendeleo la nchini Uingereza (UkAID).

"Lengo la jukwaa ni kuwaunganisha wadau ili wajadiliane matatizo yanayolikumba zao hili pamoja na kuyatafutia suluhu, kupitia jukwaa hili pia tutajadiliana sera mbalimbali za nchi na kurekebisha upungufu unaobainika," alisema.

Aliongeza kuwa Mkoa wa Mbeya ndiyo wa kwanza nchini kuzindua jukwaa la alizeti kwa maelezo, akieleza kuwa Mkoa wa Kilimanjaro ulikuwa wa kwanza kwa kuunda jukwaa la maziwa alilodai linafanya vizuri.

Mbamilo pia alisema mradi huo kwa mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini unatekelezwa katika mikoa minne ya Mbeya, Songwe, Rukwa na Katavi.

Aliwataja wadau wengine wanaohusika kwenye jukwaa hilo mbali na wakulima kuwa ni wasindikaji wa mafuta ya alizeti, wasafirishaji wa alizeti, wataalamu wa masuala ya biashara na wafanyabiashara wa zao hilo.

Mwenyekiti wa Kamati ya Uandaaji wa jukwaa hilo, Stanley Kibakaya, ambaye pia ni Ofisa Biashara kutoka Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, alisema alizeti ni miongoni mwa mazao yenye tija kubwa mkoani humo.

Alisema mafuta ya alizeti ni miongoni mwa bidhaa zenye soko kubwa katika mkoa huo na kwa taifa zima kutokana na maelezo ya wataalamu kuwa mafuta hayo ni salama zaidi kwa afya za watu kuliko aina zingine.

"Mafuta ya kupikia yanayozalishwa nchini kwa sasa ni asilimia 30 pekee na asilimia 70 tunaagiza kutoka nje ya nchi, sasa tunaamini jukwaa hili litasaidia kuongeza uzalishaji wa alizeti ili tuongeze kiwango cha uzalishaji wa mafuta na kuepuka uagizaji," alisema.

Akizindua jukwaa hilo, Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Paul Ntinika, alisema serikali ipo tayari kushirikiana na wadau hao kutatua vikwazo vinavyowakabili wadau wa zao hilo ili kuongeza tija.

Alisema serikali itasaidiana na wadau hao kuwatafutia wakulima maeneo ya kuuzia, kusimamia upatikanaji wa mbegu bora za alizeti na kuhakikisha kunakuwa na tozo sawa katika wilaya zote za mkoa huo.




Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, William Ntinika (wa pili kushoto), akimkabidhi Katibu Tawala Msaidizi Uchumi na Uzalishaji wa Mkoa wa Mbeya, Said Madito, kitabu cha mpango Mkakati wa Jukwaa la Alizeti la mkoa huo, wakati wa uzinduzi wa jukwaa hilo, jijini humo mwishoni mwa wiki. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Kituo alichochanga JPM chaanza kutoa huduma

Na Nebart Msokwa, RUNGWE

KITUO cha Afya cha Kata ya Isongole katika Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe mkoani Mbeya, kimefunguliwa na kuanza kutoa huduma.

Kituo hicho kimeanza kutoa huduma ikiwa ni miezi michache baada ya Rais John Magufuli kutoa Sh. milioni 30 ili kikamilike haraka na kuahidi kupeleka watumishi.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, alitembelea kituo hicho mwishoni mwa wiki ili kukagua maendeleo yake na alishuhudia kikiwa tayari kimeanza kutoa huduma.

Alisema kituo hicho kilichojengwa kwa nguvu za wananchi wa kata hiyo, ni miongoni mwa vichache vilivyojengwa kwa utaratibu huo, akieleza kuwa Rais asingepata nguvu ya kutoa kiasi hicho cha fedha ikiwa wananchi wangebaki nyuma.

Alisema baada ya kukabidhi fedha zilizotolewa na Rais, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Seleman Jafo, aliagiza kikamilishwe haraka ili kifunguliwe na wananchi hao waanze kupata huduma.

"Nimeridhishwa na utekelezaji wa maagizo yote yaliyokuwa yametolewa, kituo kiko vizuri na sisi kama serikali tunafurahi tunapoona wananchi wanabuni miradi, maana huu mradi ulianza na wananchi wenyewe," alisema.

Alimpongeza Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe na wasaidizi wake kwa kusimamia vizuri mradi huo, akieleza kuwa unaendana na gharama halisi ya fedha iliyotolewa.

Chalamila alisema Mkoa wa Mbeya ni miongoni mwa iliyo na vituo vya afya vingi nchini, akibainisha kuwa tangu serikali ya awamu ya tano iingie madarakani Novemba 5, 2015, mkoa huo umefanikiwa kujenga vituo vipya zaidi ya 10.

Mkurugenzi wa wilaya ya hiyo, Loema Peter, alisema mpaka sasa, kituo hicho kimejengwa kwa zaidi ya Sh. milioni 170 zilizochangwa na wananchi, halmashauri na Rais Magufuli.


Alisema halmashauri yake iliwaunga mkono wananchi hao kwa kuchangia Sh. milioni 20 zilitokana na mapato ya ndani ya halmashauri.

"Tunaendelea na usimamizi wa vituo vyote vinavyojengwa ndani ya wilaya yetu, hiki ni kituo cha tatu maana awali tulikuwa navyo viwili, yaani cha Ikuti na Masukulu, lakini kwa nguvu za wananchi tumepata hiki," alisema.

Diwani wa Kata ya Isongole, Laurence Mtawango, alimshukuru Rais Magufuli kwa kuwachangia fedha zilizosaidia kumalizia ujenzi wa kituo chao.

Alisema wananchi wa kata hiyo walihamasika baada ya kuona wanapata shida ya kutembea umbali mrefu kufuata huduma katika miji ya Tukuyu na Mbeya.

Aliwaomba wadau mbalimbali wa maendeleo nchini kuendelea kujitolea kuchangia miradi ya maendeleo inayoibuliwa na wananchi wa kata hiyo ili kuwatia moyo.





# Ndugai ashangaa wabunge upinzani

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

SPIKA wa Bunge, Job Ndugai, amesema wabunge wa upinzani wanaopinga bajeti ya serikali ni 'upuuzi' kwa sababu katika bajeti hiyo mishahara yao imo, ikiwamo ya watendaji walio katika majimbo wanayo yaongoza.

Aidha, aliwataka wabunge wa Bunge la Vijana ambao wako upande wa upinzani kutoiga kila kitu, badala yake wachuje vitu vinavyopaswa kupingwa.

Spika Ndugai aliyasema hayo wakati akifunga Bunge la Sita la Vijana liliofanyika jijini hapa kwa takribani wiki moja kwa lengo la vijana wa vyuo vya elimu ya juu kujifunza shughuli zinazoendeshwa bungeni.

Akizungumza na Bunge hilo, alisema ukiwa mbunge wa upande wa upinzani sio kila kitu kinachofanywa au kusemwa na serikali unakipinga hata kama kuna manufaa na maslahi kwa jamii inayokuzunguka unapaswa kuangalia kipi hakifai na kipi kinafaa kukataliwa.

"Wakati wa kupitisha bajeti ya serikali au kuwasilisha hoja za msingi bungeni unakuta hoja ni maana, lakini mpinzani anapinga eti kwa vile anatokea upinzani," alisema.

"Naomba niwaambie wanangu maana hapa kuna upinzani na wabunge wa chama tawala... endapo siku moja mtapata nafasi hizo mnapaswa kuchuja vitu vya kupinga," alisema Ndugai.

Ndugai alisema mapendekezo ya Bunge la Vijana atayafanyia kazi na kuona jinsi gani ya kuwaongezea muda ili wapate kujifunza zaidi.

Moja ya mapendekezo waliotoa Bunge la vijana ni kuongezewa muda wa Bunge ili wapate kujifunza zaidi mambo mbalimbali yanayofanyika.

Aidha, Ndugai aliwashauri vijana hao wabunge wapangie Bunge lao ratiba iende sambamba na Bunge la Jamuhuri ya Muungano ili wajifunze kazi zinazofanywa na mhimili huo.

"Siku hizi bungeni hatutumii makaratasi ni mwendo wa mtandao, nyie ni wasomi Bunge lijalo mje na vitendea kazi," alisema Ndugai.

Naye Spika wa Bunge la Vijana, Ramadhan Singa, alisema mafunzo ya shughuli za Bunge yanawapa uwelewa mkubwa juu ya muhimili huo wa serikali unavyofanya kazi.

**"Naomba niwaambie wanangu maana hapa kuna upinzani na wabunge wa chama tawala... endapo siku moja mtapata nafasi hizo mnapaswa kuchuja vitu vya kupinga," alisema Ndugai.**

# CBE yaomba kibali ajira za wahadhiri

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

CHUO cha Elimu ya Biashara nchini (CBE) tawi la Dodoma, kimeiomba serikali kuwapa kibali cha kuajiri wahadhiri ili kukabiliana na wingi wa wanachuo ikiwamo ongezeko la programu.

Ombi hilo lilitolewa na Makamu Mkuu wa chuo hiko, Prof. Emanuel Mjema, katika mahafali ya 54 ya chuo hicho yaliyofanyika jijini hapa kwa wahitimu 904 kutunukiwa shahada mbalimbali.

Prof. Mjema alisema wanaiomba serikali itoe kipaumbele katika nafasi za kuajiri wahadhiri katika chuo hicho na kwamba kila siku idadi ya wanafunzi inaongezeka tofauti na ilivyo kwa idadi ya wahadhiri.

"Tunaomba serikali iliangalie kwa karibu suala la kuongeza wahadhiri chuo chetu kinakua kila uchao na wanafunzi wanaongezeka, hivyo tunahitaji wahadhiri nao waongezwe ili kupunguza uhaba uliopo," alisema Prof. Mjema.

Alisema lengo ni kuona idadi ya wahadhiri inaongezeka chuoni hapo, jambo ambalo litaleta ufanisi zaidi katika utendaji wa kazi.

Akizungumza suala la upanuzi wa chuo, alisema wanakabiliwa na changamoto ya hosteli za wanafunzi ambapo hivi sasa wana hosteli zenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 260, ambapo wa kike ni 164 na wa kiume 96, huku wengine wakiishi nje ya chuo.

Alisema ili kukabilina na changamoto hiyo, wanahitaji kuanza ujenzi katika maeneo ambayo wanamiliki ardhi ili kuhakikisha wanafunzi wanaosoma katika chuo hicho wanaishi katika mazingira mazuri ambayo yatawawezesha kupata elimu bora.

Naye Mwenyekiti wa Bodi ya CBE, Prof. George Shumbusho, alisema serikali iendelee kuwekeza katika chuo hiko kwa sababu kinatoa wataalamu ambao ni muhimu katika sekta ya biashara ambayo ni muhimu nchini.

Alisema bodi imekuwa ikikutana na changamoto nyingi ambazo zinahitaji utatuzi wa haraka ili chuo kizidi kupiga hatua moja mbele ikiwamo kuzalisha wataalamu wenye weledi ambao watasaidia kutatua changamoto zilizopo katika sekta ya viwanda.

Aliishukuru serikali kutokana na jitihada inazofanya katika sekta ya elimu na kuiomba iendelee kutupia macho elimu ya juu, ambayo inatengeneza wataalamu kwa ajili ya taifa pale wanapohitimu masomo.

"Elimu ya juu ina umuhimu sana kwa sababu wahitimu huenda kujiunga katika maeneo mbalimbali ya kazi kwa ajili ya ujenzi wa taifa," alisema Prof. Shumbusho.




Rais John Magufuli, akipokea gawio la Sh. bilioni 1.15 kwa serikali kutoka kwa Meneja Uhusiano wa Kampuni ya Kuhifadhi Mafuta TIPER, Emmanuel Kondi, na Mjumbe wa Bodi ya kampuni hiyo, Jamuhuri Ngilime (kushoto) ikiwa ni sehemu ya faida ya kampuni hiyo kwa mwaka 2018, wakati wa makabidhiano jijini Dodoma juzi. Katikati ni Spika wa Bunge, Job Ndugai. **MPIGAPICHA WETU**

# Pinda ashauri vyuo mifumo kidigitali

**Na Paul Mabeja, DODOMA**

WAZIRI Mkuu mstaafu, Mizengo Pinda, amevitaka vyuo vikuu nchini kutumia mifumo ya kidijitali katika kurahisisha ufundishaji, huku akitahadharisha matumizi hayo yawe katika malengo yaliyokusudiwa, vinginevyo inaweza kuwa hatari kwao.

Pinda aliyasema hayo jijini hapa kwenye kongamano la wanataaluma wa Chuo Kikuu cha St. John's likiwa na mada kuu ya 'udijirishaji kwa elimu ya juu kwa vyuo binafsi kiungo bora kwa uchumi wa viwanda'.

"Lazima kuwe na hekima katika kutumia teknolojia maana ukiitumia vibaya inaweza kuwaumiza wahusika pamoja na watu wengine, lakini ukiitumia vyema inakusaidia kusonga mbele katika masuala mbalimbali ya kimaendeleo," alisema Pinda na kuongeza:

"Hivyo hata katika kuelekea uchumi wa kati wa viwanda, lazima kila mtu atumie vizuri teklonojia ili tufikie malengo yale ambayo tumeyakusudia," alisema.

Alisema matumizi ya teknolojia yanatakiwa kutumika katika kuboresha ufundishaji pamoja kusaidia kuimarisha dhana ya uchumi wa viwanda kama anavyosisitiza Rais John Magufuli kwamba Tanzania ni ya viwanda.

"Viwanda bila teknolojia huwezi kusonga mbele na unapozungumzia teknolojia maana yake ni pamoja na miundombinu mbalimbali ukiwamo umeme, mawasiliano na vitu vingine ambavyo vyote vitaleta uchumi wa kati kwa wananchi," alisema.

Naye Mwenyekiti wa kongamamo hilo, Askofu Philipo Baji, alisema chuo hicho kina lengo la kuhakikisha wanatumia teknolojia.

Alisema chuo kinalenga kuachana na mtindo wa zamani wa kutumia makaratasi, kwa kuanza kutumia teknolojia kuwafundisha wananchuo ili kurahisisha ufanyaji kazi wao pamoja na kuwafikia wengi kwa urahisi.

Hata hivyo, aliwataka wanachuo kujifunza zaidi masuala hayo kwani ulimwengu wa sasa ni wa sayansi na teknolojia pamoja na kutumia maarifa waliyoyapata kulisaidia Taifa kusonga mbele.

Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha St. John's, Dk. Alfred Sebahene, alisema zipo changamoto mbalimbali ambazo wanatakiwa kuzitatua zinazowakabili katika kuingia kwenye mfumo wa kidigitali.

Alisema miongoni mwa mambo yanatakiwa kuyaangalia kwa ukaribu ni umuhimu wa kuboresha vifaa na kuwa na ujuzi wa teknolojia, sera, mikakati ya kulifanya suala la kidigitali katika kutoa elimu linakuwa na mafanikio, pamoja na changamoto ya lugha.



**HABARI ZANZIBAR**

# Watanzania waelimishwa kuchangamkia fursa EAC

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema serikali imeandaa mkakati wa kutoa elimu kwa umma ili kuhakikisha wajasiriamali wanachangamkia fursa za kibiashara zitokanazo na Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC).

Aliyasema hayo jana wakati akifunga maonyesho ya maadhimisho ya miaka 20 tangu kuanzishwa kwa EAC katika viwanja vya Fumba, Zanzibar.

Majaliwa alisema mkakati huo unahusisha utafiti wa uelewa kwa Watanzania kuhusu EAC na matokeo ya utafiti huo yatatumika katika kutoa elimu kwa umma kutokana na mahitaji.

Alisema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) imeanzisha mfuko wa uwezeshaji wananchi kiuchumi kwa lengo la kutoa mitaji na huduma za kifedha zenye masharti nafuu kwa wananchi wa Unguja na Pemba.

Kwa mujibu wa Waziri Mkuu, mfuko huo unalenga wananchi wenye kipato kidogo kuzalisha mali kwa kujiajiri na kupunguza umaskini na hadi Juni, mwaka huu, mikopo yenye thamani ya Sh. bilioni 3.5 imetolewa na kuzifikia shehia 346.

Waziri Mkuu aliwataka wajasiriamali kujitathmini ili kuona wametimiza malengo ya kuanzishwa kwa EAC kwa kuboresha uzalishaji wa bidhaa zao ili zishindane katika soko la ndani na nje ya Tanzania.

Aliwataka wajasiriamali kutumia fursa za maonyesho kama hayo kwa lengo la kutangaza bidhaa zao na kuhamasisha wananchi kutumia bidhaa zinazozalishwa nyumbani.

Pia aliishauri Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kupitia Baraza la Wawakilishi kutunga sheria ambayo itatoa mwongozo kwa kila halmashauri kutenga fedha kwa ajili ya wajasiriamali ili kujiendeleza kwa kuinua vipato vyao.

Naye Waziri wa Biashara na Viwanda Zanzibar, Balozi Amina Salum Ali, alisema dhamira ya maonyesho hayo ni kuwapatia fursa wajasiriamali kutangaza biashara zao ndani na nje ya nchi na kuonyesha ubora na kubadilishana teknolojia na kwenda na wakati.

Aidha, aliwataka wananchi kutumia bidhaa ambazo zinazalishwa na wajasiriamali wa ndani ya nchi kwa kukuza uchumi wa nchi.

Mwenyekiti wa Wajasiriamali wa EAC, Josephat Rweyemamu, alisema pamoja na serikali kutatua changamoto mbalimbali, bado kuna vikwazo ikiwamo mikopo inayotolewa na manispaa kutotoka kwa wakati, benki zisizo rafiki kwa wajasiriamali na masharti magumu ya mikopo.



Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar, Balozi Seif Ali Idd, akipata maelezo kutoka kwa wajasiriamali alipotembelea mabanda mbalimbali kwenye maonyesho ya maadhimisho ya Miaka 20 ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, huko Fumba, nje ya mji wa Zanzibar wikiendi.
**PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Mahakama ya Rufani yaanza kikao Z'bar

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

KIKAO cha Mahakama ya Rufani kilianza rasmi jana Vuga mjini Zanzibar kwa ajili ya kusikiliza kesi mbalimbali za madai na jinai zilizowasilishwa mahakamani hapo.

Naibu Mrajisi wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Amir Khamis, aliwaambia waandishi wa habari jana kuwa mahakama hiyo itasikiliza mashauri 29 yakiwamo 11 ya madai 11 na matatu ya jinai.

Alisema mashauri hayo yatasikilizwa na majaji watatu wa Mahakama ya Rufani Tanzania wakiongozwa na mwenyekiti wa jopo hilo, Augustine Mwarija. Wengine ni Gerald Ndika na Rehema Kerefu.

Alieleza mashauri mengine ambayo yatasikilizwa ni maombi ya madai ya malalamiko mbalimbali kutoka kwa wahusika.

"Mahakama hii itasikiliza mashauri ya makosa ya jinai na kutoa uamuzi unaostahili ili kuhakikisha haki inatendeka," alisema.

Alisema katika mashauri hayo, inaonyesha maombi ya madai yako mengi ambayo wahusika wake walikata rufani baada ya kutoridhishwa na uamuzi wa Mahakama Kuu.

Kikao hicho cha mahakama ya rufani, kwa mujibu wa Naibu Msajili, kinaratajiwa kumalizika Desemba 11, mwaka huu.

**"Mahakama hii itasikiliza mashauri ya makosa ya jinai na kutoa uamuzi unaostahili ili kuhakikisha haki inatendeka," alisema.**

# Maswali 96 kuulizwa Baraza Wawakilishi

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

MKUTANO wa 16 wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar unatarajiwa kuanza kesho na maswali 96 yataulizwa na kujibiwa.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Katibu wa Baraza la Wawakilishi, Raya Mselem, alisema katika kikao hicho pia miswada ya sheria iliyowasillishwa na kusomwa kwa mara ya kwanza katika mkutano uliopita, itasomwa kwa mara ya pili na kujadiliwa.

Raya aliitaja miswada hiyo kuwa ni Muswada wa Sheria ya Kuanzishwa Wakala wa Serikali Mtandao, kazi zake na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Muswada mwingine, kwa mujibu wa katibu huyo, ni wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Kuanzisha Ofisi ya Mufti Na. 9 ya mwaka 2001.

"Pia katika kikao hicho kutawasilishwa Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali na kuweka masharti bora ndani yake," alisema.

Alisema muswada mwingine utakaowasilishwa ni wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Usafiri Barabarani Na. 7 ya mwaka 2003 na Muswada wa Sheria wa Kuanzisha Wakala wa Barabara Zanzibar na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Katibu huyo alisema katika kikao hicho, pia wanatarajia kupokea muswada kwa hati ya dharura wa Kuanzisha Chuo cha Mafunzo ya Sheria kwa Vitendo (Law School).

# Watumiaji mashine wapigwa msasa

**Na Enock Charles**

MANTRAC Tanzania imewazawadia wateja wake wanaotumia mashine za aina ya CAT kwa kuwapa mafunzo ya kidijitali ili kuwaongezea ujuzi na maarifa ya namna ya kutumia mashine hizo.

Akizungumza wakati wa mafunzo hayo, Mkurugenzi Mtendaji wa Mantrac Tanzania, Medhat Adly, alisema mafunzo hayo yaliandaliwa ili kuwawezesha wateja wao wafanye biashara kwa ufanisi zaidi katika maeneo yao ya kazi, huku pia kupunguza ajali na kuhakikisha wafanyakazi wanakuwa salama muda wote.

Alisema mwaka huu Mantrac imeboresha mikataba ya thamani kwa wateja ili wateja wao waweze kuchagua kile wanachokihitaji.

Mafunzo hayo yalihudhuriwa na mainjinia, mameneja miradi na mafundi ambao kwa mujibu wa Meneja Bidhaa, Mohamed El Demerdash, wateja hao pia walipata fursa ya kukutana na kubadilishana mawazo na wataalamu wa kidijitali wa caterpillar na kujifunza kuhusu caterpillar na uwezo wake katika utendaji wa kila siku.

Alisema pamoja na mambo mengine, mafunzo hayo yatasaidia kuongeza ufanisi, kupunguza gharama za uendeshaji, kupunguza ajali na kuhakikisha mashine zinakuwa katika hali ya ubora muda wote.

Mengine ni kuhakikisha usalama, ununuzi wa vipuri kwa wakati, uzingatiaji wa matengenezo na kuwa na uwezo wa kuwasiliana na Mantrac haraka kwa kubonyeza tu sehemu.

Moja ya bidhaa zilizooneshwa katika mafunzo hayo ni 'Vision Link' ambayo ni moja ya vifa vya kidijitali vyenye umuhimu mkubwa katika usimamizi wa mashine.

Mashine hizo pia zina teknolojia kama ya simu ambayo inawasaidia wateja katika usimamizi wa mashine zao na kuwasiliana na wauzaji wa caterpillar kote duniani, huku pia teknolojia hii ikiwa na uwezo wa kuwakumbusha wateja uhusu matengenezo yanayotakiwa kwa muda ambao mashine haifanyi kazi ili isiathiri uzalishaji.

Mmoja wa waliohudhuria mafunzo hayo, Geoffrey Mtimbange kutoka Twiga Cement, alisema teknolojia hiyo mpya itawasaidia kupunguza gharama za uendeshaji na kujua maeneo ya kuboresha.

Naye Pradeep Sinha, kutoka Mtibwa Sugar, alisema wamekuwa wakitumia mashine za Mantrac kwa muda sasa na kupata matokeo mazuri na hata sasa hivi wana mradi unaoendelea katika kiwanda chao ambapo wanatumia mashine za Caterpillar.

# Umeme wakwaza wakulima wa alizeti

**Na Rahma Suleiman, aliyekuwa DODOMA**

LICHA ya wakazi wa Kijiji cha Chang'ombe wilayani Kiteto Mkoa wa Manyara ni wakulima wa kilimo cha alizeti, lakini wamekua wakinunua mafuta ya alizeti kutoka maeneo mengine.

Wakazi wa kijiji hicho wanalima kilimo hicho, lakini wanashindwa kupata mafuta kutokana na kijijini hapo kutokuwa na mashine za kuchakata alizeti.

Wakizungumza na timu ya waandishi wa habari waliopatiwa mafunzo ya matumizi ya nishati jadidifu, wananchi hao walisema kuwa kutokuwa na kiwanda cha uchakatishaji wa alizeti kunatokana na gharama kubwa za umeme wa jua wanaotumia kijijini hapo.

Jane Chamaisi ni miongoni mwa wakulima wa alizeti wa kijiji hicho, alisema huzalisha zaidi ya gunia nane kwa mwaka za alizeti, lakini bado mafuta ya kula anaagiza kutoka mjini.

Jane ni miongoni mwa wakazi 5,000 wa kijiji hicho ambapo shughuli zao kuu za kiuchumi kijiji hapo ni kilimo na ufugaji,ambapo alieleza kuwa kijiji hicho wakazi wake wanatumia umeme wa jua unaozalishwa na kusambazwa na kampuni ya Power Gen.

"Huu umeme umekua na gharama kubwa na zaidi wananchi wa kijiji hiki wamekua wakiutumia kwa ajili ya taa tu kuweza kupata mwanga," alisema.

Jane aliiomba serikali kuwapelekea umeme wa Tanesco ambao wanaamini kuwa hauna gharama kubwa ukilinganishwa na umeme wa jua wanaotumia.

Kijiji hicho chenye wakazi 5,000, ni nyumba 200 pekee zenye nishati ya umeme wa jua yakiwamo makazi ya watu, taasisi na maduka ambapo umeme huo bado hautumiki sana katika shughuli za uzalishaji mali kutokana na gharama kubwa za kuulipia.

Boniface Chamaisi, mkazi wa kijiji hicho ambaye anamaliki mashine ya kukoboa na kusaga mahindi ambayo inatumia mafuta ya diseli, alisema ana uwezo wa kusimika mtambo wa kuchakata alizeti ikiwa gharama za umeme zingekuwa nafuu.

"Tunashindwa kutumia umeme wa jua kwa shughuli za uzalishaji mali kwa sababu gharama zake ni kubwa, hivyo tunaiomba serikali ituletee umeme wa Tanesco ili tuweze kuendelea na shughuli za uzalishaji mali na kujikomboa kiuchumi," alisema.

Naye wakala wa usambazaji umeme wa jua kijijini hapo, Mologo Maungo, alikiri kuwa umeme huo unagharama kubwa na wananchi wa kijiji wamekuwa wakiulalamikia na baadhi yao kushindwa kuitumia kwa shughuli za uzalishaji.

Alisema Watt moja ya umeme huo inauzwa kwa shilingi tatu kwa saa moja nyakati za mchana na shilingi sita kwa saa moja nyakati za usiku.

Mtendaji Kata ya Dongo, Izac Devid Andrew, aliishauri kampuni ya Power Gen inayotoa huduma ya umeme wa jua katika kata hiyo ambayo inavijiji vitatu ikiwamo kijiji cha Chang'ombe, ipunguze gharama za umeme, na kuiomba serikali iwafikishie umeme wa gridi kupitia wakala wa umeme vijijini REA.

Naye mhandisi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji (EWURA), Victor Labaa, alieleza mamlaka inaandaa mfumo ambao utatumika kupanga bei ya umeme kwa wazalishaji wadogo wa umeme jadidifu ili kupunguza malalamiko ya wananchi.



Meneja Bidhaa wa Mantrac Tanzania, Mohamed El Demerdash, akitoa maelezo kwa wateja waliohudhuria mafunzo ya siku moja ya kidijitali ili kuwaongezea ujuzi na maarifa ya namna ya kutumia mashine za caterpillar. **MPIGAPICHA WETU**

# Matatani tuhuma za kunajisi mtoto

**Na Mwandishi Wetu, PEMBA**

KIJANA Andrew Joseph Frank (20) mkaazi wa Kiungoni, anashikiliwa na Jeshi la Polisi Mkoa wa Kaskazini Pemba kwa tuhuma za kunajisi mtoto wa kike (4) huko Kiungoni Wilaya ya Wete Pemba.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa huo, Mohamed Shehan Mohamed alisema kuwa tukio hilo lilitokea Novemba 11, mwaka huu saa 11:00 jioni.

Alisema kuwa mtuhumiwa huyo alimchukua mtoto huyo na kwenda nae kwenye mabwawa ya chumvi yaliyopo Kiungoni na kumnajisi huko huko.

"Mtuhumiwa huyu alimchukua mtoto huyu na kwenda kumnajisi, kwa kweli alimwathiri sana kwa sababu bado ni mdogo, jambo hilo limesababisha mtoto huyo kupata maumivu makali katika sehemu zake za siri," alieleza kamanda huyo.

Alisema kuwa upelelezi wa kesi hiyo umeshakamilika, na kuwa mtuhumiwa atafikishwa mahakamani taratibu zitakapokamilika.

Katika tukio lingine, kamanda huyo alisema kuwa lilitokea Makangale Wilaya ya Micheweni Pemba, Juma M. Juma mwenye umri wa miaka 25 anatuhumiwa kumbaka mtoto wa miaka 17 ambaye ana ulemavu wa akili na miguu.

"Mtoto huyo alikwenda kumchukua na kwenda kumbaka katika shamba la mipira lililopo Makangale Wilaya ya Micheweni Pemba," alisema.

Kamanda alieleza kuwa mtuhumiwa huyo amekamatwa na Jeshi la Polisi linaendelea kumuhoji, na kuwa watampeleka mahakamani baada ya upelelezi kukamilika.

Aliwataka wananchi kuwaripoti wahalifu wa matendo hayo, na kutoa ushahidi wanapohitajika kwenda kutoa ushahidi.

"Hakuna kesi za udhalilishaji ambazo tunazifuta hapa Polisi, tunafanya upelelezi wa kutosha na ushahidi unapokuwa madhubuti ndipo tunaifikisha mahakamani," alisema kamanda huyo.

Kubaka ni kosa kwa mujibu wa sheria kifungu cha 113 (1) (a) cha Sheria ya Adhabu, Sheria namba 6 ya mwaka 2018 Sheria ya Zanzibar.

## HABARI KIMATAIFA

# Waliokufa mafuriko Kenya wafikia 56

**NAIROBI,** Kenya

IDADI ya watu waliofariki katika mkasa wa maporomoko ya ardhi yaliyosababishwa na mvua kubwa inayonyesha katika eneo la Pokot Magharibi mwa Kenya imeongezeka na kufikia 56, amesema ofisa wa serikali katika eneo hilo.

Idadi ya miili ambayo haijapatikana ni 22, baada ya mkasa huo kuyakumba maeneo ya Parua, Nyarkulian and Muino, kwa mujibu wa Gavana wa jimbo hilo, Prof. John Lonyangapuo.

Prof. Lonyangapuo alisema jana kuwa shughuli ya kusaka na kuokoa miili inaendelea. Juhudi za kuipata na kuivuta miili kutoka kwenye matope zimekwamishwa na usafiri, baada ya barabara zinazokwenda katika maeneo hayo kuharibika.

Alisema nyumba 22,000 zimeharibiwa na maporomoko ya ardhi, na kati ya watu 80,000 na 120,000 wamekosa kazi.

**Kijiji kizima kimesombwa na maji nchi Sudan Kusini, huku matukio ya mafuriko yakiripotiwa Tanzania, Ethiopia na Somalia.**

Waziri wa Mambo ya Ndani, Fred Matiang'i. Katika ujumbe wake wa Twitter, ameeleza kuwa amelazimika kutua kwa ndege katika uwanja wa ndege wa Kimataifa wa Eldoret alipokuwa akielekea katika maeneo ya mkasa wa mafuriko kutokana na hali mbaya ya hewa alipokuwa akijaribu kuelekea huko kuangalia shughuli za uokoaji:

Maofisa wanasema kuwa barabara zinazounganisha vijiji zimeharibika kutokana na mafuriko katika barabara na takriban daraja moja limeripotiwa kusombwa na maji.

Prof. Lonyangapuo ametoa wito wa dharura kwa Waziri Matiang'i akimuomba usaidizi wa helikopta kwa ajili za uokoaji katika maeneo yaliyoathiriwa na mafuriko..

Jumamosi rais wa Kenya, Uhuru Kenyatta, alituma salamu za rambirambi kwa familia zilizoathiriwa na mkasa huo.

"Nimepokea kwa masikitiko makubwa taarifa ya mkasa huu, kwa wale waliojeruhiwa na ambao wanaendelea kupokea matibabu katika hospitali mbali mbali, nawaombea uponyaji wa haraka," alisema Rais Kenyatta.

Aidha, Rais aliagiza ndege ya kijeshi kupelekwa katika eneo hilo kusaidia katika shughuli ya uokozi na kutoa wito kwa mamlaka katika eneo hilo kushirikiana na asasi za usalama kufanikisha oparesheni ya uokozi.

Chifu wa Nyarkulia, Joel Bulal, amenukuliwa na vyombo vya habari akisema shughuli za uokozi zinaendelea, kwa kuwatafuta ambao hawajulikani waliko.

Kamishena wa jimbo hilo, Apollo Okelo, alisema watu wengi huenda wamekwama chini ya matope na kuongeza kuwa shughuli ya kuwaokoa zinaathiriwa na hali mbaya ya hewa. Kumeshuhudiwa mvua nyingi katika eneo la Afrika Mashariki na upembe wa Afrika kwa wiki kadhaa sasa.

Kijiji kizima kimesombwa na maji nchi Sudan Kusini, huku matukio ya mafuriko yakiripotiwa Tanzania, Ethiopia na Somalia.

Wanasayansi wanasema hali mbaya ya hewa inatarajiwa kukumba baadhi ya nchi katika kanda hiyo kwa sababu viwango vya joto katika Bahari ya Hindi vinatarajiwa kupanda kupita kiasi cha kawaida, hali ambayo huenda ikasababisha mvua kubwa. **BBC**



Juhudi za kuipata na kuivuta miili kutoka kwenye matope yaliyosababishwa na mafuriko nchini Kenya, zimekwamishwa na usafiri baada ya barabara zinazokwenda katika maeneo hayo kuharibika. **PICHA: BBC**

## Bloomberg ajitosa urais wa Marekani

**NEW YORK,** Marekani

MFANYABIASHARA tajiri na meya wa zamani wa mji wa New York, Michael Bloomberg, amezindua rasmi kampeni yake ya kuwania kuteuliwa kuwa mgombea wa urais wa Marekani kwa tiketi ya chama cha Democratic.

Akihitimisha wiki kadhaa za uvumi, mwanachama huyo wa zamani wa chama cha Republican mwenye umri wa miaka 77, alitangaza kuwania urais kupitia taarifa iliyochapishwa kwenye tovuti yake akijisifu kuwa kwenye nafasi madhubuti ya kumshinda Rais Donald Trump.

Bloomberg amesema, Marekani haiwezi kuvumilia miaka minne zaidi ya utawala wa Rais Trump alioutaja kujaa vitendo vya kijinga na vilivyokosa maadili.

Kujiunga kwa Bloomberg kwenye kinyang'anyiro hicho kunatokea wiki kumi kabla ya kufanyika kura za mchujo, hatua inayoashiria wasiwasi uliopo ndani ya chama cha Democratic juu ya wagombea waliopo hivi sasa. **DW**

# Rwanda yazindua magari ya umeme

**KIGALI,** Rwanda

RWANDA ikishirikiana na Kampuni ya Volkswagen na Siemens, imezindua magari ya kwanza ya umeme nchini humo yatakayokuwa rafiki kwa mazingira.

Mradi huo ulioanza na magari 50 ambayo yametengenezwa kwa ajili ya majaribio yatakuwa yakitumiwa kama magari ya uchukuzi wa abiria jijini Kigali na kwingineko nchini.

Mkurugenzi Mkuu wa Volkswagen Group ya Afrika Kusini, Thomas Schäfer, amebainisha kuwa magari haya bado yapo katika majaribio na kwamba yametengenezwa 40 aina ya e.Golf. na kwamba malengo kwanza si kuuzwa na ni ghali, ingawa bei bado kutangazwa.

"Magari haya hayana mpango kuuzwa kwa wateja kwa sasa. Tunalenga kwanza kuyafanyia majaribio na kujua yanafanya kazi vipi na ndipo tutakapowajulisha iwapo zitauzwa au la. Magari haya ni ghali ikilinganishwa na yale ya kawaida, kutokana na betri yake kwani betri peke yake ina gharimu kiasi cha dola 8000 za Kimarekani, lakini umeme ukilinganishwa na mafuta ni bei nafuu," alisema na kuongeza:

Lakini iwapo serikali ikiwasaidia kwa kuweka sera mfano, kwa kupata faida nafuu, yamkini hali inaweza kuwa nzuri zaidi. Angalia China, serikali iliazimia kwamba asilimia magari 25 ya magari yanayouzwa yawe yanayotumia umeme."

Kampuni imeeleza kuwa inalenga kupanua wigo wa kazi zake katika mataifa mengi ya Afrika. Baada ya Rwanda, Ghana ndiyo inatarajia kufuata na hatimaye kwingineko.

Wakati mataifa ya Ulaya yanalenga kufikia mwaka 2030 kuwa yameshaachana na magari yanayotumia mafuta, Afrika ndiyo imeanza safari ambayo hatima yake haijawa wazi ila waliozungumza na BBC wameelezea kuwa hatimaye wao pia watafika. **BBC**

## Uchaguzi Hong Kong wakamilika

**HONG KONG,** China

UCHAGUZI wa mabaraza ya wilaya kwenye mji wa Hong Kong ulikamilika jana huku kiongozi wake Carrie Lam akikiri kuwa ushindi wa kishindo kwa makundi yanayopigania demokrasia umeonyesha jinsi raia wasivyoridhishwa na utawala wa mji huo.

Lam amesema kwenye taarifa aliyoitoa jana, kwamba uchaguzi huo umeakisi manung'uniko ya umma juu ya hali iliyopo sasa mjini Hong Kong pamoja na matatizo ya msingi ndani ya jamii. Amesema serikali yake itaheshimu na kufanyia kazi sauti ya watu wa Hong Kong katika uchaguzi uliofanyika jana, ambao umeshuhudia vyama vinavyounga mkono demokrasia vikishinda wingi wa viti kwenye mabaraza yote 18 ya wilaya.

Ingawa mabaraza ya wilaya yana wajibu zaidi wa kushughulikia masuala ya jamii, huwakilishwa pia katika kundi la wajumbe 1,200 ambao watamchagua kiongozi mpya wa Hong Kong mwaka 2022. **DW**



Mkuu wa Wilaya ya Mkalama, mkoani Singida, Mhandisi Jackson Masaka, akikagua gwaride la vijana 119 wa Kata ya Ibaga, wilayani humo, waliohitimu mafunzo ya jeshi la akiba juzi. **PICHA: ELISANTE JOHN**

# Taasisi zatii agizo la Magufuli

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SIKU moja baada ya Rais John Magufuli kutoa siku 60 kwa taasisi, kampuni na mashirika ya umma kutoa gawio, taasisi nne zimetekeleza agizo hilo kwa kutoa Sh. bilioni 2.75.

Taasisi hizo ni Self Microfinance ambayo imetoa Sh. milioni 200, Shirika la Posta (TPC) Sh. mil 350, Shirika la Reli (TRC) Sh. bilioni moja na Kituo cha Uwekezaji (TIC) Sh. bilioni 1.2.

Baada ya kutoa gawio hilo jana jijini Dodoma, Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, alisema hatakuwa na huruma na taasisi, kampuni au shirika la umma litakaloshindwa kutekeleza agizo hilo la Rais.

"Kama mnakumbuka jana (juzi), Rais alinipa kazi ya kuhakikisha taasisi hizo zinatoa gawio, kinyume chake mwenyekiti wa bodi, wajumbe wake na wakuu wa taasisi wajue wamejitoa, na alisema damu yao iwe juu ya wizara husika.

"Nitahakikisha nasimamia maagizo ya Rais, kwa atakayekaidi, nitashusha rungu bila huruma wala woga na bila kupepesa macho kwa yoyote yule," Dk. Mpango alisema.

Aliongeza kuwa zinazokusanywa si za Rais Magufuli wala Dk. Mpango, bali ni fedha za wananchi ambazo zimewekezwa huko, na kutoa gawio ni ushahidi kuwa wahusika wanazifanyia kazi.

Dk. Mpango aliwataka wenyeviti wa bodi na wakuu wa taasisi ambazo bado hazijatoa gawio, kutumia siku 59 zilizobaki kufanya hivyo ili kukwepa mkono wake.

Alisema ni vema kila taasisi, kampuni na shirika kufanya hivyo ili kujiweka salama katika utendaji wao wa kila siku.

Msajili wa Hazina, Athumani Mbuttuka, alisema kuwa baada ya kupewa agizo hilo na Rais, siku hiyo hiyo aliziandikia taasisi, mashirika na kampuni ambazo hazikuwa zimetoa gawio, kuhakikisha zinatekeleza agizo hilo.

Alibainisha kuwa taasisi nne zilizojitokeza jana, zilifanya idadi ya zilizotoa gawio kuwa 83 kati ya 266 zilizopo.

Mbali na taasisi nne zilizotoa gawio jana, taasisi zingine zilizotoa ni pamoja na Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari (TPA), Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano (TCRA), Shirika la Hifadhi za Taifa (Tanapa), Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, Wakala wa Huduma za Misitu, Taasisi ya Uhasibu na Chuo cha Usimamizi wa Fedha IFM.

# Vigogo Jiji Arusha wasimamishwa kazi

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MKURUGENZI wa Halmashauri ya Jiji la Arusha, Dk. Maulid Madeni, amewasimamisha kazi maofisa waandamizi wawili ili kupisha uchunguzi wa eneo la ujenzi stendi ya mabasi lililoko eneo la Bondeni City ekari 30.

Waliosimamishwa kazi kwa tuhuma hizo Mkuu wa Idara ya Mipango Miji na Ardhi, Dickley Nyato, na Ofisa Mipango Takwimu na Ufuatiliaji (Mchumi), Anna Mwambene.

Akizungumza jana na waandishi wa habari ofisini kwake, Dk. Madeni alisema baada ya halmashauri kubaini ubadhirifu wa Sh. bilioni 1.9 wa ununuzi wa eneo la ekari 29.5 lililoko Mtaa wa Oloresho, Kata ya Olasiti na kukataa kulipa fidia wananchi, waliamua kutafuta ekari 30 za bure eneo la Bondeni City.

"Eneo hili lilifanyiwa tathmini huko nyuma na muhtasari uliandikwa Februari 24, 2017 ukitutaka tulipe fidia Sh. bilioni 1.1, lakini mwaka huo huo Machi 6 ukaandikwa muhtasari mwingine ukitaka tulipe Sh. bilioni 1.9 sasa mimi nikakataa," alisema.

Alisema kutokana na mvutano huo, alifanya uchunguzi na kuwataka wakuu hao wa idara kumwandikia barua za kujieleza juu ya mamlaka ya kubadilisha uamuzi wa baraza walikopata na kuongeza kiasi hicho cha fedha.

Kwa mujibu wa Dk. Madeni, waliandika barua zao na kumpelekea Novemba 19, mwaka huu, lakini baada ya kuzisoma hakuridhika na sababu zao na kuwasimamisha kazi kupisha uchunguzi zaidi dhidi yao.

Alisema watumishi hao na yeye waliitwa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi) jijini Dar es Salaam, lakini cha kushangaza walidanganya kikao hicho kuwa eneo la Bondeni City halina hati kwa madai kuwa iliyopo imeshaisha muda wake kutokana na kutolewa Aprili 6, 1956 na ukomo wake ulikuwa Oktoba 30, 1982 na kushauri halmashauri kutonunua.

"Kwa makusudi kabisa wakati wakijua eneo hili bado lina hati iliyotolewa mwaka 1949 ya miaka 96 ambayo itaisha mwaka 2048, walifanya hili ili kuhalalisha ubadhirifu wao wa halmashauri inunue eneo walilokataa la Sh. bilioni 1.9 walizoongeza kinyemela.

Kutokana na uamuzi huo, alisema ofisi ya Nyato itashikiliwa na Saruni Lukumay na Idara ya Mipango, Takwimu na Ufuatiliaji ya Mwambene itashikiliwa na Mathias Sindika.

Alimwamuru Mwambene kuripoti ofisi za mwajiri wake mara mbili kwa wiki na hataruhusiwa kutoka nje ya mji wa Arusha.


THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
SUMMONS FOR FILING WRITTEN STATEMENT OF DEFENCE
(Order V Rule I (b) CPC)
IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF MTWARA
AT MTWARA
CIVIL CASE NO. 21 OF 2019
BAHATI SUGILE.....................PLAINTIFF
VERSUS
ADILI HATIBU & ANOTHER.........DEFENDANT

TO: KHAMISI ALLY ABDALAH

Whereas the above named Plaintiff (s) has have instituted a suit against you upon the claim, the particulars of which are set out in the annexed copy of the plaint.

YOU ARE HEREBY NOTIFIED that you must file your WRITTEN STATEMENT OF DEFENCE in duplicate within twenty one days of service of this notice upon you. If there are more than one Plaintiffs, additional copies of your written statement of defence must be filed sufficient for service on each of the Plaintiffs. If there are more Defendants than one and the defence is not a joint defence, there must be filled sufficient copies for service on each of the other Defendants.

TAKE NOTICE that the case also has been fixed for mention on the 26 of November, 2019 at 8:30 o'clock in the forenoon.

AND TAKE FURTHER NOTICE that if you default in filing of the written statement of Defence within the time specified the court may pronounce judgment against you.

GIVEN UNDER MY HAND AND THE SEAL OF THE COURT this 7 day of November, 2019.

115531302



THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
SUMMONS FOR FILING WRITTEN STATEMENT OF DEFENCE
(Order V Rule I (b) CPC)
IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF MTWARA
AT MTWARA
CIVIL CASE NO. 21 OF 2019
BAHATI SUGILE.....................PLAINTIFF
VERSUS
ADILI HATIBU & ANOTHER..................DEFENDANT

TO: ADILI HATIBU

Whereas the above named Plaintiff (s) has have instituted a suit against you upon the claim, the particulars of which are set out in the annexed copy of the plaint.

YOU ARE HEREBY NOTIFIED that you must file your WRITTEN STATEMENT OF DEFENCE in duplicate within twenty one days of service of this notice upon you. If there are more than one Plaintiffs, additional copies of your written statement of defence must be filed sufficient for service on each of the Plaintiffs. If there are more Defendants than one and the defence is not a joint defence, there must be filled sufficient copies for service on each of the other Defendants.

TAKE NOTICE that the case also has been fixed for mention on the 26 of November, 2019 at 8:30 o'clock in the forenoon.
AND TAKE FURTHER NOTICE that if you default in filing of the written statement of Defence within the time specified the court may pronounce judgment against you.

GIVEN UNDER MY HAND AND THE SEAL OF THE COURT this 7 day of November, 2019.

115531302



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA,

TANGAZO

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa kati ya **tarehe 26/11/2019** mpaka tarehe **29/11/2019** kampuni ya **BONITE BOTTLERS LTD** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **HOLILI BORDER** kuelekea **SHIRI MATUNDA INDUSTRIAL AREA** kupitia **MOSHI MJINI** gari hilo lenye namba za usajili:

   **Truck KBZ 903A**
   **Trailer ZD 4287**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:
   Urefu - mita 5.2
   Upana - mita 3.1
   Kimo - mita 22
3. Njia itakayotumika: **HOLILI hadi SHIRI MATUNDA INDUSTRIAL AREA** kupitia MOSHI MJINI,

   Gari zitasafiri muda wa mchana tu (kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12.00 jioni)

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.**



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA,

Tarehe 18/04/2019

TANGAZO

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya **ALHAMISI tarehe 28/11/2019** kampuni ya **FAMARI INVESTMENT** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka TUNDUMA kuelekea DAR ES SALAAM, gari hilo lenye namba za usajili:

   **T 366 DLQ/ T 944 DPF**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:
   Urefu - mita 21
   Upana - mita 3.00
   Kimo - mita 4.6
3. Njia itakayotumika: **TUNDUMA hadi DAR ES SALAAM kupitia VIGWAZA.**

   Gari zitasafiri muda wa mchana tu (kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12.00 jioni)

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.**

215532102

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

MATANGAZO MCHANGANYIKO

**NIPASHE NI JIBU LAKO**

NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO
KWA BEI NAFUU SANA
Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz,
au piga simu: 0767 223311

**2 ACRE YARD FOR RENT**

Facing New Julius Nyerere International Airport. Call: +255 754 375 967. Email: **gold@goldtz.net**

*Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku*

---

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M 1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**
**KATIKA MAHAKAMA YA WILAYA DODOMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI NA. 87 OF 2019**

**TANGAZO**

Ombi la **ANNA PETER MHANDO NA ABINEL PETER MHANDO** kuteuliwa msimamizi wa mirathi ya marehemu PETER ABINEL MHANDO watu wote wanaodai kuwa na mahusiano wowote a mirathi ya marehemu huyo na wana nia ya kupinga au kuthibitisha uteuzi wa mwombaji wanaalikwa kufika mahakamani kuhudhuria kesi mnano Tarehe 06-12-2019 ili kuwasilisha mapingamizi yao au la kabla ya huyo muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo.

IMETOLEWA TAREHE 15/11/2019

115531702

---

**ROYAL RUNNER'S AND GENERAL SUPPLIES T. LTD &COURT BROKER**

**MNADA WA HADHARA**

KWA AMRI TULIYOPEWA NA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA DODOMA MJINI TUTAUZA KIWANJA KILICHOPO IPAGALA PLOT NO. 3 BLOCK D IPAGALA EAST. TAREHE 03/01/2020 SAA 4:00 ASUBUHI

**KWA MAWASILIANO ZAIDI. 0713913150.**

115531702

---

**KUPOTELEWA NA KADI MBILI ZA PIKIPIKI**

**SEBASTIAN KABANDIZE SIMON.**

Anatangaza kupotelewa na kadi mbili za pikipiki aina ya Sanya, zenye Namba: MC635CBD, chasis No. LK1PCKL16H1051433,Engine No. 162FMJ470515712 na Na. Namba. MC267CAS Chasis No: LKIPCKL16H1063002, Engine No: 162FMJ470515027. Kadi ziliibiwa, na aliripoti kituo cha polisi cha Bukoba tarehe 2/11/2019 na kupewa No: KAG/BUK/RB/489082/2019. Na KAG/BUK/RB/498843/2019.

Kwa yeyote atakayeiona haipeleke kituo cha polisi kilichoko karibu naye.
Au awasiliane naye. No: 0787460563.

115531402

---

**JOB VACANCY**

**F & B PHARMACY**

Looking for Registered Pharmacist urgently in Dar es salaam.

Send your credentials and applications to info.fandbpharmacy@gmail.com.

Requirements, Bachelor of Pharmacy and a registered member of the Pharmacy Council of Tanzania.

115531202

---

**KUPOTEA KWA KADI ZA BAJAJ**

WEMAELY ELIAZA MBWAMBO anatangaza kupotelewa na kadi za Bajaj zenye namba za usajili MC 463 APN na MC 504 APW (BAJAJ TVS).

Yeyote atakayeziona atoe taarifa kituo cha polisi.

Control No. 991088742989.

115532002

---

**KADI YA GUTA IMEPOTEA**

**ALAN ADRIAN MPIHIGWA** anatangaza kupotelewa na kadi ya guta yenye namba za usajili MC 252 AUN model KAPOR. Yenye chasis namba: LAPHDM708F0005302.

Yeyote atakaeiona anaombwa atoe taarifa kituo cha polisi,

Taarifa ya Polisi: MOR/MOR/RB/498914/2019.

2155325O2

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

Katika mahakama ya mwanzo
CHAMWINO MOROGORO
Usimamizi wa mirathi No;72/2019

Ombi la HAMIDA HAJI MSANGI Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu HANIFA MSANGI HAJI

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 11/12/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 25/11/2019

115532402

---

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO.95 OF 2019**
**In the matter of the Estate of the LATE CHARLE MCHANDE CHEJELE OF DODOMA CITY**

**And**

**In the matter of the Application for letters of Probate and Administration of estate by MELINA MCHANDE CHEJELE**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules)**

All persons claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letters ) is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before 26th day of Nove 2019.

Presented for filling this 21 day of November, 2019

115532202

---

**KUPOTEA KWA CHETI**



**ZAHARA SAIDI ADAMU** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba CS 16000252523 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **SHULE YA SEKONDARI MSAJE** mwaka 2016.


Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi:
**MS/RB/8202/2019.**

115531802

---

**KUPOTEA KWA CHETI**



**KASSIMU ALLY JONGO anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S2348/0022 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia SHULE YA SEKONDARI ILALA ISLAMIC mwaka 2008.**

**Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.**

**Taarifa ya polisi:**
**DAR/MSI/RB/500037/2019.**

115531902

---

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku

Nipashe
MWANGA WA JAMII

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI MICHEZO



# GUARDIOLA ASEMA CITY HAITAKATA TAMAA

**MANCHESTER,** England

PEP Guardiola amesisitiza Manchester City wamethibitisha kwamba kamwe hawatakata tamaa kwenye mbio zao za kuwania ubingwa wa Ligi Kuu dhidi ya Liverpool licha ya kupitwa pointi tisa.

City, ambao wamepitwa pointi moja na Leicester waliopo nafasi ya pili, waliifunga Chelsea mabao 2-1 Jumamosi na kujivuta nafasi ya tatu, wakati Liverpool waliendeleza rekodi ya kutofungwa msimu huu kwa ushindi dhidi ya Crystal Palace.

Guardiola ana imani kwamba, kikosi chake hakitapoteza imani, hasa baada ya kuwa klabu ya kwanza kwa kipindi cha muongo mmoja kuweza kutetea taji lao msimu uliopita baada ya kuongozwa na Liverpool kwa tofauti ya pointi saba, kabla ya kuwafikia na kuwapiku msimu uliopita.

"Presha pekee tutakayokuwa nayo ni pale tutakapopoteza mchezo wa Ligi Kuu. Si mara ya kwanza kwa Manchester City katika kipindi cha miaka 125 katika historia kwamba pengine wanaweza kupoteza kwenye Ligi Kuu," alisema Guardiola.

"Kama tutapoteza taji la Ligi Kuu tutakwenda kujaribu msimu ujao, hatukukata tamaa msimu uliopita na ndio sababu tulishinda tena. Pengine tunakwenda kupoteza, lakini timu hii kamwe haitakata tamaa. Timu hii inajaribu na ndio maana tuliifunga Chelsea.

"Kama una shaka, basi msimu uliopita tusingeweza kufanya kile tulichokifanya na kutwaa taji. Baada ya kushinda pointi 100, kushinda mataji manne, hilo halijawahi kutokea hapo kabla."

# Solskjaer alia na uzoefu Man United

**MANCHESTER,** England

OLE Gunnar Solskjaer amesema kukosa uzoefu kwa wachezaji wake vijana na kutokujua namna gani ya kushinda kwenye hali fulani, baada ya kuishuhudia Manchester United ikitoka nyuma kwa mabao mawili na kupata sare ya 3-3 dhidi ya Sheffield United juzi, ugenini.

Mabao kutoka kwa kinda wa miaka 19, Brandon Williams, Mason Greenwood mwenye umri wa miaka 18 na Marcus Rashford mwenye miaka 22, walibadilisha upepo kwenye dimba la Bramall Lane wakati United ilipoongoza kwa muda, lakini hilo halikumzuia Solskjaer kulaumu kiwango walichoonyesha kipindi cha kwanza.

Kufungwa kungeongeza presha kwa Solskjaer, ambaye amepata ushindi mara mbili tu kwa United katika mechi nane za Ligi Kuu zilizopita na mshambuliaji huyo wa zamani wa United alielezea kukosekana kwa kujiamini kwa wachezaji hao.

"Katika soka, unatakiwa na kushinda mchezo na hatukuwa na uwezo wa kushinda baada ya dakika 70," alisema Solskjaer akiwaambia waandishi wa habari.

"Vijana ni chipukizi na si kwamba wanakosa uwezo; pengine ni kutojiamini. Andreas (Pereira) na Fred kwenye safu ya kiungo hawakuweza kucheza pamoja hapo kabla, lakini kwa jinsi walivyokuja baada ya (Sheffield United) kufunga la pili, hakika ilikuwa na hamasa kubwa.





# *Aubameyang agomea mkataba mpya Arsenal*

**LONDON,** England

MSHAMBULIAJI wa Arsenal, Pierre-Emerick Aubameyang ameripotiwa kwamba, amegoma kuongeza mkataba mpya pale kwenye dimba la Emirates, kwa mujibu wa ESPN.

Huku taarifa nyingine zikisema kwamba, ananyatiwa na miamba wa Ligi Kuu ya Hispania, Barcelona.

Nyota huyo wa kimataifa wa Gabon ana mkataba na Arsenal mpaka mwaka 2021, lakini hana mpango wa kuongeza mkataba mpya na Arsenal inaweza kulazimika kumuuza mwishoni mwa msimu huu kama hataongeza mkataba.

Aubameyang anaona Arsenal haina mwelekeo wa kushiriki Ligi ya Mabingwa Ulaya na yeye ni mmoja kati ya wachezaji wanaoibeba klabu hiyo kwa kufunga mabao mengi.

Inadaiwa Barcelona inamuona Aubameyang mwenye umri wa miaka 30, kama mshambuliaji wa kutoa upinzani kwa Luis Suarez ambaye anaweza kuondoka mwishoni mwa msimu huu baada ya kuanza kupungua kwa makali yake.

# Kane: Mourinho ataipa taji Tottenham

**LONDON,** England

HARRY Kane anaamini Jose Mourinho anaweza kutengeneza tofauti kwa Tottenham na kuweza kuwasaidia kumaliza ukame wa miaka 11 bila taji.

Katikati ya wiki iliyopita, Spurs ilimtimua Mauricio Pochettino na ndani ya saa 12 nafasi yake ikachukuliwa na Mourinho.

Mourinho, alirudi kwenye benchi la ukocha miezi 11 baada ya kuwa nje, na akaiongoza timu hiyo kupata ushindi wa mabao 3-2 dhidi ya West Ham Jumamosi, ukiwa ni mchezo wa kwanza kwa Spurs kushinda ugenini kwenye Ligi Kuu tangu Januari 20.

Pamoja na kazi nzuri aliyoifanya Pochettino kuiwezesha Spurs kuwa moja ya timu bora nchini England, miaka yake mitano na nusu aliyokaa hapo hakuweza kutwaa taji lolote, licha ya kucheza fainali mbili na nusu fainali mara tatu.

Kane hajawahi kukaa kimya kuhusu nia yake ya kutwaa taji pale Spurs na sasa ana matumaini kwamba, Mourinho ndio mtu anayeweza kumsaidia kufikia mafanikio hayo.

"Anataka kushinda. Amejithibitishia kuwa ni mshindi. Nimeshaweka wazi kwamba nipo kwenye hatua katika maisha yangu ya soko ambapo nataka kushinda mataji," alisema Kane.

"Nimeshaweka wazi nataka kushinda kitu hapa na ni mwaka mkubwa kwangu mimi na wachezaji wenzangu."





# SARRI WALA HAJUTII BENCHI RONALDO

**TURIN,** Italia

MAURIZIO Sarri amesisitiza hakuna tatizo lolote baada ya kumpumzisha Cristiano Ronaldo wakati Juventus ikimenyana na Atalanta kwenye mchezo wa Ligi Kuu ya Italia, Serie A, licha ya 'Bianconeri' hao kutokuwa na kiwango cha kuvutia.

Ronaldo hakuchezeshwa Jumamosi huku akiendelea kujitazama tatizo lake la goti, na kutokuwapo kwake kulizua hisia kwa mashabiki wengi, hadi Gonzalo Higuain alipofunga mara mbili na Paulo Dybala kufunga moja na kuiwezesha kutoka nyuma na kupata ushindi wa 3-1.

Sarri, ambaye alipamba vichwa vya habari wakati alimpomtoa nje Ronaldo kwenye mchezo dhidi ya AC Milan kuelekea kwenye mapumziko ya mechi za kimataifa, anatumaini kumtumia mchezaji huyo wa zamani wa Real Madrid katika mchezo dhidi ya Atletico Madrid kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, kesho Jumanne.

Hata hivyo, alielezea kwamba hakukuwa na tatizo lolote kwa kumuacha mshambuliaji huyo nje kwenye mchezo dhidi ya Atalanta.

"Natumaini atarudi kwenye mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya Jumanne (leo). Ana matatizo kidogo ambayo yalionekana wakati wa mazoezi," alisema Sarri akiiambia Sky Sport Italia.

"Mengi yatategemea na jinsi atakavyojihisi, kuchoka na anahitaji muda wa kupumzika. Alijihisi na alikubali, lilikuwa jambo zuri kwa sasa kumpumzisha ili apate muda zaidi wa kujisikilizia goti lake.

"Nilikuwa na furaha kumpumzisha, na hilo lilikuwa jambo muhimu zaidi kwetu kuhakikisha kwamba anapata wakati mzuri wa kupumzika na kujisikilizia."



# Kante afunguka alivyoikataa PSG

**LONDON,** England

MCHEZAJI N'Golo Kante amesema kwamba alikataa ofa kutoka kwa Klabu ya Paris Saint-Germain kwa sababu ana furaha pale Chelsea.

Mabingwa hao wa Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1, PSG kwa muda mrefu wamekuwa wakihusishwa na kutaka kumsajili Mfaransa huyo na iliripotiwa kwamba walijaribu kumsajili baada ya kuwa na kiwango cha kuvutia kwenye Kombe la Dunia mwaka 2018.

Usajili wake ulishindikana na Kante, ambaye anachukuliwa kama mmoja wa viungo bora kwenye Ligi Kuu ya England, kwa sasa yupo kwenye msimu wake wa nne pale Stamford Bridge.

Alisaini mkataba mpya wa miaka minne na klabu hiyo Novemba mwaka 2018 na hana mpango wa kuondoka kwa sasa.

"Kuna wakati hujui kwa uhakika wapi unapotaka kwenda, lakini unajua kile ambacho tayari unacho," alisema Kante akiiambia Canal+ wakati alipoulizwa kuhusu mpango wake wa kutakiwa PSG.

"Nilijua nipo Chelsea na nilijihisi vizuri hapa Chelsea. Juu ya hilo, yalikuwa maamuzi ya soka.

"Nilijihisi vizuri jijini London na nilijihisi furaha kwa mradi unaoendelea hapa na kwa hiyo nina furaha kukaa hapa."

Kante alijiunga na Chelsea mwaka 2016 baada ya msimu mmoja na Leicester City, ambako alishinda taji lake moja la Ligi Kuu kati ya mataji yake mawili.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28, alifunga bao lake la tatu msimu huu kwa Blues hao wakati wakichapwa 2-1 na Manchester City juzi, Jumamosi.

%%%%%%

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# KLOPP KWA VAN DIJK, MBAPPE KWA MESSI

●●● Ni kuhusu nani anastahili Ballon d'Or mwezi ujao, kila mmoja atoa sababu huku...

**LIVERPOOL,** England

WAKATI Kocha wa Liverpool, Mjerumani Jurgen Klopp akisema Virgil van Dijk anapaswa kumpiku Lionel Messi na kutwaa tuzo ya Mchezaji Bora wa Mwaka ['Ballon d'Or'] mwezi ujao, mshambuliaji wa Paris Saint-Germain, Kylian Mbappe amesema kwake anayestahili mwaka huu ni straika huyo wa Barcelona.

**Beki wa kimataifa wa Uholanzi, Van Dijk amekuwa na mwaka mzuri na Liverpool, akiwasaidia 'Wekundu' hao kutwaa Kombe la Ligi ya Mabingwa Ulaya Juni mwaka huu.**

Na ilibaki kidogo watwae ubingwa wa Ligi Kuu England msimu uliopita, lakini kwa sasa wanaongoza katika mbio hizo baada ya kutopoteza mechi yoyote hadi sasa msimu huu.

Klopp anaweza kuona ni kwa nini nyota huyo wa Barcelona, Messi ataweza kuwa chaguo maarufu katika tuzo hiyo binafsi, kwa sababu ya mafanikio yake kikazi.

Lakini badala ya kumpa Messi tuzo ya Ballon d'Or kwa mara ya sita, Klopp anaamini kuna sababu ya msingi kwa beki wa Liverpool kuondoka na tuzo hiyo pale jijini Paris Desemba 2, mwaka huu. Kiungo wa Real Madrid, Mcroatia Luka Modric alikuwa mshindi wa tuzo hiyo mwaka jana, ambayo hutolewa kwa mwaka na Jarida la Soka la Ufaransa.

Klopp alisema: "Kama utampa Ballon d'Or mchezaji bora wa kizazi hiki, basi utakuwa ukimpa mara zote Lionel Messi, hivyo ndivyo ilivyo.

"Lakini kama utampa mchezaji bora wa msimu, basi alikuwa ni Virgil van Dijk. "Hivyo, sijui sahihi itafanyaje kazi, lakini hivyo ndivyo ninavyoona.

"Kama ni kwa ajili ya mchezaji bora wa wote, basi ni Lionel. Mchezaji bora wa msimu, ni Virgil. Tutaona."

Lakini kwa upande wa nyota wa kimataifa wa Ufaransa, Mbappe ambaye alimaliza nafasi ya nne kwenye kinyang'anyiro cha Ballon d'Or 2018, na kisha kutwaa tuzo ya Kopa Trophy, inayotolewa kwa mchezaji bora mwenye umri chini ya miaka 21.

Hiyo ikiwa ni baada ya kufunga mabao 33 katikia mechi 29 za Ligue 1 alizowachezea mabingwa hao wa Ufaransa katika msimu wa 2018-19, wakati huu akiwa ameanza mechi tano tu msimu huu na kufunga mabao matano, Mbappe anaona anayestahili Ballon d'Or ni Messi.

"Kwa msimu binafsi ni [Messi] alikuwa bora mwaka huu. Mara nyingine ninahofu," Mbappe aliendelea. "Ni muoga, kama utashindwa kama mchezaji, unakuwa na hofu, na wakati unapopoteza katika mechi kubwa, swali ni, huu ndiyo mwisho wake? Ilikuwa vizuri, lakini sasa imekwisha!

"Lakini haidumu muda mrefu, kwa sababu kitu kizuri kuhusu soka ni kwamba hauna muda mrefu wa kufikiri."

## ZISIKUPITE

### SANCHO KUITOSA UNITED

MANCHESTER United inamuwinda Jadon Sancho, 19, lakini amesisitiza hatazami uwezekano wa kuondoka Borussia Dortmund na badala yake winga huyo wa England anasubiri kuendelea kubaki hapo Ujerumani licha ya kujihisi kama "mbuzi wa kafara" kwa kiwango kibovu kinachoonyeshwa na timu hiyo. ***(Athletic via Metro)***

### BENITEZ ATAJWA WEST HAM

CHRIS Hughton na Rafael Benitez wapo katika mstari wa kwenda kuinoa West Ham kama kocha Manuel Pellegrini atatimuliwa, wakati huu klabu hiyo ikiwa imepoteza mechi saba. ***(Guardian)***

### ALLEGRI KUMRITHI EMERY

KOCHA mwingine aliyepo katika presha kubwa ya kutimuliwa kwa sasa ni wa Arsenal, Unai Emery, ambaye nafasi yake inatajwa kwamba inaweza kurithiwa na kocha wa zamani wa Juventus, Max Allegri pamoja na kocha msaidizi wa Manchester City, Mikel Arteta. ***(Mail)***

### ANCELOTTI KAMTOA MOURINHO

KOCHA wa Napoli, Carlo Ancelotti alikuwa katika orodha ya kurithi mikoba ya Mauricio Pochettino pale Tottenham, lakini alikuwa "ghali sana" na ndipo Spurs ikaamua kumgeukia Jose Mourinho badala yake. ***(Mail)***

### AZIANIKA LIVERPOOL, ARSENAL

WINGA wa Bournemouth, Ryan Fraser amekuwa akihusishwa na Everton, Liverpool na Arsenal wakati mkataba wake utakapomalizika majira ya joto yajayo, lakini winga huyo mwenye umri wa miaka 25, hajakaribia kufanya uamuzi juu ya mustakabali wake wa baadaye. ***(Mirror)***

### BALOTELLI ASHUKIWA BRESCIA

MSHAMBULIAJI wa Brescia, Mario Balotelli, 29, amekuwa akiambiwa aonyeshe "shahuku" zaidi kama anataka kupata nafasi ya kucheza. ***(Mail)***

### ENRIQUE KUMTEUA CASAS

KOCHA aliyerejea kuinoa Hispania, Luis Enrique, atamteua Jesus Casas kama msaidizi wake. ***(Marca - in Spanish)***

### SANCHEZ KUPELEKWA SOKONI

WEST Ham inajiandaa kumuuza kiungo Mcolombia Carlos Sanchez, 33, katika dirisha la Januari, wakati huu mchezaji huyo akijiandaa kuwa mchezaji huru majira ya joto yajayo. ***(Sun)***

### AKE AMULIKWA TOTTENHAM

TOTTENHAM imeelekeza macho yake kwa beki wa Bournemouth, Nathan Ake, 24, lengo likiwa Mholanzi huyo kumrithi Jan Vertonghen, ambaye mkataba wake unamalizika majira ya joto yajayo 2020. ***(Football Insider)***

### ARSENAL KUMKOSA UMTITI

ARSENAL inaweza kumkosa beki wa Barcelona, Samuel Umtiti, 26, kutokana na Mfaransa huyo kupendelea zaidi kurudi klabu yake ya zamani, Lyon kama ataamua kuondoka Nou Camp. ***(L'Equipe - in French)***

### YAMTAZAMA BADIASHILE

NEWCASTLE United inamfuatilia beki wa Monaco, Benoit Badiashile baada ya mashushu wake kumtazama mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 18 akichezea klabu yake dhidi ya Bordeaux. ***(Newcastle Chronicle)***

HABARI MICHEZO

### MSIMAMO LIGI KUU BARA



| | P | W | D | L | F | A | PTS |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. Simba | 10 | 8 | 1 | 1 | 19 | 3 | 25 |
| 2. Kagera Sugar | 11 | 7 | 2 | 2 | 16 | 9 | 23 |
| 3.TZ Prisons | 12 | 4 | 8 | 0 | 14 | 9 | 20 |
| 4. Lipuli | 11 | 5 | 3 | 3 | 19 | 12 | 18 |
| 5. Alliance | 11 | 4 | 5 | 2 | 10 | 8 | 17 |
| 6. Azam | 8 | 5 | 1 | 2 | 8 | 4 | 16 |
| 7. Polisi Tanzania | 10 | 5 | 1 | 4 | 11 | 10 | 16 |
| 8. Mtibwa Sugar | 12 | 4 | 4 | 4 | 10 | 11 | 16 |
| 9. Namungo | 11 | 5 | 1 | 5 | 10 | 11 | 16 |
| 10. Ruvu Shooting | 12 | 4 | 3 | 5 | 9 | 13 | 15 |
| 11. Coastal Union | 11 | 4 | 2 | 5 | 11 | 10 | 14 |
| 12. Mbao | 12 | 3 | 5 | 4 | 9 | 10 | 14 |
| 13. Yanga | 6 | 4 | 1 | 1 | 9 | 6 | 13 |
| 14. JKT Tanzania | 10 | 3 | 3 | 4 | 8 | 10 | 12 |
| 15. Mwadui | 12 | 2 | 6 | 4 | 8 | 11 | 12 |
| 16. Biashara Utd | 11 | 2 | 3 | 6 | 6 | 11 | 9 |
| 17. KMC | 9 | 2 | 2 | 5 | 6 | 10 | 8 |
| 18. Mbeya City | 11 | 1 | 5 | 5 | 7 | 17 | 8 |
| 19. Ndanda | 10 | 1 | 4 | 5 | 6 | 11 | 7 |
| 20. Singida Utd | 12 | 1 | 4 | 7 | 5 | 15 | 7 |

# WANAWAKE CECAFA WATAKA KLABU BINGWA WANAWAKE

**Na Somoe Ng'itu**

BAADA ya kumalizika kwa mashindano ya Kombe la Chalenji jana, viongozi wanawake kutoka nchi za Afrika Mashariki na Kati wameomba mabosi wao kuanzisha michuano ya ngazi za klabu kama ilivyo kwa wenzao wanaume ambayo maarufu huitwa Kombe la Kagame.

Akizungumza kwa niaba ya wenzake, Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Soka Kenya (FKF) na Mkuu wa msafara wa timu ya nchi hiyo, Doris Petra, alisema wanaamini michuano hiyo itaendelea kuwapa nafasi ya kuwaimarisha zaidi wachezaji wanawake.

**Petra alisema pia itakuwa ni programu nyingine ya kuwajenga wachezaji wanawake ambao kwa sasa wameanza kuonyesha ushindani ndani ya ukanda huu wa Afrika Mashariki na Kati.**

"Tunasema sasa wanawake tuko tayari kushindana katika ngazi ya klabu, tunacheza ligi na tungependa kuona klabu za wanawake zinashindana, kama tunavyoona Gor Mahia watapambana na Yanga, Simba au APR," alisema Petra.

Aliongeza kuwa wanashukuru kuona kwa mara ya kwanza mwaka huu ndani ya Cecafa wanaendesha mashindano mawili ya wanawake na hii ni dalili njema kwamba viwango vya wachezaji vitaimarika na kuongeza hamasa kwa nyota chipukizi.

"Leo (jana), tumemaliza mashindano ya wakubwa, mwezi ujao tutakutana Uganda katika mashindano mengine ya umri chini ya miaka 17, hii ni njia nzuri ya kukuza soka la wanawake, njia sahihi ya kuendeleza vipaji, naamini tutafika mbali siku si nyingi," Petra aliongeza.

Mashindano ya Kombe la Chalenji kwa wasichana wa umri chini ya miaka 17, yanatarajiwa kushirikisha nchi saba ambazo ni Uganda, Burundi, Tanzania Bara, Djibouti, Zanzibar, Eritrea na Ethiopia.



Mchezaji wa Kilimanjaro Queens, Happynes Mwaipaja, akiwatoka wachezaji wa Kenya katika mechi ya fainali Kombe la Cecafa kwa Wanawake iliyopigwa Uwanja wa Chamazi jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Uganda waishukuru TFF ikimaliza ya tatu Cecafa

**Na Shufaa Lyimo**

TIMU ya Taifa ya Wanawake Uganda, imeshika nafasi ya tatu kwenye michuano ya Afrika Mashariki na Kati (Cecafa Challenge Cup) kwa Wanawake baada ya kuifumua Burundi kwa mabao 2-0.

Katika mchezo huo uliokuwa na ushindani mkali, hadi kipindi cha kwanza kinamalizika timu zote zilitoka bila kufungana.

Mabadiliko yaliyofanywa na Uganda katika kipindi cha pili kwa kumtoa Ikwaputa Fazila na kumuingiza Nababi Amina, yalionekana kuinufaisha kufuatia kupata bao la kuongoza katika dakika ya 60 kupitia kwa Nababi Amina.

Mchezo uliendelea kuwa mkali huku Burundi ikitaka kusawazisha, lakini mambo yazidi kuwaendea kombo baada ya Uganda kuandika bao la pili dakika ya 81 kupitia kwa Nalujja Shamira.

Baada ya mchezo huo kumalizika Kocha Mkuu wa timu ya Uganda, Faridah Bulega mbali na kuwapongeza wachezaji wake, alisema mechi hiyo ilikuwa na upinzani mkali.

Aidha, alilishukuru Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), kwa kuhakikisha mashindano hayo yanafanyika kwa amani na utulivu wa hali ya juu.

"Mchezo wa leo ulikuwa mzuri na wenye ushindani mkubwa, nashukuru tumepata nafasi ya tatu,"alisema Faridah huku akifafanua kuwa alitamani kuona wanacheza fainali, lakini mambo yalikwenda tofauti jambo ambalo aliahidi kulifanyia kazi kwenye mashindano yajayo.

Kwa upande wa Kocha Msaidizi wa Burundi, Ininahhazwe Belyse, alisema mchezo ulikuwa mzuri na kwamba licha ya kufungwa wachezaji wake walicheza vizuri.

"Tunashukuru kwa hatua tuliyofika, tangu mwanzo tulitarajia kushika hata nafasi ya tatu, lakini bahati haikuwa upande wetu," alisema Belyse.

# Kocha Prisons alia na washambuliaji

**Na Shufaa Lyimo**

KOCHA Mkuu wa timu ya Tanzania Prisons, Adolf Richard, amesema tatizo la safu yake ya ushambuliaji kushindwa kutumia nafasi wanazozitengeneza ndilo linalomuumiza kichwa kwa sasa.

Akizungumza na Nipashe, kocha huyo alisema atahakikisha anafanyia kazi tatizo hilo, ili kuiepusha timu hiyo na janga la kushuka daraja.

"Safu yangu ya umaliziaji imekuwa tatizo kwa sababu mara nyingi tunapokuwa uwanjani wachezaji wangu wanapata nafasi za wazi, lakini wanashindwa kuzitumia," alisema kocha huyo.

Alisema itamlazimu kufanya kila njia ili tatizo hilo limalizike katika timu yake ambayo ana lengo la kuifikisha mbali zaidi.

"Lengo ni kuifikisha mbali timu yangu kwa kutatua matatizo yote ili iendelee kuwapo kwenye Ligi Kuu," alisema.

Aliwaomba mashabiki wao waendelee kuisapoti timu hiyo ambayo ipo nafasi ya tatu kwenye msimamo wa Ligi Kuu ikiwa na alama 20 baada ya kushuka dimbani mara 12 ikiwa ni michezo miwili mbele dhidi ya vinara Simba wenye pointi 25, huku Kagera Sugar yenye alama 23 ipo nafasi ya pili baada ya kushuka dimbani mara 11 msimu huu.

# Michezo

Jumanne Novemba 26, 2019

Nipashe






Klopp kwa Van Dijk, Mbappe kwa Messi UKURASA 30


**MABINGWA...**



Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu (kulia), akimkabidhi Kombe la Cecafa kwa Wanawake, nahodha wa Kenya, Dorcas Nixon, baada ya kuutwaa ubingwa huo kwa kuifunga Kilimanjaro Queens ya Tanzania Bara mabao 2-0 kwenye mechi ya fainali iliyopigwa Uwanja wa Chamazi jijini Dar es Salaam jana. Anayeshuhudia ni Rais wa TFF, Wallace Karia. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Kenya yawanyima Kili Queens rekodi

**Na Adam Fungamwango**

TIMU ya soka ya Wanawake ya Tanzania Bara, Kilimanjaro Queens, imeshindwa kuweka rekodi ya kulitwaa jumla Kombe la Chalenji kwa Wanawake wa Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati (Cecafa) baada ya kukubali kipigo cha mabao 2-0 kwenye mechi ya fainali iliyochezwa Uwanja wa Azam Complex, Chamazi jijini Dar es Salaam jana.

Umati uliofurika kwenye uwanja huo, haukutosha kuifanya timu hiyo kutimiza azma yake ya kutwaa kombe hilo kwa mara nyingine tena kama ilivyolibeba mara mbili wakati michuano hiyo ilipofanyika nchini za Uganda na Rwanda.

Mwiba kwa Kili Queens alikuwa ni straika mtokea benchi, Jentrix Shikangwa aliyeibuka mfungaji bora kwa kufunga jumla ya mabao 10, ambaye aliingia kipindi cha pili na kufunga mabao yote mawili dakika ya 70 kwa penalti na kisha dakika ya 87 kwa mkwaju mkali kutoka wingi ya kulia.

Kenya inaondoka na kombe huku ikiwa si tu kwamba haijapoteza mechi, lakini pia bila kuruhusu bao lolote kwenye michuano hiyo wakati Kilimanjaro Queens nayo pia hayo ni mabao yake ya kwanza kuruhusu tangu kuanza kwa michuano hiyo msimu huu.

# AUSSEMS KUTIMULIWA MJADALA MZITO SIMBA

## ●●● Kuwekwa kitimoto leo, makocha wa zamani wa klabu hiyo wapinga asitimuliwe, wasema...

**Na Somoe Ng'itu**

WAKATI mbivu na mbichi kuhusu nafasi ya Kocha Mkuu wa Simba, Mbelgiji Patrick Aussems, kuendelea kuwafundisha mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara inatarajiwa kujulikana leo jijini Dar es Salaam, kumezuka mjadala mzito kutoka kwa wadau wa soka wengi wakiwa wa klabu hiyo wakitaka tofauti zilizopo zimalizwe na kocha huyo aendelee kuinoa timu hiyo.

**Aussems anatarajia kuhojiwa na Kamati ya Maadili ya Klabu ya Simba kutokana na kudaiwa kuondoka nchini na kwenda Afrika Kusini kufanya mazungumzo na timu nyingine hali ya kuwa kanuni za mkataba wake bado zinambana kufanya hivyo.**

Kocha huyo aliondoka nchini kwa muda wa siku tatu na kudai anakwenda kwao kutokana na kukabiliwa na matatizo ya kifamilia, baada ya kuujulisha uongozi wa klabu kwa barua pepe, huku akiahidi kurejea tena kwenye majukumu yake ya kila siku.

Taarifa zilizopatikana jijini zinasema kuwa Simba ilichukizwa na kitendo hicho na kueleza kwamba kilichofanywa ni utovu wa nidhamu.

"Tuliamua kumuacha ili kuweka nguvu katika mechi dhidi ya Ruvu Shooting ambayo ilikuwa mbele yetu na kuamua kuliweka suala lake kiporo, kila kitu kitajulikana Jumanne atakapokutana na Kamati ya Maadili," kilisema chanzo chetu.

Hata hivyo, baada ya mechi dhidi ya Ruvu Shooting ambayo Simba ilishinda 3-0, Aussems, alilazimika kupewa ulinzi mkali na askari kufuatia kuzongwa na mashabiki wa klabu hiyo wakitaka kupiga naye picha huku wengi wakieleza asitimuliwe.

Lakini alipoulizwa jana kuhusu mustakabali wa kocha huyo, Mtendaji Mkuu wa Simba, Senzo Mazingiza alisema yote yanayosemwa kuhusu Aussems kwamba anaondoka Simba ni uvumi tu.

"Aussems bado ni kocha wa Simba, yote yanayosemwa ni uvumi kama kuna taarifa itatolewa rasmi, kinachoendelea nasema ni uvumi tu," Mazingiza alisema.

Lakini wakizungumza kwa nyakati tofauti jana, aliyekuwa mchezaji na kocha wa zamani wa klabu hiyo, Abdallah "King" Kibadeni, yeye alisema: "Kiufundi bado sijaona tatizo, labda kama ni nje ya hapo na kama kuna mengine tofauti na hapo inabidi watueleze na sisi tuyajue ndiyo tunaweza kusema kwa kuwa timu inaongoza ligi na inacheza vizuri."

Kwa upande wake mchezaji na Kocha wa zamani wa Simba, Jamhuri Kihwelu 'Julio', yeye alisema makocha kweli wanaajiriwa ili wafukuzwe, lakini kwa sasa haoni sababu ya timu hiyo kumfukuza Aussems.

"Ninachoweza kusema mimi ndani ya Simba kuna baadhi ya watu si wa mpira hapo ndipo tatizo lilipo, suala la kumfukuza Aussems huenda tayari kuna watu wanataka kutumia mwanya huo kufanya mambo yao, lakini itakuwa ni tatizo kubwa kwa timu kumfukuza kwa sasa maana kuajiri kocha mwingine kwa sasa kutawachanganya wachezaji.

"Timu inafanya vizuri, kocha mwingine akija atakuja na falsafa zake, hivyo unaweza kujikuta unawavuruga wachezaji kabisa," alisema Julio.

Naye mwanasoka nguli wa zamani, Kenny Mwaisabula, yeye alisema: "Labda kama kuna mambo mengi madogomadogo basi wayarekebishe timu isonge mbele, lakini kwa upande wa kocha sioni tatizo maana kama ni kucheza vizuri inacheza na inaongoza msimamo wa ligi, sijui wanataka nini kwa sasa."

Habari zaidi zinaeleza kuwa makocha kutoka sehemu mbalimbali duniani wanaendelea kutuma maombi kwa ajili ya kutaka kuchukua mikoba ya kocha huyo ambaye msimu uliopita aliifikisha Simba kwenye hatua ya robo fainali ya mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

"Kinachoangaliwa zaidi ni kanuni za mkataba wake, amefanya kinyume na vipengele vilivyopo, ametuvunjia heshima, kwa kifupi tayari mchakato wa kupata kocha mpya umefikia asilimia 70," kilieleza chanzo chetu.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >